**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Kamal Basha Pandu | Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo. |
| 2.Mhe. Ali Mzee Ali | Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais. |
| 3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe. |
| 4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge. |
| 5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni. |
| 6.Mhe. Haji Omar Kheri | Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu. |
| 7.Mhe. Soud Yussuf Mgeni | Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Wawi. |
| 8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani. |
| 9.Mhe. Hamza Hassan Juma | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura. |
| 10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais. |

| | |
|---|---|
| 11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe. |
| 12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki | MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais. |
| 13. Mhe. Machano Othman Said | Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni. |
| 14.Mhe. Samia Suluhu Hassan | MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake. |
| 15.Mhe. Burhan Saadat Haji | MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni. |
| 16.Mhe. Asha Abdalla Juma | MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais. |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi. |
| 18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry | MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais. |
| 19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki. |
| 20.Mhe. Zainab Omar Moh'd | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake. |
| 21.Mhe. Idi Pandu Hassan | Mwanasheria Mkuu wa Serikali. |
| 22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Mzee Ali Ussi | Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani. |
| 24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari | Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu. |
| 25.Mhe. Khamis Jabir Makame | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni. |
| 26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole. |
| 27.Mhe. Tafana Kassim Mzee | Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini. |
| 28.Mhe. Omar Ali Shehe | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Chake-Chake. |
| 29.Mhe. Zakiya Omar Juma | "Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake. |
| 30.Mhe. Abass Juma Muhunzi | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Chambani. |
| 31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga. |
| 32.Mhe. Haji Faki Shaali | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Jimbo la Mkanyageni. |
| 33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake. |
| 34.Mhe. Hamad Masoud Hamad | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole. |

| | |
|---|---|
| 35.Mhe. Said Ali Mbarouk | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Gando. |
| 36.Mhe. Rashid Seif Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani. |
| 37.Mhe. Mohamed Ali Salim | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani. |
| 38.Mhe. Asaa Othman Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete. |
| 39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake. |
| 40.Mhe. Najma Khalfan Juma | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake. |
| 41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile. |
| 42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. |
| 43.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini. |
| 44.Mhe. Ali Denge Makame | Jimbo la Amani. |
| 45.Mhe. Ali Haji Ali | Jimbo la Mkwajuni. |
| 46.Mhe. Ali Moh’d Bakari | Jimbo la Tumbe. |
| 47.Mhe. Ali Suleiman Ali | Jimbo la Kwahani. |

| | |
|---|---|
| 48.Mhe. Ame Mati Wadi | Jimbo la Matemwe. |
| 49.Mhe. Ame Ussi Juma | Jimbo la Nungwi. |
| 50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake. |
| 51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila | Jimbo la Fuoni. |
| 52.Mhe. Ashura Abeid Faraji | Nafasi za Wanawake. |
| 53.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Nafasi za Wanawake. |
| 54.Mhe. Dadi Faki Dadi | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba. |
| 55.Mhe. Fatma Abdalla Tamim | Nafasi za Wanawake. |
| 56.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | Jimbo la Mji Mkongwe. |
| 57.Mhe. Haji Mkema Haji | Jimbo la Koani. |
| 58.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji | Uteuzi wa Rais. |
| 59.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani. |
| 60.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba. |
| 61.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope. |
| 62.Mhe. Mkongwe Nassor Juma | Nafasi za Wanawake. |
| 63.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga | Jimbo la Chwaka. |
| 64.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja. |
| 65.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake. |
| 66.Mhe. Omar Ali Jadi | Jimbo la Kojani. |
| 67.Mhe. Pembe Juma Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja. |

| | |
|---|---|
| 68.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu | Jimbo la Muyuni. |
| 69.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake. |
| 70.Mhe. Said Khelef Ali | Jimbo la Bumbwini. |
| 71.Mhe. Salim Abdulla Hamad | Jimbo la Mtambwe. |
| 72.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni. |
| 73.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni. |
| 74.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde. |
| 75.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Nafasi za Wanawake. |
| 76.Mhe. Zahra Ali Hamad | Nafasi za Wanawake. |

**Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**.

## BARAZA LA SABA LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

### Kikao cha Kwanza – Tarehe 21 Januari 2009

*(Kikao kilianza saa 3.00 Asubuhi)*

### DUA

*Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua*

### TAARIFA YA SPIKA

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kwanza karibuni tena katika mkutano wetu wa kumi na nne, baada ya kuahirisha mkutano wa kumi na tatu. Kifungu cha 71(2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 toleo la mwaka 2003, inaeleza kwamba Spika wa Baraza la Wawakilishi atatoa taarifa rasmi kwa Baraza na kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, kuhusu kiti cha Mjumbe Mwakilishi kuwa wazi katika kutekeleza masharti ya kifungu cha 71(1).

Aidha, kifungu cha 6 cha kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2007 kinaeleza ifuatavyo.

"*Spika atatangaza katika Baraza kuhusu kifo cha mjumbe yoyote kinapotokea na pia atatoa taarifa ya kifo hicho kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, au Rais kwa kadri itakavyokuwa katika kiti cha mjumbe aliyefariki kuwa wazi".*

Waheshimiwa Wajumbe kwa kutekeleza matakwa na maelekezo ya vifungu hivyo vya Katiba na Kanuni nilivyovinukuu hapo awali, kwa huzuni na masikitiko makubwa natangaza mbele ya Baraza hili kwamba Mhe. Daudi Hassan Daudi Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Jimbo la Magogoni amefariki dunia. Mhe. Daudi Hassan Daudi alifariki dunia siku ya Ijumaa, tarehe 19 Disemba, 2008. Kwa hivyo kiti cha Mjumbe Mwakilishi cha Jimbo la Magogoni kipo wazi kuanzia tarehe hiyo.

Vile vile nawaarifu kwamba tayari nimeshatoa taarifa rasmi kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, ili kwa hatua zake kwa mujibu wa sheria, naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Baraza letu hili la wawakilishi la Zanzibar kutoa mkono wa pole kwa familia ya marehemu, ndugu, jamaa na marafiki, wananchi wa jimbo la Magogoni na waheshimiwa wajumbe wote wa

Baraza la Wawakilishi kwa kuondokewa na kipenzi chetu mwenzetu huyu Mhe. Daudi Hassan Daudi.

Waheshimiwa Wajumbe sote kwa pamoja tumuombe Mwenyezi Mungu atupe mioyo ya subra na tumuombee Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi Amin.

Sasa kutokana na taarifa hiyo nichukue nafasi hii kuwaomba tusimame kwa muda wa dakika moja ili tukumbuke kifo cha mwenzetu.

*(Hapa Baraza lilisimama kwa dakika moja kwa kukumbuka kifo cha Mhe. Daudi Hassan Daudi)*

**Mhe. Spika:** Katika mkutano wa Kumi na Tatu wa Baraza la Saba la Wawakilishi uliofanyika tarehe 15 Oktoba, 2008. Baraza lilipitisha miswada minne ya Sheria kama ifuatavyo.

1. Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Utozaji wa Kodi itakayojulikana kama Kodi ya Majengo na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

2. Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Shirika la Magazeti ya Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

3. Mswada wa Kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Barabara Zanzibar namba 2 ya mwaka 2000, pia ilipitishwa.

4. Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Nam. 2 ya mwaka 2005.

Kama inavyotakiwa chini kifungu cha 90(3) cha Kununi za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2007, naomba kutoa taarifa kwamba miswada hiyo imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Baada ya hayo nawashukuru sana waheshimwa wajumbe.

## HATI ZA KUWASILISHWA BARAZANI

**Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:**
Nakla za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 24 Oktoba,2008 naomba kuwasilisha.
**Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Habari Utamaduni na Michezo:**

Nakla ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Sensa na Filamu za Maonyesho ya mwaka 2009, na Mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. M wenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. (Mhe. Ali Suleiman Ali)** Mhe. Spika, nimesimama hapa kwa heshima kabisa naomba kuwasilisha Hati mezani kuhusu Mswada wa Sheria ya Kunzisha Bodi ya Sensa na Filamu za Monyesho na Mambo mengine yanayohusiana na hayo naomba kuwasilisha.

**Mhe. Waziri Kivuli na Naibu Waziri Kiongozi Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo:**Hotuba ya Maoni ya Upande wa Upinzani kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Sensa na Filamu za Maonesho na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

**Mhe. Spika,** nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Mwenyekiti na Mhe. Waziri kivuli kwa sababu marekebisho haya yalikuja ghafla jana, na kulikuwa hakuna muda wa kutosha, kwa hivyo nawashukuru sana kwamba wamemudu kuwasilisha hati mezani kwa mujibu wa taratibu za kanuni.

## MASWALI NA MAJIBU

### Nam. 45

### Usafishaji wa Mji na Vijiji, Zanzibar

**Mhe. Ali Suleiman Ali -** Aliuliza:

Nchi ya Rwanda imejiwekea utaratibu wa kila mwananchi kufanya usafi wa maeneo yote wanayoishi, Mjini na Vijijini, ikiwa ni pamoja na Madukani, Mikahawani, Masokoni, Hospitali, Skuli na sehemu nyenginezo.

(a) Kwa kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuwahamasisha wananchi wa Zanzibar kusafisha maeneo yao, Je. Mhe. Waziri, Wizara yako imechukua juhudi zipi katika kufanikisha suala hili.

(b) Je, ipo haja ya kuanzisha utaratibu wa kisheria utakaowalazimisha wananchi wa Zanzibar kudumisha usafi wa maeneo yao, na sio suala hili kufanywa na Baraza la Manispaa peke yake.

(c) Kama ipo, Ni lini Wizara yako itaandaa utaratibu huo.

**Mhe. Nchi Afii ya Waziri Kiongozi - Alijibu:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Swali lake Nam. 45 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabala sijajibu naomba kutoa maelezo kidogo halafu baadae uniruhusu nijibu swali lake. Mimi kwanza nimpongeze sana Mhe. Ali Suleiman Ali kwa kuweza kumtuma kwenda safari nje ya nchi na ile faida aliyoiona kule akaja kuandikia swali barazani. Nampongeza sana na nawaomba na waheshimiwa wengine wanapopata safari za nje, basi yale wanayoona kule ambayo yatasaidia nchi yetu, wakirudi watuletee ili na nchi yetu iweze kufaidika.

Mimi mwenyewe nilitembelea Rwanda na katika kwenda niliangalia suala hili hili la usafi, ambalo Mhe. Ali Suleiman aliloulizia, kimsingi siri ya mafanikio ya wenzetu wa Rwanda, kwanza wanatii sheria zilizotungwa na Bunge lao. Lakini kubwa zaidi, wenzetu sasa hivi wana utaratibu mzuri ambao wamejiwekea katika kuweka usafi katika mji wao, vitu ambavyo sisi kama Wazanzibari tunaoitakia mema nchi yetu, basi ilikuwa ni vizuri mambo mazuri tuliyoona kwa wenzetu na sisi tuweze kuyaiga. Wenzetu wana siku ambayo kila mwisho wa Mwezi wanafunga shughuli zote, na barabara zinafungwa, kuanzia saa 11.00 asubuhi mpaka saa 4.00, wenzetu wanashirikiana katika suala la usafi wa mazingira. Gari ambazo zinaruhusiwa ni gari za Majeshi, Polisi pamoja na Ambulance ambazo mara nyingi huwa zinatumika kwa dharura au gari za mabalozi.

Gari nyengine ambazo zinaruhusiwa kutembea, basi zinapewa kibali maalum na zinalipa kwa Baraza la Manispaa, kwa hivyo muda ule wote kuanzia asubuhi wananchi wote wa Rwanda wanahakikisha wanasafisha maeneo yao, na ndio maana leo nchi ya Rwanda ni nchi ambayo inapigiwa mfano katika nchi za Baraza la Afrika. Baada ya kutoa ufafanuzi huo, sasa naomba nimjibu swali lake kama hivi ifuatavyo.

(a) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuwahamasisha wananchi wa Zanzibar kusafisha maeneo yao. Katika kufanikisha kazi hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira (Idara ya Mazingira), imekuwa ikiishajiisha jamii juu ya kufanya usafi wa mazingira yanayowazunguka; kuendesha kampeni za usafi katika maeneo mbali mbali mijini na vijijini; pamoja na kuzifanyia tathmini Halmashauri za Wilaya juu ya utaratibu mzima wa udhibiti wa taka. Aidha, Serikali imeshaanza kazi ya kuliboresha Baraza la Manispaa kwa kulipatia vitendea kazi na kazi hii itaendelea kwa Halmashauri na Mabaraza ya Miji huko Pemba.

(b) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa ipo haja ya kuanzisha utaratibu wa Kisheria utakaolazimisha wananchi wa Zanzibar kudumisha usafi wa maeneo yao, na sio suala hili kufanywa na Baraza la Manispaa peke yake. Hata hivyo, haina maana kuwa kwa wakati huu hakuna utaratibu huo. Utaratibu uliopo hivi sasa unawalazimisha wafanya biashara kufanya usafi katika maeneo yao. Hivyo, tutazifanyia marekebisho kanuni za Halmashauri na badala ya kuwalazimisha wafanya biashara kudumisha usafi katika maeneo yao iwe kwa wananchi wote.

(c) Kazi ya kuzifanyia marekebsiho kanuni hizo inahitaji uangalifu mkubwa, ili kuepuka migongano baina ya Serikali na wananchi. Hivyo, ni matarajio ya Wizara yangu kuwa kazi hii ifanyike kwa haraka, lakini itahusisha kupata mapendekezo kutoka kwa wadau mbali mbali ikiwa ni pamoja na wananchi wenyewe katika utekelezaji wa sheria hii.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa hapa kwetu katika Manispaa zetu au Halmashauri zetu kuna taratibu za Manispaa kuwatolesha wafanya biashara mbali mbali shilingi mia mbili kwa siku, kwa ajili ya kuweka mazingira yetu safi au katika maduka yao na sehemu mbali mbali hata paki za magari. Lakini la kusikitisha ni kwamba fedha hizo si nyingi na athari yake ni kule kukosekana kile kilichokusudiwa ambao ni usafi.

Je. Mhe. Waziri hili kupitia Manispaa na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi ni mkuu wa shughuli za serikali, ana mpango gani wa kulifanyia maarifa na kuzungumza na watu wa Manispaa kwa kuwa watu wanalipa fedha zao na usafi haufanyiki na sasa ufanyike.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Kimsingi ni kweli Baraza la Manispaa linawatoza kibiashara hasa wenye maduka ada ya shilingi elfu sita kwa mwezi, kwa ajili ya kufanya usafi, lakini kimsingi suala hili la usafi ni suala la wafanya biashara wenyewe, sio suala la Manispaa. Nitatoa mfano hata kule Rwanda wafanyabiashara ikifika saa 11.00 maduka yao yote yanafungwa, wakishafunga wanafagia halafu zile taka wanazikusanya pembeni. Kwa hivyo, Baraza la Manispaa wao kazi yao ni kuja kuzichukua zile taka na kwenda kuziweka katika maeneo yanayohusika.

Hata Baraza la Manispaa la hapa, kuna sheria namba tatu ya mwaka 2005 ninayo pale. Baraza la Manispaa limepewa mamlaka ya kutengeneza kanuni ndogo ndogo na zipo ambazo zinaeleza kwamba, Baraza la Manispaa

litakwenda kuchukua taka zilizokusanywa. Sasa kama tutasema Manispaa wapite kufagia katika maduka yote, hawana uwezo wa wafanyakazi wa kuweza kufanya kazi katika kila duka. Lakini, suala la usafi wa mazingira hata hizi nyumba zetu, ipo sheria ya Manispaa ambayo inasema katika nyumba yako iliyokuzungumka zikikutikana taka, basi wewe unapigwa faini ya shilingi elfu sabiini. Kwa hivyo, sheria ile inamtaka mwananchi katika mazingira ya nyumba yake, mtu yoyote anayekuja kumchafulia na kumtupia taka anayo haki na yeye kumlazimisha kuzoa taka zile, vyenginevyo zile taka zikija zikikutikana, ina maana yeye ndio atakuja kupigwa faini.

Kwa hivyo, bado naendelea kusema sisi ni wawakilishi wa wananchi tujitahidi kuwashajihisha wananchi wetu wasafishe majumba yao, wafagie halafu zile taka wakazitupe katika maaneo yanayohusika na Baraza la Manispaa, kazi yake ni kwenda pale kuzizoa zile taka na kwenda kuzitupa katika majaa ambayo yamewekwa na serikali.

**Mhe. Moh'd Ali Salim:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa nilivyomfahamu Mhe. Waziri alivyokuwa akizungumza ni kuwa Manispaa kazi yake ni kuchukua taka zilizokusanywa.

Je, wale kinamama walio na mafagio waliopangwa katika sehemu mbali mbali za chochoro kazi yao ni kufanya nini, ni kuchukua zile taka zilizokusanywa au ni kufagia wakakusanya taka na wenye vile vigari wakaja kuchukua.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, narejea tena maelezo yangu, usafi wa nyumba au mazingira yanayozunguruka nyumba usafi ule unatakiwa kwa mwananchi mwenyewe. Wale kinamama wanaopita na mafagio wale kazi yao ni kusafisha barabara na chochoro. Kwa hivyo sehemu za barabara na chochoro zile ni sehemu ambazo Baraza la Manispaa wao ndio wanasafisha. Lakini katika maeneo yanayozunguuka ile nyumba ya mtu binafsi, suala lile linabakia kwa mtu mwenyewe. Ndio maana katika sehemu ya Mji Mkongwe na sehemu nyengine tofauti, na hasa hawa ndugu wetu Wahindi wao wanajitahidi sana na wanaweka viporo na wale wafanyakazi wa Manispaa wakija wanachukua kile kipolo cha taka wanakwenda kukitupa.

Lakini, sisi Waswahili ndio wenye matatizo, tunasubiri mpaka yule mfanyakazi wa Manispaa ndio aje atusafishie nyumba zetu, sasa hilo ni tatizo. Sasa mimi kupitia Baraza lako tukufu na kupitia kwa Mhe. Moh'd Ali Salim, naomba niwapongeze sana ndugu zetu wenye asili ya Kihindi kwa kuweza kutekeleza sheria hii ya Manispaa.

**Mhe. Salmin Awadha Salmin:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Wakati akijibu swali la nyongeza la Mhe. Moh'd Ali Salim Mhe. Waziri amesema kwamba wafanyakazi wa Baraza la Manispaa huwa wanafanya shughuli za kusafisha barabarani na sehemu za vichochoroni.

Kwa kuwa eneo la Manispaa la Zanzibar ni eneo kubwa kwa nini wafanyakazi wale wanakuwa wako katika maeneo ya Mji Mkongwe tu badala ya kupangwa na maeneo ya Ng'ambo kama vile katika jimbo la Kwahani na Magomeni.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, nilifikiria labda nikijibu vizuri sitoulizwa tena swali la nyongeza kumbe ndio yanazidi.

Kuhusu suala la usafi hasa wa mji kwa kutegemea kwamba tuwategemee wafanyakazi tu wa Baraza la Manispaa kusafisha mji wote, itakuwa ni kazi kubwa na idadi ya wafanyakazi itabidi iongezeke zaidi. Sasa nitatoa mfano ule ule wa Rwanda ambayo ni nchi inayotolewa mfano hata Ulaya. Wenzetu kule walivyofanya wameshajihisha vikundi vya ushirika na vikundi vya mazingira, bahati nzuri hapa kwetu kama tunaanzisha vikundi vya mazingira, basi kupitia mradi wa *MACEMP* wanaweza kuomba fedha na kupatiwa vifaa kwa ajili ya kuweza kufanyia usafi wa mazingira. Kwa hivyo, wenzetu wamefanikia kwa hivyo na hata Namibia, vile vile wenzetu wameanzisha vikundi vya ushirika katika maeneo mbali mbali.

Hata ile Rwanda sio Manispaa peke yao wanaosafisha, ni vikundi vya ushirika vilivyojikusanya na wananchi wenyewe kupitia sheria ndogo ndogo za Baraza la Manispaa, wanaweka sheria ya kulipa ada kwa mujibu walivyopanga wao wenyewe. Nawashukuru sana Wilaya ya Magharibi waliwahi kujaribu zoezi hilo, hata jimbo langu la Kwamtipura, jimbo la Mkele tuliwahi kuanzisha kikundi cha ushirika cha kuweza kuzoa taka.

Lakini, tatizo linarudi pale pale wananchi wetu wanapochangishwa shilingi moja kwa ajili ya uzoaji wa taka wanakuwa wanashindwa, sio hawawezi, lakini wanashindwa na vile vikundi vinavyoanzishwa vinakuwa vinakufa kwa kushindwa kuwalipa mishahara wale wanaoanzisha na yale maeneo inakuwa yanashindikana. Sasa hivi kuna kikundi Wilaya ya Magharibi pale wanajiita jina lake kidogo limenitoka. Lakini, kimsingi wameweza kununua mabero, magari alikodi kwa ajili ya usafishaji wa mji, lakini ule mradi matokeo yake umemshinda. Kwa sababu anashindwa kuwalipa wananchi ada na vile vile kushindwa kupata *support* ya kuweza kuwalazimisha wale wananchi kuweza kulipa.

Kwa hivyo, bado narejea tena suala la usafi ni la jamii yenyewe tuhamasishe wananchi wetu na tuanzishe vikundi vya ushirika na wananchi wenyewe katika maeneo yetu ya mjini au vijijini, wakubali kuchangia kwa kufanya usafi wa mazingira, kwa kulipia japo ada ya shilingi mia moja kwa kila siku kwa ajili ya kusafisha mji.

**Nam. 84**

**Sheria za Zanzibar Kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili**

**Mhe. Salmin Awadh Salmin - ** Aliuliza:

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Ibara ya 87(2). Kila mswada, kila sheria inayotungwa na Baraza la Wawakilishi itaandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

(a) Hivi Mhe. Waziri, zipo sheria zilizotungwa na Baraza la Wawakilishi na zikaandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

(b) Kama zipo ni sheria zipi.

(c) Mhe. Waziri, utakubaliana na mimi kuwa kuendelea kuandika sheria zetu kwa lugha ya kigeni kunawafanya wananchi wetu washindwe kuzielewa vyema sheria za nchi yao.

(d) Kwa nini Sheria zinazopelekwa kwa Mhe. Rais kwa ajili ya kuidhinishwa *(ASSENT)* zinaandikwa kwa lugha ya kigeni.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora -** Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake No. 84 lenye sehemu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Kifungu cha 87(2) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinaelekeza kuwa kila Mswada wa Sheria na kila Sheria inayotungwa na Baraza la Wawakilishi, itaandikwa kwa lugha ya Kiswahili na ikihitajika kwa lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo lugha zote mbili Kiswahili na Kiingereza zinakubalika.

(b) Katiba ya Zanzibar ya 1984 ambayo ndio Sheria Kuu (Sheria Mama) ya nchi imeandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

(c) Lugha inayotumiwa katika majadiliano ndani ya Baraza la Wawakilishi, Miswada ya Sheria huandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo ninaamini kuwa wananchi wanapata fursa nzuri ya kuzielewa Sheria zinazotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(d) Kama nilivyojibu katika (a), Kiswahili na Kiingereza ni lugha zinakubalika katika uandishi wa sheria. Kwa sababu mfumo wetu wa sheria unatokana na mfumo wa sheria wa Uingereza *(UK),* yaani *(Common Law System),* na kwa kuwa nchi zote duniani ambazo ziliwahi kutawaliwa na kwa kuwa nchi hizo zote zinaendelea kushirikiana kupitia chombo cha Kimataifa cha Jumuiya ya Madola *(Common Wealth),* basi Sheria zetu huandikwa kwa lugha ya Kiingereza kama ni njia moja wapo ya kudumisha ushirikiano huo.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo;-

Mhe. Spika, swali lililoulizwa hapa mara nyingi katika tafsiri yaani katika sheria zetu zikitiwa saini na Mhe. Rais huwa zinatiwa kwa lugha ya Kiingereza, natumaini asilimia 99 au asilimia 90 ya Wazanzibari, lugha yao kuu ni ya Kiswahili.

(a) Mhe. Waziri haoni ni vyema Mhe. Rais anapoweka saini zetu aweke katika lugha zilizokubalika Kiingereza na Kiswahili?

(b) Labda mimi sifahamu kidogo nataka kujua kwani Zanzibar ilitawaliwa na Mwingereza?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali mama ni kwamba,

(a) Sheria zetu zinaandikwa katika lugha zote mbili kwa Kiswahili na Kiingereza. Anaposema Mhe, kwamba ile inayotiwa na Rais inaandikwa kwa Kiingereza, lakini pia inakuwepo sheria ya Kiswahili nayo pia inakuwa *accepted* vile vile kwamba imekubaliwa kutumika kama sheria.

Tujue kwamba sheria hatutumii sisi peke yetu, tunatumia sisi hapa ndani lakini pia Mabalozi na wageni mbali mbali huwa wanazitaka sheria hizi na wanataka kuzifahamu. Kwa hivyo zikiwa katika lugha ya Kiingereza wanazifahamu.

(c) Mhe. Spika, swali lake la pili ni kwamba Zanzibar ilitawaliwa na Mwingereza? Napenda kumjibu kwamba Zanzibar ilikuwa na watawala wa kigeni wawili kwa wakati mmoja.

**Mhe. Moh'd Ali Salim:** Ahsante Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza.
Kwa kuwa katika Baraza hili tukufu la Wawakilishi, Miswada tunayoijadili ni ya Kiswahili na kwa kuwa wakati huu kunakuwa na Mswada mwengine katika lugha ya Kiingereza lakini haujadiliwi hapa Barazani.

Je, kuna uhakika gani kuwa ule wa Kiswahili na ule Kiingereza maana yake ni sawa sawa ?

**Mhe. Wazi wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, mara nyingi ule wa Kiswahili ndio unaotafsiriwa kwa Kiingereza. Na mara nyingi wajumbe wa Baraza lako tukufu huomba kupatiwa Miswada yote miwili ili waweze kujua kwamba maana zimekwenda sawa. Kwa hivyo hii jitihada inapita kuhakikisha kwamba maana zinakuwa sawa kwa mujibu wa lugha ya kisheria.

**Nam. 27**

**Utaratibu wa Dhamana za Kazi Hospitali ya Mnazi Mmoja**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu** - Aliuliza:

Kwa kuwa wananchi wengi hasa wagonjwa wanaolazwa hospitali wanashindwa kujua na kutofautisha dhamana, madaraka na vyeo vya wafanyakazi wa hospitali hasa kati ya daktari, muuguzi na "*orderly*" ambapo wote hao huitwa madaktari.

(a) Mhe. Waziri, kwa faida ya Baraza hili na kwa niaba ya wananchi unaweza ukatueleza kwa ukamilifu na kwa mpangilio vyeo, wadhifa na dhamana za uongozi mzima wa wafanyakazi wa hospitali ya Mnazi Mmoja kuanzia Daktari Mkuu hadi "*Orderly*".

(b) Unaweza kutueleza kwa majina yao na wadhifa wao au vyeo vyao uongozi mzima wa Wizara kuanzia Waziri hadi Karani Mkuu.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii -** Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 27 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, baada ya mageuzi ya muundo wa Wizara, Hospitali ya Mnazi Mmoja ilifanywa kuwa ni Idara mnamo mwaka 2003 na kuteuliwa Mkurugenzi wake.Kwa sasa Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja inajumuisha hospitali ya Kidongo Chekundu (*Mental*) na Mwembeladu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja inaongozwa na Mkurugenzi ambaye anasaidiwa na:-

- Mganga Mkuu anayesimamia mambo yote ya Tiba.
- Muuguzi Mkuu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja anayesimamia mambo yote ya Wauguzi.
- Katibu wa Hospitali anayesimamia shughuli zote za makarani, ma-*orderly*, madereva, walinzi na kadhalika.
- Mhasibu
- Afisa Uhusiano
- Afisa Utumishi
- Mkuu wa Kitengo cha Mafunzo
- Mkuu wa sehemu ya ufundi
- Mkaguzi wa hesabu za ndani.

Mhe. Spika, dhamana za viongozi hawa wote ni:-

i. Kusimamia utendaji wa kazi kwa watendaji walio chini yao.

ii. Kutoa mafunzo /kuelekeza katika utekelezaji wa shughuli za kazi.

iii. Kutatua matatizo yanayojitokeza katika utendaji wa kazi na kadhalika.

(b) Mhe. Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inaongozwa na viongozi wafuatao:-

| | |
|---|---|
| • Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry | Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii |
| • Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Naibu Waziri |
| • Dr. Moh'd Saleh Jidawi | Katibu Mkuu |
| • Dr. Malik Abdulla Juma | Mkurugenzi Mkuu |
| • Dr. Jamala A. Talib | Mkurugenzi wa Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. |
| • Dr. Salhiya A. Muhsin | Mkurugenzi wa Kinga na E/Afya |
| • Dr. Abdalla Juma Saadalla | Mkurugenzi Tiba |
| • Nd. Said Abdulla Natepe | Mkurugenzi Mipango na Sera |
| • Nd. Juma Rajab Juma | Mkurugenzi Afya ya Jamii |
| • Nd. Ahmed Moh'd Awadh | Mkurugenzi wa kudhibiti Madawa ya Kulevya na Kurekebisha Tabia. |
| • Nd. Halima Salum | Mkurugenzi Ustawi wa Jamii |
| • Nd. Mkasha H. Mkasha | Afisa Mdhamini Pemba |
| • Nd. Abdulrahman Ahmada Vuai | Mhasibu Mkuu wa Wizara |
| • Nd. Habib Ali Sharifu | Mfamasia Mkuu |
| • Nd. Twaha Makame Silima | Afisa Utumishi |
| • Nd. Rashid Abdulla Ali | Karani Mkuu |

Mhe. Spika, pia wapo wakuu wa vitengo, miradi, Mkuu wa Chuo cha Afya Mbweni na Maofisa mbali mbali na wenye dhamana katika sehemu zot za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ikiwa Mhe. Mwakilishi atataka kujua majina yao tunamkaribisha wakati wowote katika wizara yangu ya Afya na Ustawi wa Jamii.

**Mhe. Ali Abdalla Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba nimuulize kama ifuatavyo.

Ametueleza utaratibu mzuri na mtiririko wa uongozi katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Je, katika hospitali za kanda na vijijini mtiririko huo uko vipi ?

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, kuhusu hospitali za Kanda ziko chini ya Mkurugenzi Kinga halafu yuko daktari dhamana ambaye anaitwa Z*onal Medical Officer* halafu wapo *(DMO) District Medical Officer*. Kwa Unguja kanda yote ni zoni moja ambaye daktari zamana wake yuko Lumumba.

Kwa upande wa Pemba Afisa Mdhamini ndio anakuwa *zonal medical officer*. Kwa hivyo, Wilaya ya Mjini yuko D*istrict* M*edical Officer* . Kila Wilaya kuna D*istrict Medical Officer* ambaye anakuwa dhamana na anakuwa na vituo vyake na kila kituo kina mkuu wake na watendaji wake wa kazi.

**Mhe. Mwajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza au mawili.

(a) Mhe. Spika, napenda kuumuliza Mhe. Waziri ma-*orderly* hasa kazi yao ni nini hadi kufikia kuitwa daktari ?

(b) Kwa kuwa ma-*oderly* wengine hawaridhiki kuitwa jina hilo. Je, Mhe. Waziri una mpango gani wa kukaa nao pamoja ili ma-*oderaly* hao wajue vyeo vyao au dhamana zao na kuvitumia ipasavyo ?

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, *orderly* kazi yao ni kufanya usafi katika hospitali inategemea yuko wapi. Kwenye kituo cha Afya kazi yake ni kuhudumia na kufanya usafi sehemu zote za kituoni. Na katika Hospitali pia ni kufanya kazi za usafi. Hapa Unguja tumezoea wananchi, sio katika kituo au katika hospitali mfanyakazi yeyote wa hospitali ikiwa *orderly*, *nurse*, karani huwa anaitwa daktari, lakini ukweli yule si daktari yule ni

*orderly*. Kazi yake ni kufanya kazi za usafi, hata kama hapendi kuitwa hivyo lakini huko nje ataitwa daktari kwa sababu anafanya kazi hospitali.

Tunaomba kuanzia sasa madaktari waitwe madaktari na hawa wahudumu wetu wa usafi waitwe na wao ni wafanyakazi wa kufanya kazi za usafi, lakini ni vigumu kufanya hivyo. (*Vicheko*)

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Spika, kwa kuwa kazi ya *orderly* ni kufanya usafi. Lakini kwa kuwa ma-*orderly* katika baadhi ya hospitali na Zahanati hutibu watu kupiga sindano, kutia watu *drip* n.k.
Je, mwenye dhamana ya kulizuia hili ni nani, maana muda mrefu tumekuwa tunapiga kelele na bado halijatekelezwa.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, kazi ya *orderly* ni kufanya usafi sio kupiga sindano wala kutia watu drip. Kama atafanya kazi hiyo ni kosa na litakapotokea jambo lolote itabidi ashtakiwe. Sisi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hatuwaruhusu ma-*orderly* kufanya kazi hizi, sio kazi zao.

Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi tunakwambia kwamba *orderly* sio kazi yake kutia drip wala kupiga sindano wala haturuhusu.

**Nam. 48**

**Mafanikio ya Wizara ya Kazi Katika Kutekeleza Programu ya Kupambana na Ukimwi**

**Mhe. Anaclet Thobias Makungila –** Aliuliza:-

Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto imefanikiwa kiasi gani katika kutekeleza program ya kupambana na ukimwi katika maeneo ya kazi na kuhakikisha kwamba haki za wanawake na watoto zinaendelea kulindwa pamoja na kuwainua wanawake kiuchumi kwa kuwapa ushauri na mafunzo ya kukuza uchumi na kuwapunguzia umaskini ?

**Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto –** Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 48 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuwa wazima na tukaweza kushiriki katika mkutano huu, Inshaalla Mungu atazidi

kutupa afya njema na busara na hekima kutengeneza yale ambayo wananchi wetu wametutuma.

Mhe. Spika, mapambano dhidi ya Ukimwi ni wajibu wa kila taasisi na kila mtu. Wizara yangu ambayo inasimamia masuala ya kazi na usalama sehemu za kazi ina wajibu wa moja kwa moja kushughulikia masuala ya ukimwi sehemu za kazi, kwa lengo la kukinga maambukizi sambamba na kudhibiti ubaguzi na unyanyasaji katika kazi.

Mhe. Spika, mipango na mikakati mbali mbali imewekwa na kusimamia katika utekelezaji na Wizara yangu pia nguvu imetiliwa zaidi katika mapambano dhidi ya Ukimwi. Mipango iliyopewa kipa umbele miongoni mwake ni:-

(1) Kuliweka suala la ukimwi katika Sheria za Kazi ambapo kila Mwajiri anatakiwa kuweka utaratbu maalum wa kukinga maambukizi, vile vile kutokuwabagua waathirika waliopo kazini. Sheria ya Ajira Nam. 11 ya mwaka 2005 imewataka waajiri kuwaelimisha wafanyakazi wao pamoja na kuweka katika sera zao sharti linalohusu ukimwi. Aidha katika kila sera, mipango na mikakati inayofanywa na wizara yangu katika utekelezaji wa majukumu yake tunaweka masuala yanayohusu ukimwi.

(2) Wizara kupitia Vitengo vya Afya na Usalama kazini na Ukaguzi kazi, hukagua na kuelimisha wafanyakazi na waajiri juu ya ugonjwa huu thakili sambamba na kutoa elimu kupitia vyombo vya habari pamoja na kushirikiana na wadau, ILO, Waajiri na Shirikisho la Vyama vya wafanyakazi hufanya mikutano, semina na mambo mbali mbali kutafakari na kuweka mikakati ya kuondoa janga hili. Wizara yangu inakataza unyanyasaji wa aina yoyote katika ajira dhidi ya wenye maradhi ya Ukimwi au Virusi vya maradhi hayo.

(3) Vile vile kupitia Kamati ya kitaalamu ya Ukimwi ya Wizara taaluma kuhusu Ukimwi imekuwa ikitolewa kwa wafanyakazi wa mawizara.

Mhe. Spika, vile vile, katika jitihada za wizara za kuhakikisha kwamba haki za wanawake na watoto zinaendelea kulindwa. Wizara imechukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za ushauri nasaha na usuluhishi kwa akina baba na akina mama ambao huwasilisha malalamiko yao ya kifamilia Wizarani. Aidha imekuwa ikiendesha mafunzo maalum ya Haki za Watoto kwa watendaji wote wa Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto Unguja na Pemba kwa lengo la kukuza utendaji wao na kuhakikisha haki za Wanawake na Watoto

zinalindwa na kuheshimiwa. Pamoja na hayo, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi za Sheria imekuwa ikiendesha vipindi tofauti kupitia Redio na TV pamoja na kutoa makala katika magazeti kwa lengo la kutoa Taaluma ya kisheria ili kuiwezesha jamii kuzielewa sheria hizo na kulinda haki zao.

Mhe. Spika, pia wizara katika utekelezaji wa haki za watoto nchini, imeanza hatua za awali za kutayarisha Mswada wa Sheria moja ya Mtoto (*Child bill*) ambayo itajumuisha masuala yote yanayohusu uhai, hifadhi na maendeleo ya Mtoto. Hadi sasa tayari Kamati ya kitaalamu yenye jumla ya watu 11 kutoka sekta tofauti zinazoshughulikia masuala ya watoto imeundwa kwa lengo la kutayarisha Mswada wa Sheria hiyo. Pia wizara inahakikisha hakuna Mtoto ambaye hajafikia umri wa kuajiriwa anaajiriwa, Ni kosa kisheria mwajiri kumuajiri mtoto aliye chini ya umri wa miaka 17.

Mhe. Spika, katika jitihada za wizara za kuwainua Wanawake kiuchumi kwa kuwapa ushauri na mafunzo ya kukuza uchumi na kuwapunguzia umaskini. Wizara imekuwa ikiendesha Makongamano maalum kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba pamoja na baadhi ya watendaji wa sekta zinazohusiana na Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Makongamano hayo yanatoa fursa kwa wanawake hao kujadili kwa kina namna gani wanaweza kujiinua kiuchumi na kijamii, ambapo changamoto kubwa inayoonekana ni wanawake kujenga moyo wa kujielimisha zaidi na kujitokeza katika shughuli za maendeleo. Aidha wizara imekuwa ikiendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake wa Wilaya za Unguja na Pemba pamoja na kuvitembelea vikundi kwa kuvipatia ushauri wa kitaalamu ili viweze kuendesha shughuli zao kwa ufanisi. Wizara pia inawahamasisha wanawake kujiunga na SACCOS na kuweza kupata mkopo nafuu ili kuweza kuwasaidia kujinyanyua kiuchumi. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Spika, kwanza nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Vijana, Wanawake na Watoto kwa jibu lake zuri na refu ili kutupa ufafanuzi tuliokuwemo humu tuweze kufahamu sisi na wananchi wetu wanaotusikiliza wayafahamu.

Mhe. Spika, pamoja na majibu hayo kwa kuwa wizara hii madhumuni yake ni kuleta ajira kwa vijana wetu na kutafuta haki za watoto na akina mama. Swali langu ni kwamba kwa kuwa hivi sasa hivi maradhi ya ukimwi yanazidi kuendelea na vitangi katika nchi yetu hii ya Zanzibar, wanaendelea kwa kasi ya juu. Hata leo asubuhi katika mawiyo ya sauti ya Tanzania Zanzibar tumesikia taarifa kuna mtu mmoja mwanamme mwenye umri wa miaka 42 au 45 kama sikosei, amemuingilia kinyume na maumbile mtoto mdogo mwenye umri wa miaka 12 lakini kwa bahati mbaya Mahakama yetu, ingawa siingilii Mahakama

maamuzi yake lakini nitoe taarifa tu, imetoa adhabu ya miaka miwili tu kwa yule muhalifu aliyefanya kitendo hicho kibaya.

Je, Mhe. Waziri kwa kuwa hili tumelisikia leo kwa uwazi kabisa, wizara itachukua hatua gani juu ya kumsaidia mtoto yule. Na kwa kuwa huyu ni mmoja lakini wapo wengine ambao tunaweza kumpelekea Mhe. Waziri kwa kuwa tunapenda kusikiliza sauti ya Tanzania Zanzibar na kusikiliza mawiyo, wanatoa taarifa za ukweli kabisa. Watu kama hawa Mheshimiwa unatoa wito gani ili kuhakikisha kwamba unawasaidia kwa wale wahalifu wanaofanya kitendo kama hicho wapate adhabu wa kukomeshwa ili kisitokee tena ?

**Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, Wizara yangu inasikitishwa sana na vitendo hizi ambavyo vinaonekana kama kuongezeka kuhusu mambo ya vitangi. Kwa kupitia hapa nalaani sana vitendo hivyo na pia nalaani sana hili jambo ambalo limetokea na leo hii limeripotiwa. Kama alivyosema mwenzangu hatupaswi kuingilia utaratibu wa Mahakama, lakini tunaweza tukafanya kama *lobby group*. Mhe. Ali Suleiman wewe unayomamlaka na unaweza kuleta hoja binafsi izungumzwe hapa kuhusu suala hilo. Kwa sababu sote linatuuma sana na tutafuta namna ya pamoja.

Lakini pia Waziri wa Katiba na Utawala Bora yupo na kama hayupo basi ataambiwa na waliokuwepo kwamba hatujaridhika na hukumu hiyo. Tunatoa wito kwa *lobbies* wanawake sote tuungane tupinge kitendo hiki na tuombe adhabu kali na tuombe hiyo kesi irudiwe tena kama taratibu za kisheria zinavyoelekeza. Lakini mimi na wizara yangu na wenzangu wote na nyinyi humu naamini kwamba huu utangi hatuupendi na tunataka huu utangi utoboke tupumzike roho zetu. Ahsante.

**Mhe. Spika:** Mchukue hatua za kukata rufaa na msije mkachukua hatua nyengine ambazo zitaiingilia utaratibu Mahakama.

**Mhe. Muhydin Moh'd Muhydin:** Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii naomba nimuulize Mhe. Waziri maswali yafuatayo:-

Alipokuwa akijibu alisema kwamba wizara yake inawasaidia akina mama kuwapa mikopo kwa ajili ya kujiendeleza na akina mama hao wanafanya juhudi hiyo. Lakini wanakabiliwa na tatizo la soko katika bidhaa zao wanazozalisha.

(a) Je, Mhe. Waziri anashirikiana vipi na Mhe. Waziri wa Biashara katika kutatua tatizo hilo linalowakabili wanawake ?

(b) Wizara yake ni wizara inayosimamia jamii na jamii imefanyika na makundi mawili lakini inavyoonekana wizara yake inashughulikia zaidi kundi moja la hiyo jamii. Je, hili kundi la pili la hii jamii analishughulikia vipi Mhe. Waziri ?

**Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, kwanza kuhusu mashirikiano baina yangu na Waziri wa Biashara na Utalii na Uwekezaji ni makubwa sana na sisi tunajitahidi kuwapa mafunzo hao wajasiri mali ili watengeneze bidhaa zilizokuwa bora ambazo litapata soko kwa urahisi. Kwa hivyo ni kusema kwamba suala hilo la soko linafanyiwa kazi na yapo mabadiliko yaliyopatikana kutokana na bidhaa zinazotengenezwa na wajasiri mali wetu kutoka hapa kwetu Zanzibar.

Kwa mfano mara hii Tanzania tumeweza kuibuka washindi katika maonyesho ya Jua kali, Nguvu Kazi kule Kigali na bidhaa zilizotoka Zanzibar ndizo zilizotia fora. Kwa hivyo kwa hilo tutaendelea kuongeza mashirikiano baina yetu.

Swali lake la pili kuhusiana na kundi la jamii. Kwanza ningefurahi sana kama angesema kundi lipi ambalo limeshughulikiwa na lipi ambalo limeachwa. Maana jamii iko kubwa, lakini ninavyomjua yeye kwa ule uchokozi wake anaona kama mimi napendelea zaidi wanawake. Ni kweli lakini tunawashughulikia na vijana vile vile ambao na wanaume wamo katika hao vijana na tuna mipango kabambe ya kuwasaidia kimaendeleo.

Usiwe na wasi wasi lakini ukumbuke kwamba wanawake ndio wenyewe, wanawake ndio wanaoaminika, wanawake ndio mama zetu, wanawake ndio dada zetu na wanawake ndio wake zetu.

**Nam. 23**

**Kuvuja kwa Jengo la Uwanja wa Ndege wa Zanzibar**

**Mhe. Ali Suleiman Ali –** Aliuliza:-

Jengo la Uwanja wa ndege wa Zanzibar linavuja katika sehemu ya Abiria wanaosubiri usafiri. Aidha sehemu hiyo pia haina vipozea hewa.

(a) Je , Mhe. Waziri unafahamu kuwa tatizo hili ni la muda mrefu na bado linaendelea kuwepo bila ya kupatiwa ufumbuzi ?

(b) Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba kasoro hiyo inaushushia hadhi uwanja wetu ?

(c) Kwa kuwa kasoro hiyo inaupunguzia sifa uwanja wetu, Je. Mhe. Waziri huoni kuwa tatizo hilo linaathiri pia Sekta ya Utalii nchini ?

**Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake ninaomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Tatizo la kuvuja katika sehemu ya Abiria katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar linatokana na uchakavu wa mabomba ya maji yaliomo katika ukuta wa juu ya sehemu hiyo. Jitihada mbali mbali za kuziba sehemu hiyo zilikuwa zikifanyika bila ya mafanikio kutokana na kutotatuliwa kwa suala la msingi kama nilivyokwisha kueleza hapo juu.Hata hivyo tatizo hilo hivi sasa halipo, ambapo sehemu hiyo imekuwa haivuji tena baada ya kujulikana kwa tatizo la msingi na kufanyiwa matengenezo makubwa pamoja na kuongezwa vipoza hewa.

Baada ya maelezo hayo naomba sasa kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama nilivyokwisha kueleza hapo juu katika maelezo yangu ya msingi kuwa tatizo hilo la kuvuja hivi sasa halipo tena katika kiwanja cha ndege za Kimataifa cha Zanzibar baada ya kufanyiwa matengenezo makubwa katika sehemu hiyo, pamoja na kuongeza vipoza hewa katika sehemu ya kupumzikia abiria. Aidha kuwepo kwa kasoro hiyo haikuwa sababu ya kushusha hadhi yetu katika kiwanja hicho na kushusha sekta ya utalii kutokana na kuongezeka kwa idadi ya ndege kubwa za kigeni zinazofika na abiria na kuchukua abiria katika kiwanja hicho.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali moja la nyongeza (a) na (b) kama ifuatavyo kwa ufupi kabisa.

a) Mhe. Spika, kwanza niipongeze Idara ya Uwanja wa Ndege kwa kutujengea *canopy* ambayo lile tatizo la muda mrefu hivi sasa tunaamini limeondoka. Lakini nilikuwa nataka kumwambia Mhe. Waziri kwamba pamoja na uzuri huo uliokuwepo sasa hivi. Je, wizara ina mpango gani wa haraka angalau kuweka mabenchi ya kukalia kwa wale wanaosubiri usafiri.

b) Kwa kuwa hivi sasa viwanja vyote duniani vinaendelea na wakati tuliokuwa nao, sio mizigo inafika inangojea mkokoteni ichukuliwe kwenye ndege iletwe pale wenyewe wasubiri kwenye mapokezi ya mizigo. Wizara ina mpango gani wa makusudi kutafuta ule ukanda ambao unazunguka katika nchi zote duniani ili mzigo unapowekwa pale iwe mtu anachukua anaondoka ?

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, kwanza tunashukuru pongezi zake kwamba ni kweli baada ya kuwa na kero la muda mrefu kwa abiria wetu wa ndani na wa nje, Wizara yetu ya Mawasiliano na Uchukuzi imeweza kujenga *canopy* ya muda ambayo ikimalizika tutafuata ushauri wake kwa kuangalia uwezekano wa kuweka viti. Lakini ni kwamba tunahofia isiwe ndio matembezi ya watu kwenda kukaa pale, tutajitahidi tuwe na viti ambavyo vitawasaidia abiria wanaoingia na kutoka katika nchi yetu.

Pia naomba nichukue nafasi hii kuwaeleza Waheshimiwa Wajumbe kwamba tuna mpango endelevu kwa Uwanja wa Ndege na hivi karibuni tunatarajia kwamba lile suala la muda mrefu la *run way* tunalipatia ufumbuzi kwa sababu tayari tumeshatoa *tender*. Makampuni matatu ya *INTER BETOL* ya. Holland, *SOGEA* ya France na *MNO* ya Holland wame-*tender*. Kwa hivyo, mchakato wa kumpata mkandarasi tunatarajia utakuwa hivi karibuni na tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie kabla ya mwezi wa Machi mambo yote yawe hadharani ili tuanze shughuli hizi.

Kwa upande wa kuwa na sehemu za kuchukulia mizigo. Hilo nalo ni mpango wetu kwa sababu pamoja na hilo, hata *terminal building* zetu sasa zimeshapitwa na wakati. Wakati kinajengwa kiwanja kile ilikuwa wastani wa kuingiza watu 200 pengine kwa siku, sasa hivi tunapokea abiria zaidi ya 100. Kwa mfano, siku ya Jumatano siku hizi tunakuwa na wast*ani* wa ndege 9 mpaka 11 za kimataifa kwa kila Jumatano. Kwa hivyo, hali ni kwamba lazima tuboreshe kiwanja chetu na ni matarajio yetu kwamba wananchi na Waheshimiwa Wawakilishi mtatuunga mkono katika suala hili.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Ahsante Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nakumbuka kwamba ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2005 iliazimia makubwa katika viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba.

Je, Mhe. Waziri anaweza kulieleza Baraza lako tukufu maazimio yale ya ilani ya chama chake anayoyatekeleza yamefikia kiwango gani na kwa sababu muda unayoyoma ana hakika kabla ya kufika 2010 utekelezaji wa ilani ile itakuwa ameusimamia vizuri ?

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, napenda kulihakikishia Baraza hili kwamba Chama cha Mapinduzi kitatekeleza kwa kiwango safi sana katika viwanja vya ndege. Pia moja ya ilani ni kufanya hiyo *run way* na tunatarajia tutaimaliza kwa miezi 15 iwe tayari. Hata Pemba tuna mpango endelevu na nafikiri sasa hivi ukienda pale uwanja wa ndege wa Pemba *VIP* zote mbili tunatumia ile ya chini na ya juu Mhe. Mwakilishi ukienda, nakuomba tumia yoyote katika hizo mbili. Lakini ni kwamba Chama cha Mapinduzi ilani yake sio ya miaka mitatu ni ya miaka mitano. Kwa hivyo, sisi tuna hakika na miaka mitano na Mwenyezi Mungu akipenda tuje tupate hizo kura za CCM zote mbili kwa sababu ni chama bora zaidi.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri ameondoka bila ya kumwambia aondoke, ananijua kwamba nilitaka kusema sasa tuendelee lakini hajakimbia maswali.

**Nam. 8**

**Matatizo yanayoukabili Ushirika wa Chumvi Pemba**

**Mhe. Ali Abdalla Ali** – Aliuliza:-

Wananchi wengi wa Pemba waliamua kuunda vikundi vya ushirika ili kuekeza katika uzalishaji wa chumvi kwa lengo la kujikwamua kimaisha. Hata hivyo, bado wanakabiliwa na tatizo la kukosa mikopo, kukosa soko la uhakika na hata uwezo wa utiaji wa madini joto (*iodine*), mambo ambayo yanakwamisha uzalishaji na kuwavunja moyo wananchi hawa.

a) Je, Mhe. Waziri kuna ukaguzi wowote unaofanyika kwa vikundi hivi kwa lengo la kuangalia matatizo yao na kuwasaidia ?

b) Kwa kuwa vikundi vingi hupatiwa mikopo ili kuongeza uzalishaji, kwa nini Ushirika wa Chumvi haupatiwi mikopo hiyo?

(c) Je, kuna sababu zipi zinazokwamisha kutotafutiwa soko katika nchi za jirani, ili wananchi hawa wafikie malengo waliyojiwekea?

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 8 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, vikundi vya uzalishaji chumvi vipo chini ya uangalizi wa ushirika wao uitwao *ZASPA* yaani (*Zanzibar Salt Producer Assossiation)* pamoja na Idara ya Viwanda ndani ya Wizara ya Utalii Biashara na Uwekezaji

kuvitembelea vikundi vya uzalishaji wa chumvi katika maeneo yao tofauti. Katika ziara hizo yafuatayo yamegundulika.

Kuna mashamba mengi hasa yaliyoanzishwa nje ya utaratibu wa *NIGP* ambayo hayapo kwenye muundo stahiki na kusababisha maji kutoingia au kutoka inavyotakiwa. Pia kuna upungufu wa *machine* za kusukumia maji kuingiza au kutoa kwenye mashamba. Vile vile kuna upungufu wa utaalamu, wataalamu kwa sasa hivi wanatoka Tanzania Bara hapa kwetu kuna wataalamu wachache sana.

Kuna suala la kutokutabirika kwa hali ya hewa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa ulimwenguni, hivyo kufanya wazalishaji kutokuwa na uzalishaji wa uhakika yaani kuna msimu wanaotegemea maji yangeingia kwamba mawimbi yangekuwa makubwa, lakini kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa inakuwa sio hivyo. Kwa hivyo, ndio uzalishaji unakuwa hauna uhakika.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba chumvi hii sasa inatiwa *iodine*, lakini bado haijafikia kiwango kinachotakiwa kwa uhakika kamili wa chumvi inayouzwa madukani.

Jengine chumvi inauzwa katika hali ya mawe wakati mahitaji makubwa ni chumvi ya unga. Swali jengine ni uhifadhi wa chumvi bado ni wa kienyeji sana haijafikia hadhi inayokubalika yaani ufungaji wa chumvi wenyewe.

Kufuatia matatizo hayo yaliyogundulika hatua zifuatazo zinachukuliwa.

a) *ZASPA* inaleta wataalamu kila baada ya muda ili kurekebisha mashamba yawe na muundo wa kuvuta au kutoa maji kwa nguvu ya mtiririko. Hii itasababisha kupunguza gharama za kutaka *machine* za kusukumia maji kutoka baharini na kutoa kwenda baharini.

b) Kutoa mafunzo kwa vikundi juu ya uzalishaji wenye tija, uwekaji wa *iodine* na uhifadhi wa chumvi yenyewe.

c) Ili kufikia kiwango kinachotakiwa kimataifa *machine* za kusaga chumvi ya mawe kuifanya kuwa ya unga zimeshanunuliwa na sasa ziko katika hatua ya kumalizia kufungwa na kujaribiwa.

d) *ZASPA* kupitia mikopo na misaada imeshanunua na kufunga *machine* za kuwekea *iodine* ili chumvi ishughulikiwe kwenye vituo maalum. Pia *machine* za *laboratory* kwa ajili ya kujaribia

kiwango na sifa za chumvi zimeshanunuliwa lakini bado hazijafungwa.

e) Malighafi ya kufungia zenye maandishi maalum ya *ZASPA* pamoja na *machine* za kufungia nazo zinatarajiwa kupatikana hivi karibuni. Pamoja na hatua zilizochukuliwa bado *ZASPA* inakabiliwa na changamoto ya mtaji kutokidhi mahitaji ya wanachama.

Kwa maana hiyo juhudi ya kutafuta mikopo ili kukuza mitaji kwa vikundi na *ZASPA* yenyewe bado zinaendelea na wizara tuko nyuma katika hili. Kuna Shirika linaitwa *Gust Trust* ambalo huwa linatoa mikopo kwa kiwango cha 100,000/- lakini tumezungumza nao waongeze kiasi cha mikopo hiyo ili vikundi kama hivi vya ushirika viwe vinafaidika pia na mikopo hiyo.

Mhe. Spika, haja ya kutafuta masoko ya nje kwa hivi sasa haipo, kwa sababu mahitaji ya chumvi hapa Zanzibar ni tani 7500 mpaka 8000 kwa mwaka. Uzalishaji wa ndani wa hapa nchini ni tani 3000 mpaka 3500 kwa mwaka. Hiyo ina maana kwamba chumvi inayozalishwa nchini ni kidogo kuliko mahitaji na ndio maana kuna chumvi inayotoka nje. Mhe. Spika, ahsante sana.

**Mhe. Ali Abdalla Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba mashamba mengi ya chumvi bado hayajatimiza mia kwa mia kutia maadini ya *iodine*, lakini baadhi ya mashamba hayo chumvi hiyo inauzwa na kitaalamu inaambiwa kwamba chumvi hiyo haina *iodine* unapata maradhi ya *goitre*. Je, hao wakulima wa namna hiyo anawashauri nini.

b) Kwa kuwa bado vikundi vingi vya chumvi viko Pemba vinafika 50. Je, hapa Unguja anahamasisha vipi ili watu wajitokeze kulima hiyo chumvi ?

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Spika, ni kwamba uwekaji wa *iodine* unasimamiwa na wataalamu ndani ya *ZASPA* na kwamba *ZASPA* hairuhusu vikundi kuuza chumvi bila ya kuweka *iodine*. Kwa maana hiyo *ZASPA* wametoa vifaa maalum vya kujaribia chumvi kama ina *iodine* au haina iodine. Hapa ningetoa wito kwa wanunuaji kutumia vifaa hivyo na kujaribu chumvi wahakikishe kwamba ina *iodine* kabla ya kununua.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba vikundi vingi vinavyofika 55 viko Pemba na kwa hapa Unguja kuna vikundi 4 au 5 lakini ni maeneo mawili, eneo la Chukwani Buyu na eneo la Donge Muwanda ndiko wanakozalisha chumvi. Sasa Idara ya Viwanda itaendelea kufanya utafiti na kubaini maeneo kadhaa ambayo yangeweza kuzalisha chumvi na kuwaomba wananchi wafanye ushirika waingie katika uzalishaji huo. Kwa sababu tunategemea baada ya yote niliyoyataja kukamilika chumvi inayozalishwa Zanzibar itakuwa na sifa na viwango vinavyotakiwa na tutapunguza uagiziaji kutoka nje. Kwa hivyo, uzalishaji wa chumvi unaweza ukatoa ajira kwa vijana vijijini.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kwa kuwa Zanzibar hivi sasa tuna upungufu mkubwa wa vitu tunavyosafirisha, haoni kwamba chumvi inawezekana ikawa ni suluhisho la kuanza kupata kitu cha kusafirisha na tukaanza kushughulikia hii miradi ya chumvi ili tukaweza tukapata kitu cha kusafirisha na kuweza kujipatia fedha zaidi na ajira zaidi ?

b) Wizara imefanya utafiti wa soko katika nchi za *SADC* na imegundua nini katika soko hilo la nchi za *SADC ?*

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Spika, ni kweli kwamba inawezekana tukiwa na *production* kubwa ya chumvi yenye viwango vya kimataifa vinavyotakiwa chumvi ikawa ni zao la kusafirisha, inawezekana hilo. Ndio maana nikasema wizara inaendelea kufanya utafiti ili kubaini maeneo zaidi ya kuzalisha chumvi ili kutoa ajira zaidi kwa vijana, lakini chumvi itakapokidhi soko la ndani basi bila shaka tutatafuta njia ya kusafirisha.

Naomba nikiri, kwamba wizara bado haijafanya utafiti wa soko la chumvi ndani ya *SADC*, lakini tunachukua changamoto na tutafanya hivyo na kuona uwezekano wa soko katika nchi mbali mbali ili tuongeze uzalishaji hapa nchini.

**Nam. 12**

**Usomaji wa Mita za Majumbani**

**Mhe. Said Khelef Ali –** Aliuliza:-

Wasomaji wa mita za umeme huwa wanachelewa kufika majumbani kwa ajili ya usomaji wa mita hizo, aidha huchelewa kuleta bili kwa ajili ya malipo.

(a) Je, Mhe. Waziri kuna kitu gani kinachodhorotesha swali hili ?

(b) Je, Mhe. Waziri unaweza kuniambia idadi kamili ya wasomaji mita katika Mkoa wa Kaskazini Unguja ?

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 12 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa wasomaji wetu wa mita za umeme wanachelewa kusoma mita na kugawa bili. Hii inasababishwa na mpango mzima wa usomaji mita. Hivi sasa kila msomaji wa mita anasoma mita za wateja wasiopungua elfu moja na mia mibli (1200). Hivyo wateja wengine wanasomewa mita mapema na kupata bili zao mapema na wateja wengine husomewa na kupewa bili zao mwisho wa mwezi.

Mhe. Spika, wizara yangu imeliona tatizo hilo na tayari imo katika kukamilisha utaratibu wa kuajiri wasoma mita zaidi ili kuhakikisha kuwa mita zote zinasomwa kwa wakati na bili za umeme zinasambazwa mapema.

(b) Mhe. Spika, idadi kamili ya wasomaji wa mita kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja ni watatu (3). Hata hivyo, wizara kupitia Shirika la Umeme inakamilisha taratibu za uajiri wa wasomaji mita wengine wapya wawili (2) ambapo wanatarajiwa kuanza kazi mwezi wa Februari, 2009 ambapo itapelekea kuwa na wasomaji mita hao kuwa watano katika Mkoa huo.

**Mhe. Said Khelef Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri huoni kwamba msoma mita mmoja huyu kuanzia Nungwi hadi Bumbwini ni kuwa analeta usumbufu hasa kwa wananchi kwa sababu msoma mita huyu anaweza kuja tarehe 5 lakini mwezi mwengine akaja tarehe 10 huoni kuwa tunawapa mzigo mkubwa hawa wateja wetu.

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Spika, sio dhamira la Shirika la Umeme kuwapa shida wateja wake. Mhe. Spika, nchi yetu ina wateja wa umeme wapatao 87,000 Pemba wako 11,000 na waliosalia wote wako kisiwa cha Unguja. Tumechukua hatua kadhaa ambazo za kuondosha tatizo hili.

1. Kuendelea kwa kasi na mradi wa uwekaji wa mita za TUKUZA ambapo tukimaliza mradi wa awamu ya mwanzo kwa kufunga mita 20,000 ambazo tayari 13,000 zimeshafungwa, tukimaliza mita hizo 7000 tutakuwa na wateja wa mita za TUKUZA 40,000 kwa maana itakuwa tayari wateja tumeshawagawa mara mbili na tutakuwa zaidi ya nusu tayari wana mita za TUKUZA.

2. Tunaendelea na mradi huu wa kuhaulisha Shirika la Umeme kifedha ambao unaendelea vizuri na miongoni mwa sehemu za mradi huo ni kuongeza zaidi mita za TUKUZA na kutizama muundo huu wa utumishi na upangaji upya hasa hao wasomaji wa mita ili tuendelee upunguza shida hii wanayoipata wateja wetu.

**Mhe. Moh'd Ali Salim:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa utaratibu huu wa kusoma mita una matatizo kadhaa yakiwemo kuchelewa kusoma, wakati mwengine kukisia tu, kuchelewa kupeleka *bill*, wakati mwengine kupeleka *bill* kwa mdomo badala ya maandishi, upungufu wa wasoma mita.

Mhe. Spika, kwa kuwa kupambana na matatizo haya ufumbuzi wake ni kuwa na umeme wa mtu kwenda kununua akisha akaweka katika mita yake.

Je, katika mpango wake wizara inakusudia itakapofika mwaka gani watumizi wa umeme wote Zanzibar wawe na mita za TUKUZA wananunua na kutumia umeme katika mita zao.?

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Spika, haki ya mteja wa Shirika la Umeme si kupata bili ya makisio wala sikuletewa *bill* kwa mdomo, anapaswa kupata *bill* iliyosomwa na iliyokuja kwa utaratibu maalum wa *invoice* za Shirika la Umeme. Kutokana na matatizo tuliyoyaeleza awali ni kwamba kwa bahati mbaya sana haya yapo yanajitokeza. Kwa hivyo tunawaomba wateja wetu ni kwamba wanapokuwa hawana uhakika wa *bill* zao wafike kwenye vituo vya Shirika la Umeme kupata uthibitisho wasikubali *bill* za kukisiwa kwa mdomo wala *bill* za makisio kwa jumla wanapaswa kupata *bill* iliyokuwa na uhakika na wao kufanya malipo yao.

Mhe. Spika, mpango wa wizara ni kwamba ifikapo mwaka 2012 wateja wote wanaotumia umeme nchini mwetu kuwa na mita za TUKUZA.

**Nam. 5**

**Uimarishaji wa Huduma za Kilimo kwa Wakulima wa Zanzibar**

**Mhe. Ali Abdalla Ali –** Aliuliza:-

Kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu ambapo wananchi zaidi ya asilimia 70 wanategemea kuendeshea maisha yao, aidha ni sekta ya pili inayochangia pato kubwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, pembejeo na madawa ya kilimo ni ghali sana, kiasi ambacho wakulima wetu hawamudu kuzinunua na kuwapelekea kupata tija ndogo na kushindwa kufaidi matunda ya kazi yao.

(a) Je, Mhe. Waziri unajua kwamba mbolea ya chumvi inauzwa kwa bei ya Tsh. 60,000/= kwa mfuko mmoja wa kilo 50.

(b) Kwa kuzingatia ukweli kwamba bei hiyo iko juu sana kulinganisha na kipato cha wakulima wetu, je utakubaliana na mimi kwamba wakulima wetu wa vijijini hawamudu kuinunua mbolea hiyo.

(c) Je, Mhe. Waziri unafahamu kwamba, ili Mkulima aweze kupata huduma ya Trekta ya kuchimbuliwa eka moja, ni lazima achangie Tsh. 30,000/-; na vile vile achangie Tsh. 30,000/- kwa ajili ya kupata huduma ya kuburuza na kufanya 60,000/= kwa jumla.

(d) Kwa kuzingatia hali duni ya wakulima wetu. Je, huoni wakulima wengi hawawezi kumudu gharama hiyo.

(e) Je, serikali ina msimamo gani wa kuyaondosha matatizo hayo yanayowakabili wakulima wetu ?

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 5 lenye vifungu (a) , (b), (c),(d) na (e) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, napenda kumjuilisha kwamba bei ya mbolea ya chumvi/urea kwa mfuko mmoja wa kg 50 inauzwa kwa Tsh. 27,000/= na sio Tsh. 60,000/=.

(b) Pamoja na kwamba bei hiyo bado ni ya juu sana kwa wakulima wetu lakini bado serikali imeshafidia sana kwa kiasi hicho.

(c) Mhe. Spika, ukweli ni kwamba serikali haiwatozi wakulima gharama za kuchimbia wala kuvurugia lakini badala yake wakulima hutakiwa kuchangia gharama ya mafuta ya kufanyia kazi hizo. Gharama hizo hubadilika kulingana na bei za mafuta zinavyobadilika. Wakulima hutakiwa kuchangia lita 15 za diseli, kwa kulimiwa au kuvurugiwa ekari moja.

Mhe. Spika, mwanzoni mwa ukulima wa mpunga 2008/2009 bei za mafuta zilikuwa wastani wa Tsh. 2000/= kwa lita, hivyo bei hiyo ilikaribia kufikia sh. 30,000/= kwa ekari moja. Napenda kumuhakikishia Mheshimiwa kwamba bei ya mafuta imepungua sana kwa sasa hivi.

(d) Spika, ni kweli wakulima hawawezi kumudu kulipa gharama hiyo.

(e) Serikali kupitia wizara yangu hili suala tumeliona na iko mbioni kulitafutia ufumbuzi.

**Nam. 16**

**Mikakati ya Kuimarisha Kodi**

**Mhe. Ali Denge Makame** – Aliuliza:-

Kwa kuwa madai ya ukwepaji wa kodi mkubwa unaofanywa na baadhi ya makampuni hasa yaliyowekeza katika shughuli za utaliiu.

a) Je, tokea kuanzishwa kwa sekta ya utalii Zanzibar kumewahi kufanyika utafiti wowote wa kuchunguza ukwepaji wa kodi unaofanywa na baadhi ya wawekezaji ?

b) Kama utafiti huo ulifanyika nini matokeo ya utafiti huo na vipi matokeo hayo yameweza kufanyiwa kazi ili kusaidia ukusanyaji wa mapato ?

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi** – Alijibu:-

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 16 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kusema kweli hakujafanyika utafiti wowote wa kitaalamu kuhusiana na ukwepaji wa kodi unaofanywa na baadhi ya wawekezaji. Adiha, nakiri kwamba suala la ukwepaji wa kodi lipo na kwa kushirikiana na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji tunalifanyia kazi kwa pamoja suala hili. Hivi sasa Mhe. Spika, utaratibu unaotumika ni kufanya ukaguzi kwa wawekezaji wa miradi yote hasa katika sekta ya utalii na tayari wapo baadhi ya wawekezaji ambao wamegunduliwa na taratibu za kisheria zimefuatwa ikiwa ni pamoja na kuwapiga faini na hatimaye kuwataka walipe zile kodi ambazo wamepaswa kulipa.

Mhe. Spika, napenda kumjuilisha Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwamba tayari serikali hivi sasa imeshatangaza tenda kwa ajili ya kumpata mshauri mwelekezi ambaye atafanya utafiti huo ambao utawahusisha maeneo mbali mbali katika sekta ya utalii pamoja na yale maeneo ambayo yamebainika kupoteza mapato. Ni matarajio ya wizara yangu kwamba utafiti huo pia utasaidia kutoa mbinu mbali mbali za kupambana na upotevu huo wa mapato.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na kuwa wawekezaji ndio wanaokwepa kulipa kodi lakini inasemekana kuna sababu kubwa ambazo hawa wanaotoa nafasi za uwekezaji kupoteza kodi kwa mfano kodi ya ardhi kwa miaka 30 basi wote huwa hawaijui.

Mhe. Waziri hivyo kodi ya ardhi kwa mwekezaji mgeni kwa miaka 30 anatozwa kiasi gani ?

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, nakubaliana naye ni kweli kwamba kuna baadhi ya wawekezaji ambao wamekuwa wakikwepa hizi kodi za ardhi, lakini kwa kweli lazima niipongeze Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwani hivi sasa wamechukua hatua madhubuti na maalum na Mhe. Mwakilishi atakubaliana na mimi kwamba katika jimbo lake kuna baadhi ya wawekezaji ambao wamechukua maeneo wakayazungusha ukuta hawajayajenga. Walikodi ardhi hiyo ili wajenge lakini hawakufanya hivyo, basi ardhi hizo tumezichukua na pia baada ya kugundua kwamba hizo kodi za ardhi walikuwa hawalipi. Sina hakika kiwango cha ile bei ningemuomba Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi anisaidie kwa jibu sahihi la kiwango cha bei.

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Spika, naomba kusaidia jibu la ziada juu ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, kodi ya ardhi ina historia tangu ilipoasisiwa utaratibu wa uwekezaji na ukodishaji wa ardhi kupitia Sheria ya Usimamizi wa Ardhi Nam. 12 ya mwaka 1992. Miaka hiyo kodi ilikuwa inaanzia dola mia moja hadi mia tano kwa hekta na kila miaka ilivyokuwa ikiendelea imekuwa ikibadilika. Hivi sasa maeneo ya pwani kabisa yaliyokuwa mazuri yanakodishwa kwa kuanzia US$ 7,500 kwa hekta na kila ukipanda juu kwa maana ya maeneo ya maweni bei hiyo huwa inapungua. Pia ukodishwaji wa ardhi inategemea na mradi wenyewe. Kwa mfano, ikiwa mradi umepindukia dola milioni hamsini na kuendelea aghalabu wawekezaji huwa wanaiomba serikali kuwapunguzia kodi ya ardhi ili wapate unafuu katika kurejesha mikopo yao na kupunguza ule muda ambao wataweza kupata faida.

Nashukuru Mhe. Spika.

## Shughuli za Serikali

### Mswada wa Sheria ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho

*(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)*

**Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tena kwenye shughuli zetu za Baraza la Wawakilishi kutekeleza majukumu ya wananchi kama tulivyojikubalisha wenyewe.

Pili naomba uniruhusu na mimi niungane na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kutoa rambi rambi kwa wafiwa wa Mhe. Daud Hassan Daud Mwakilishi ambaye tumempoteza na tumuombe Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahala pema peponi. **AMIN**.

Mhe. Spika, sasa noamba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho ya mwaka 2009 kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 3(1) cha mswada huu.

Mhe. Spika, madhumuni makubwa ya kuwasilisha mswada huu wa sheria ni kuondosha utata uliopo katika sheria Nam. 6 ya mwaka 1983 ijulikanayo kwa jina la Baraza la Sanaa za Muziki, Ngoma, Michezo ya Kuigiza na Filamu za Sinema ya mwaka 1983.

Mhe. Spika, sheria hii ya Nam. 6 kama ilivyo jina lake imekusanya mambo mengi ambayo yanazihusisha taasisi mbali mbali kama kusimamia utekelezaji

wake. Matokeo yake kumekuwa na migongano ya taasisi katika kudhibiti maadili ya Mzanzibari wakati wa kusimamia sheria hizo na kuifanya kazi ya uhakiki wa sanaa, filamu na matangazo ya picha kuwa ngumu mno.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wananchi kwa jumla wamekuwa wakitoa malalamiko juu ya kuyaona maadili yetu, silka na utamaduni wa Mzanzibari yanavyoendelea kuporomoka. Kwa mfano, wajumbe na wananchi wanalalamika kuhusu aina ya filamu na sanaa zetu zinavyooneshwa hadharani bila ya kufanyiwa sensa na uhakiki.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haikuyapuuza malalamiko hayo. Baada ya utafiti wa kutosha imegunduliwa kwamba kasoro hizo zimetokana pamoja na mambo mengine mkanganyiko wa sheria Nam. 6 ya mwaka 1983 hii iliopo. Kwa sababu hiyo, wizara yangu imeomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu pendekezo la kuanzishwa Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho na mambo yanayohusiana nayo chombo ambacho sasa kitajitegemea wenyewe chenye nguvu za kisheria, muhuri wake na kitakachoweza kushitaki na kushitakiwa na kutekeleza mambo mengine yanayohusiana na hayo kwa mujibu wa sheria na kanuni zitakazotengenezwa na waziri.

Mhe. Spika, mswada huu unakusudia kuleta sheria ya kuanzisha Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho ili kulinda na kuhifadhi mila, silka, utamaduni na maadili ya Mzanzibari na kwamba sanaa sasa haitoruhusiwa kupotosha maadili hayo. Waraka huu unapendekezwa kuanzishwa bodi hiyo. Bodi hii itakuwa ni chombo cha juu kabisa kisheria cha kusimamia mambo ya filamu na sanaa za maonesho ambazo huoneshwa hadharani, sanaa hizo sasa zitafanyiwa uhakiki kabla ya kuoneshwa kwa jamii.

Mhe. Spika, rasimu ya sheria ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho itakuwa na sura tano zifuatazo:-

Sura ya Kwanza: Jina la tafsiri ya maneno.

Sura ya Pili: Kuanzishwa kwa bodi, wajumbe wa bodi, hadhi ya kisheria, kazi za bodi, muda wa wajumbe, uwezo na taratibu za bodi. Kuteuliwa kwa Afisa Mtendaji wa Bodi na itaelezea kazi zake.

Sura ya Tatu: Masuala ya fedha, matumizi na ukaguzi wa hesabu.

Sura ya Nne: Makosa na adhabu.

| | |
|---|---|
| Sura ya Tano: | Mambo mengineyo ambayo ni wizara kutunga kanuni na kufutwa kwa sehemu nyengine za sheria Nam. 6 ya mwaka 1983. |

Mhe. Spika, naomba kusisitiza kwamba mapendekezo ya mswada huu sio kuifuta sheria Nam. 6 ya mwaka 1983, badala yake mswada huu unapendekeza kufuta vifungu au kifungu cha 18 hadi 36 cha sheria Nam. 6 ya mwaka 1983 kama ilivyoelezwa katika sehemu ya tano kifungu cha 24 cha mswada huu ambacho kiko ukurasa wa 233.

Mhe. Spika, rasimu ya sheria hii ambayo sasa itakuwa ni sheria inayojitegemea iliyotokana na Sheria Nam. 6 ya mwaka 1983 ya Baraza la Sanaa na Muziki, Ngoma, Michezo ya Kuigiza na Sinema itasaidia sana katika kulinda maadili ya Wazanzibari yasipotoshwe.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa niwaombe wajumbe kwa heshima kubwa wauchangie mswada huu ili hatimaye waukubali na upitishwe katika kikao hiki cha Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii):** Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi juu ya Mswada wa Sheria ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kukutana hapa tukiwa na afya njema katika kutekeleza kazi zetu za kawaida za kujadili na kupitisha miswada mbali mbali ukiwemo mswada uliopo mbele yetu wa kuanzisha Sheria ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho.

Aidha, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kuwasilisha muhtasari wa taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi juu ya mswada niliokwisha uainisha hapo juu.

Mhe. Spika, pia naomba nichukue nafasi hii niungane na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mhe. Daud Hassan Daud aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magogoni. Kifo chake ni msiba mkubwa

kwa Baraza letu, familia yake na wananchi aliokuwa akiwawakilisha. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema Peponi – **Amin**.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya kamati nimshukuru Naibu Waziri Kiongozi ambaye pia ni Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na watendaji wa wizara yake kwa mashirikiano makubwa waliyotupa wakati tulipoujadili mswada huu.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila nisipowashukuru kwa dhati wajumbe wa kamati yetu kwa michango yao muhimu waliyoitoa wakati tulipoujadili na kuupitisha mswada huu muhimu.

Mhe. Spika, naomba niwataje wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Suleiman Ali | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Ame Mati Wadi | - | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ali Haji Ali | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Ali Mzee Ali | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Haji Faki Shaali | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Hasnuu Moh'd Haji | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Mohammed Ali Salim | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Raya Suleiman Hamad | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Salim Abdalla Hamad | - | Mjumbe |
| 11. | Ndg. Ramadhan Khamis Masoud | - | Katibu |

Mhe. Spika, Kamati imefurahishwa sana na hatua iliyochukuliwa na serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa kutuwasilishia mswada huu wenye lengo la kuanzisha Bodi ya Sensa na Filamu za Maonesho ambayo kisheria itakuwa na kazi ya kuhakikisha kwamba filamu na sanaa za maonesho hazipotoshi mila, silka na utamaduni wetu.

Mhe. Spika, kuwasilishwa kwa mswada huu hapa Barazani kunaleta faraja kwa Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakipiga kelele juu ya kuporomoka kwa maadili yetu kwa vipengele mbali mbali kikiwemo cha filamu za sanaa za maonesho.

Mhe. Spika, zimeelezwa sababu mbali mbali zilizopelekea kupotoshwa kwa maadili yetu kupitia filamu na sanaa za maonesho. Miongoni mwa sababu hizo ni kama zifuatazo:-

a) Kuwepo kwa sheria Nam. 6 ya mwaka 1983 ambayo imekuwa na kasoro nyingi zilizopelekea kukwaza utekelezaji wa sheria hiyo. Sheria hiyo imepelekea kuwepo kwa maingiliano makubwa ya kikazi kati ya Baraza la Sanaa na Muziki na Bodi ya Sanaa za Maonesho katika suala zima la kusimamia na kulinda mila, silka na utamaduni wa Mzanzibari.

b) Baraza la Sanaa limekuwa likitoa vibali vya maonesho mbali mbali kabla ya Baraza la Sensa na Maonesho kufanya kazi yake. Aidha, Baraza la Manispaa hutoa ruhusa ya kuweka mabango ya matangazo bila ya kuhakikiwa na Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho.

Mhe. Spika, mswada huu utakapojadiliwa na kupitishwa utaleta faida zifuatazo:-

1. Kuwa na chombo ambacho kisheria kitasimamia mambo ya filamu na sanaa za maonesho zioneshwazo na kurikodiwa hadharani kwa lengo la kulinda na kuhifadhi mila, utamaduni na silka zetu.

2. Taasisi zilizokuwa zikiingiliana kikazi sasa kila moja itakuwa na jukumu lake kwa mujibu wa sheria iliyopo.

3. Filamu za sinema, kanda za video, mabango ya biashara au matangazo maalum, majarida mbali mbali na maonesho yote ya michezo ya kuigiza na burudani za sanaa yatahakikiwa kabla ya kuoneshwa hadharani.

Mhe. Spika, matangazo ya shughuli za burudani, filamu zitakazorikodiwa ndani na nje ya Zanzibar kwa ajili ya kuoneshwa hadharani nazo zitahakikiwa kabla ya kuoneshwa.

Mhe. Spika, kamati inaona kwamba lengo la mswada linaweza kufanikiwa kwa mpango ufuatao:-

a) Bodi itakayoundwa itawezeshwa vilivyo kifedha kwa ajili ya kutekeleza kazi zake na mambo mengineyo.

b) Bodi itafanya kazi zake ipasavyo bila ya kuingiliwa au kutishiwa na mtu au chombo chochote chengine.

c) Bodi itafanya kazi zake kwa uadilifu.

d) Bodi itajitangaza kwa umma ili ipatikane kwa urahisi kwa ajili ya kupewa taarifa kuhusu kupotoshwa kwa maadili.

e) Taasisi za umma kama vile bandari, viwanja vya ndege, uhamiaji na vyombo vya usalama vitashirikiana kwa dhati na bodi katika kusimamia na kulinda maadili yetu.

f) Serikali na jamii itashirikiana vyema na bodi hii ili maadili yetu yalindwe na kutunzwa kama ipasavyo.

Mhe. Spika, hata hivyo wakati serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo imetuwasilishia mswada huu hapa Barazani kwa lengo la kulinda na kuhifadhi maadili yetu ni vyema pia tukafikiria namna ya kulinda na kuhifadhi maadili yetu kupitia televisheni zetu zikiwemo zile za *cable* na mtandao wa i*nternet* ambazo huonesha filamu na picha kinyume na maadili yetu ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, kamati imeufanyia marekebisho mswada huu na marekebisho hayo yamegawika kama ifuatavyo:-

1. Marekebisho ya mswada kwa kuongeza maneno ili usomeke vizuri. Mfano katika kichwa cha habari cha mswada badala ya neno 'maonesho' yameongezwa maneno 'ya mwaka 2009'.

2. Marekebisho ya mswada kwa kuzibadilisha irabu kwa baadhi ya maneno ili maneno hayo yaende sawa na maingiliano ya mpangilio wa maneno mengine. Kwa mfano, neno 'yeyote' badala yake lisomeke neno 'yoyote'.

3. Marekebisho ya mswada kwa kuongeza vifungu ili mswada uimarike zaidi mfano wa kifungu cha 8 kimeongezwa kifungu ambacho kimekuwa kifungu cha 8(1) ambacho kinaelezea idadi ya mikutano ya bodi kwa mwaka na uwezo wa kuitisha vikao vya dharura inapobidi.

4. Marekebisho ya mswada kwa kuviweka sawa vifungu au baadhi ya maneno ili ulete maana iliyokusudiwa kwa mujibu wa sheria inayotaka kufungwa. Kwa mfano, neno 'hadharani' lilionekana kutoleta maana iliyokusudiwa na badala yake kuandikwa vile ilivyokusudiwa kama inavyoonekana katika nakala ya marekebisho ya mswada ambayo kila mmoja wetu anayo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba uniruhusu kwa kuwa na mimi ni mmoja katika Wajumbe wa Baraza lako hili ingawa Mwenyekiti akishasoma

hotuba hii ndio inakuwa basi naomba kutoa maelezo kidogo kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani.

Mhe. Spika, nafikiri kila mwananchi katika nchi yetu hii ana haki ya kujua sheria zinazotungwa na sheria hizi ziwanufaishe wananchi wetu kwa ajili ya kulinda kama ulivyoelezewa mswada huu kwamba madhumuni yake ni kuhakikisha wananchi wetu wanakwenda sambamba na kulinda mila na desturi zetu. Tukitaka tusitake kila nchi ina utaratibu wake, nchi zote duniani hivyo ndivyo zilivyo. Kwa mfano, tukitoka hapa tukipata nafasi ya kwenda kutembea nchi za wezetu kama vile China, Ujerumani, Marekani, Uganda, Rwanda, Zambia mote humo mna desturi na mila zao ambazo ni nzuri na vivutio kwa watalii na watu wanaotembelea katika sehemu hizo.

Mhe. Spika, mimi naweza kusema kwamba Zanzibar tuna mambo mengi ya kujivunia kutokana na utamaduni wetu, mila na silka zetu, hizi zote tunaziacha bila ya kujitambua na tukaingia katika mila ambazo hazitusaidii. Naamini mgeni yeyote anapotoka nje kama atatembea katika nchi anayokwenda kutembea anaangalia mila za hapo ziko vipi.
Mhe. Spika, mimi nilipata bahati ya kutembea katika maonyesho mbali mbali na kukaribishwa katika maeneo ya shughuli za kienyeji mfano Rwanda. Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto bahati mbaya yuko nje hivi sasa angelikuwa shahidi wetu, ngoma za utamaduni za Rwanda ni nzuri sana tena ni za asili ambazo ukiziona utazipenda.

Rwanda hakuna mambo ya kujifunga kiuno, naomba radhi kusema hivyo, ukajikatia kama unavyotaka wewe, hakuna. Kule inakwenda mikono tu na jamii inaelimika kwamba ishara hii ya kuelimisha hivi na ukaweza kutokwa na machozi au la kufurahisha ukacheka, lakini hakuna chengine kinachofanya kazi katika mwili wako baada ya mikono tu. Namuomba Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo hili namuomba hii bodi yetu aipe fursa ya kutembelea katika nchi za karibu ili wakajionee vipi wenzetu utamaduni wao wanavyouthamini na watalii wanakuja kusoma kiasi gani.

Mhe. Spika, hata mazingira ya nyumbani ni utamaduni. Hapa niliuliza swali zuri sana juu ya usafi wa maeneo yetu katika nchi, ukimwambia mwananchi safisha mbele ya duka lako atakwambia aah! hiyo kazi ya Manispaa kumbe anajivunjia hadhi. Sasa utamaduni aliokuwa nao yeye ni wa kumrejesha nyuma lakini angekuwa anafanya kusafisha maeneo yake basi ingekuwa ni kigezo na utamaduni kwa mwengine na yeye akaiga.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba hii bodi Mhe. Waziri aipe uwezo itembelee nchi za jirani katika makabila mbali mbali ili wasome vipi watalii wanaweza

kutoka kwao wakenda kusoma kule juu ya mila na utamaduni wa nchi za wenzetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani na kwa niaba ya Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii naunga mkono kwa asilimia mia moja mswada huu. Pia ninaomba wenzangu wauchangie kwa hali na mali ili kuhakikisha wananchi wetu wanatutegemea, sisi tuwaweke katika mazingira mazuri ya kuelewa umuhimu wa kulinda mila, utamaduni, desturi na silka zetu kwa vizazi vyetu vijavyo.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono ahsante sana.

**Mhe. Najma Halfan Juma (Waziri Kivuli Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo):** Mhe. Spika, kwa niaba ya kambi ya upinzani sasa nawasilisha maoni yao kupitia Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Sensa na Filamu ya Sanaa za Maonesho na mambo yanayohusiana na hayo kwa kuunga mkono uanzishwaji wa bodi hii.

Mswada bila shaka umefika wakati muafaka ambapo sasa taifa letu la Zanzibar linahitaji dira yenye mwelekeo wa kudhibiti viashiria vyote vyenye kudhamiria upotoshaji wa maadili yetu. Hivyo kuundwa kwa bodi ni dalili tosha kwamba serikali sasa imebaini mwelekeo mzima wa maadili yetu tayari umemezwa na uhuru usio na mipaka. Nakusudia uhuru usio na mipaka kwa maana ya kutokuwa na udhibiti wa filamu na mambo yanayohusiana na hayo.

Pamoja na ufahamu wa maneno ambayo yamefafanuliwa maana yake bado kuna tafsiri isiyo sahihi ya aina ya michezo ya kuigiza inapoitwa ya kuigiza bila ya kuangalia utiwaji wake katika kundi hilo. Bado tunahitaji kuangalia michezo yetu ya kikwetu na Tanzania Bara, kwani baadhi ya michezo haiendani na ukweli juu ya utamaduni wetu ambapo tayari vyombo vyetu vya habari hurusha filamu au majukwaa yetu na kauli za burudani zimejengea umaarufu na kuvuta hisia hasa la rika dogo kiasi kwamba kwao mchezo wa kuigiza au filamu tayari umewapa mvuto.

Mhe. Spika, ipo mifano ya ngonjera ambazo maneno yatumikayo au vivazi vitumiwavyo tayari vimeathiri utamaduni wetu wa visiwani. Mmong'onyoko wa maadili kidogo ni mpevu hivi sasa Zanzibar na utandawazi umeshindwa kujizuia usitudhuru kwa sababu mianya kadhaa iko wazi bila ya kupata chombo kama hiki cha uangalizi. Nasema tupo kati bado hatujaelewa zaidi.

Tumekuwa na tafsiri nzuri katika mswada huu juu ya vipengele vilivyotajwa na kifungu cha 2 cha mswada lakini tafsiri hizi ni vyema ziangaliwe zaidi juu ya

visiwa vyetu na tusijifunge na kujihusisha kwengineko. Tafsiri tuitakayo ni yenye kutusaidia ndani yetu zaidi na tujihalalishie wenyewe. Tunaposema ngoma basi fikra zetu ziwe ngoma zetu na ngoma iwe ni ngoma, maana leo hii hata Maulidi ya Homu tayari yamegeuzwa kuwa ni kikundi cha sanaa wakati maneno ya Mwenyezi Mungu yanatumiwa katika Maulidi ya Homu, au neno nyumba ya burudani

bado kuna mashaka katika uhalisi wake kwani hata vilabu vya pombe sasa ni nyumba ya burdani. Mhe. Spika, nina mashaka kwamba mswada huu hautokuwa na nguvu ya kusimamia tafsiri yake pale vilabu kama hivi vitakapojitetea kulingana na mamlaka au wizara iliyotofauti na wizara iliyoandaa mswada huu.

Katika tafsiri ya sanaa sikubaliani na maneno noti kuingizwa. Hii inatokana na uwezo mdogo tulionao katika kuhoji, kuharibu au kuzuia jambo hilo ambalo mamlaka ya chombo chochote hapa Zanzibar haina uwezo huo.

Mhe. Spika, nikigusia sehemu ya pili ya kifungu cha nne nina wasi wasi na uwezo huo wa Bodi katika kulidhibiti hili hasa kulingana na uwezo mdogo wa teknolojia ya *Internet* au kupitia *satellite* ambapo asilimia kubwa sasa ya rika la vijana limetekwa na matumizi ya teknolojia hizo. Hivyo mswada uweke bayana uwezo huo jinsi ambavyo hautakuwa umedhibiti au kuhakiki kwa maana ya kudhibiti.

Mhe. Spika, kwa kuwa mswada huu unataja uundwaji wa Bodi sikubaliani na si halali hata kidogo mswada kutotaja wazi wazi nafasi ya viongozi wa kiimani au kiroho kutohusishwa kuwa wateuliwa. Kwani sote tunaelewa msaada mkubwa unatolewa wa kuelimisha na kujenga heshima ya jamii ya Kizanzibari ambayo Mashekhe au viongozi wa imani ya dini nyengine huwa wanahubiri juu ya mema na maovu hayo. Iwapo mswada huu utapewa nafasi ni vyema wizara husika iwe na jicho la mbali zaidi pale uteuzi wa wajumbe watakapokiuka uvumiliano wa kisiasa na kuifanya bodi husika kusikika katika sura ya kufaidika zaidi, wajumbe wa bodi hadi kusahau wajibu wao.

Mhe. Spika, nitakubaliana na mswada huu iwapo waziri atakuwa muwazi katika vifungu vilivyotolewa tafsiri na pia suala la uteuzi wa bodi na jinsi ya kukabiliana na mitandao ambayo inaipiku hali halisi ya muono wa mswada huu.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

**Mhe. Ali Abdalla Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kutoa mchango wangu wa mawazo katika mswada uliowasilishwa hivi asubuhi.

Mswada ambao ni muhimu na umekuja katika wakati muafaka pamoja na kuwa ulichelewa kidogo. Lakini mimi Mhe. Spika, nahisi pia haujachelewa kiasi hicho.

Mhe. Spika, baada ya kukushukuru wewe pia nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na waterndaji wake wote kwa kuweza kukaa na kutafakari na kuweza kutuletea mswada huu ambao naamini sababu na madhumuni imeelezwa kwa urefu sana, kwamba ni katika kulinda silka zetu na tamaduni zetu katika nchi yetu, ukilinganisha kwamba nchi yetu ni visiwa. Mhe. Spika, mimi naamini ukishapita mswada huu na ukafatiliwa uzuri, basi nadhani dhamira na malengo yale yaliyokusudiwa yanaweza yakapatikana.

Mhe. Spika, mimi kwa upande wangu mswada ni mdogo sana na sitokuwa na mambo mengi. Nina mambo mawili matatu.

Mhe. Spika, kwanza ni kutaka ufafanuzi na pili zile sehemu ambazo sikufahamu nipate kufahamishwa na mwisho nitoe mawazo yangu juu ya mswada huu.

Mhe. Spika, nikiingia kwenye mswada nianze hii sehemu ya mwisho ambayo inazungumzia sababu na madhumuni. Mswada umeeleza, sababu na madhumuni makubwa ni kulinda na kuhifadhi mila, silka na tamaduni zetu za Mzanzibari. Nadhani mtu yeyote akisikia hayo anajua dhamira ya mswada na mambo mazuri na uzuri huu ambao tumekusudia, na sisi tuweze yale yetu kuyadhibiti na yale ya nje yasiweze kuingia na kuvuruga yetu, kiufupi maana yake ni hiyo. Sasa nadhani kikubwa sasa hivi kwa kuwa tayari tumeanza kuutunga mswada huu, basi pia kuja kusimamiwa pakachukuliwa jitihada kubwa za kuweza kuusimamia.

Mhe. Spika, mchango wangu wa kwanza nitakuja kwenye ukurasa 228 sehemu ya kwanza utangulizi, hapa kuna ufafanuzi wa maneno. Kwa hivyo hapa kidogo na mimi nilikuwa nataka kufahamishwa baadhi ya sehemu ambazo sikuzifahamu. Tafsiri ya kwanza ambayo kidogo nilikuwa nataka nipate msaada kuna sehemu imetafsiriwa neno “burudani”.

Mhe. Spika, kuna matatizo sijui kama yamenikuta mimi ama na wezangu. Mhe. Spika, huu mswada wa rangi katika kusoma ni mgumu kidogo, sijui kwa kuwa sivai miwani au vipi. Lakini umenisumbua, usiku umenishinda niweza kuusoma hivi asubuhi. Sasa mimi nineomba tungejaribu kwa karatasi nyeupe na wimo mweusi tungeweza, kwa hivyo umetupa usumbufu sana. Sasa mimi nashauri kwamba safari nyengine kama karatasi hapa hapana, basi angalau tuagize kwa wenzetu Bara, tupate kitu ambacho kinaridhisha na unaweza kusoma bila ya matatizo.

Mhe. Spika, naomba unistahamilie kwa hayo matatizo niliyoyasoma. Burudani inasema hivi:-

Kujumuisha michezo ya sarakasi, karagosi, maonyesho ya dansa, picha, kazi za sanaa, muziki, tarabu, ngoma na mazingaombwe na mengine kama yapo.

Kwanza, mimi tatizo lango hili mazingaombwe, nilitaka nielezwe kiurefu mazingaombwe limekusudiwa nini. Kwa sababu ngoma tunajua kuna beni, kidumbaku. Sasa hii mazingaombwe ni nini, nilitaka nitafsiriwe, ili niweze kujua zaidi labda ingewekwa maana ni kitu fulani nadhani hii tuiweke wazi kwa wananchi.

Pili, filamu maana yake ni ukanda au sahani ya santuri iliyorikodiwa, maumbile yenye kutoa tafsiri ya kitu iwe kaseti au video na iliyokusudiwa kuonyeshwa hadharani. Mimi nadhani kwa sheria hii tuongeze na kitu hadhari ni uwanjani, kwenye kumbi na kila kitu. Lakini yapo mambo yanakuja hapa kisiri watu wanaoneshana majumbani na pia yanapotoa watoto wetu. Sasa mimi nadhanii tuweke si hadharani tu, lakini na siri kwa sababu hii ni sheria na huku mbele kuna adhabu. Sasa kama mtu anakuja na kitu cha siri akatizana na kikavunja maadili tutamkamatia kipengele gani. Sasa mimi ningeshauri na hapa isiwe hadharani, lakini tuongeze na siri vile vile.

Mhe. Spika, wako watu wanachukuwa kanda ambazo haziruhusu kuonyeshwa katika maadalili yetu, lakini watu wanajifungia usiku na wanaonyesha. Sasa mtu kama yule akikamatwa kwa sheria hii, hatuna pa kumshika, tuseme na siri vile vile. Kwa hivyo na wale wanaonesha kanda ambazo hazina ruhusa ki siri na wao wanaweza kukamatwa kwa mswada huu. Sasa mimi napendekeza hapo tuongeze na neno siri kama itakuwa ndio kisheria au itatafutiwa pahala, lakini bado kanda za siri ndio zinazopotosha utamaduni wetu.

Mhe. Spika, ya tatu kuna sehemu inaitwa michezo wa kuigiza pia pina matatizo kidogo. Hii inasema hivi inajumuisha mchezo wowote wa kuhudhunisha, kufurahisha, kuchekesha wa kufanya vitendo vya kuchekesha, uimbaji, kuigiza hadithi, ngoma, kuigiza mchezo unaoigizwa bila ya kutumia maneno.

Mhe. Spika, sasa mimi nilitaka nijue huu mchezo huo unaoigizwa bila ya kutumia maneno utatumia kitu gani, hata mtu huyo ajue mchezo huu unasema hivi na unaelekeza hivi kwa ishara. Mimi nadhani nipate maelekezo zaidi kwa sababu sifahamu. Mimi najua mchezo wowote kuna mtu anakuja na anazungumza yule anamjibu na yule anasema hivi. Lakini mchezo usiotumika maneno nataka ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, halafu nyumba inasema kuwa nyumba ya burudani maana yake ni nyumba yoyote, hema au jengo jengine la namna yoyote au mahali popote panapoonesha sinema, burudani au michezo ya kuigiza hadharani au kwa malipo inayojumuisha pia chombo cha nchi kavu au majini.

Sasa tukitaka kusema ukumbi wetu wa salama watu wanafanya harusi wanacheza ngoma tutie kwenye fungu gani, mwenzangu kazungumza hapa au kwenye Baa. Sasa hivi watu wanafurahi wanacheza na kila kitu, sasa hii itatiwa fungu gani katika tafsiri. Kwa hivyo, niliomba na hili vile vile kama limesahauliwa ama linaingia kwenye hii nyumba, basi nipate ufafanuzi akija Mhe. Waziri ili tuweze kufahamu zaidi.

Mhe. Spika, nikiendelea kwenye mchango wangu sehemu ya pili. Kuanzisha kwa bodi ya sensa ya filamu na sanaa za maonesho. Hapa nije moja kwa moja kwenye kazi za Bodi ukurasa wa nadhani 229.

Hapa inasema kazi ya pili ya Bodi kuhakiki filamu zinazokodishwa ndani au nje ya Zanzibar, kwa madhumuni ya kuonesha hadharani. Nadhani hapa imekusudiwa kwamba kama zitakuja filamu kutoka nje ama ndani kabla hazijaoneshwa katika jamii wao wanaziangalia kama kitu cha kutolewa kitolewe. Lakini kwa bahati mbaya ama nzuri mimi mwenywe binafsi nitatoa mfano kwa utoaji huu nitaohadithia hapa mimi siridhiki nao. Sasa kama kutakuwa na njia nyengine ya utoaji nadhani Mhe. Waziri akija atatuleeza.

Mhe. Spika, hivi karibuni mimi niliangalia TV, mimi si mtizamaji sana wa TV ukaoneshwa mchezo wa kimapenzi watu wamekutana kwenye kusoma wametaka urafiki wamekubaliana na wakaalikana, lakini wamekwenda mpaka wakafika nyumbani na wakanywa soda ukumbini wameondoka wakwernda mpaka chumbani, mtu akaanza kuvua nguo sasa ndio inakatwa, halafu mnakuta wamesharudi ukumbini. Sasa ukataji ule mtu umeshamueleza kama mimi mtu mzima najua kuwa wamekwenda kufanya nini na wameshafanya nini. Sasa pale hukupunguza lile jambo limeshajulikana. Sasa kama kupunguza, basi wako ukumbini wanakunywa soda kabla ya kwenda chumbani ni unakatwa unakuta wako pale pale ukumbini, kitendo hiki cha kwenda chumbani hakitojulikana.

Sasa nadhani katika upunguzaji wa sensa sifundishi kazi, lakini kimawazo yangu kama Bodi itakuwa inapata kanda kama hizi usingoje mtu akaingia chumbani, kwa sababu lile lengo la kwenda kule litajulikana na watoto watafahamu na chumbani, si lazima kwendea hilo tu watu wanakwenda kulala na kupumzika kule. Lakini kwa hapa mimi kwa filamu hiyo sikuona mimi faida ya kukatwa tungemaliziwa tu.

Sasa mimi naomba Bodi katika upunguzaji huo tungoje kitendo hicho mtu hajakifikiria yuko ukumbini anakunywa soda unajua wakitoka hapo watakwenda hatua fulani inakatwa, unaona wameshaingia garini na wanakwenda zao. Sasa nadhani hii ni ushauri wangu katika kupunguza haya mambo ambayo naamini itakuwa inatulinda kwenye tamaduni zetu.

Mhe. Spika, jengine kwa kuwa nimezungumza habari ya hizi filamu nitatoa mfano wa michezo mitatu mbayo nimehisi hapa petu tunao wasanii wengi sana wa michezo na nadhani kwa nchi za karibu, sisi tulitangulia kuonesha nichezo hii ya kuigiza hii kama ya kimaendeleo ya kimapinduzi ama ya kimapenzi. Lakini utakuta sasa hivi wenzetu wamekwenda mbali mno, na wametuacha mbali mno vile vile na nimewaza kwa nini wenzetu wametuacha, hivi nimeona wenzetu wameanzisha Vyuo vya Utamaduni na Sanaa ambao Bara wanacho Chuo Bagamoyo. Wasanii wetu wanakwenda wanasoma pale inakuwa michezo yao ya kule kwa mfano: Hivi karibuni niliangalia mchezo tuna msanii wetu anaitwa Chimbeni, lakini kwenye mchezo anaitwa Mashaka jina la mchezo. Huu mchezo unamaanisha uke wenza alioa wake wawili na kwa  bahati ana uwezo yeye alikuwa na maana ya ugomvi unatokeaje kwenye uke wenza. Sasa alijenga nyumba ya ghorofa mke mkubwa akamweka chini na mke mdogo akamuweka juu. Sasa kwa waswahili wakaona kaambuliwa mke mdogo kwa nini wa  mwanzo akae chini na mdogo akae juu. Lakini wenyewe waliridhiana na wakakubaliana.

Lakini uchochezi wa majirani wakamchochea yule mkubwa wewe mkubwa umewekwa chini nyumba yako mwenyewe yeye unajua anakaa juu na anakutemea mate wewe. Pakaingia ugomvi kwa nini mke mkubwa kawekwa chini na mdogo kawekwa juu. Mhe. Spika, hapa ukija kimantiki haina maana yoyote, lakini kwenye mchezo imeleta funzo, kwa nini wako wawili mmoja kaekwa juu na mmoja kaekwa chini, kama juu wote waweko juu na kama chini wote waweko chini.

Mhe. Spika, sasa hapa mimi nitakuja kwenye michezo wa wenzetu, mfano huku Bara sasa kuna michezo katika *DVD*, kuna mchezo sana anacheza Ray na Kanumba. Hawa wenzetu sasa michezo yao iko juu sana, kwa sababu ukikuta mchezo huo  na ukitizama na ile ya Nigeria huwezi kufananisha yaani ukisema kuwa huu wa Nigeria na huu wa Tanzania, isipokuwa utajua kuwa wamo ndani ya nchi yetu. Kanumba alicheza mchezo mmoja wa kutoa uaminifu kwa rafiki yake, huyu alisoma n na kwa  bahati akatoroka alifeli  na mwenzake akaendelea na kwa bahati Kanumba akahamia kijijini. Kule akawa mtu duni sana na rafiki yake aliporudi akawa milionea na yuko katika kutafuta biashara akamkuta Kanumba yuko katika hali mbaya sana, akamchukuwa kwa hali hii nikakuanzishe maisha akamwambia. Lakini mkeo atakubali mimi unichukuwe hapa ukaniweke kule. Akaenda mjini na kumweka vizuri akawa mzuri kuliko

yule Ray. Sasa mama uaminifu ukamtoa na huyu Kanumba na yeye vile vile akadanganywa kidogo na akaanza kumuibia rafiki yake.

Baada ya kuona vile mwanamke ameshajulikana na Kanumba ameshajulika akamuiba mke wa rafiki yake wakaja huku Unguja akamficha huku lakini huku nchi ndogo kauliza mwenyewe akapajua na akamkuta Kanumba kamuua kwa ufupi ni hivyo.

Lakini Ray yeye katunga mchezo wa kitamaduni wa nchi yetu sehemu ya kimasai. Yeye alikwenda soma Uchina na kule akapata rafiki wa kike na yule akataka lazima amuoe na akawambia mimi kwa tamaduni za kwetu huwezi akamwambia mimi kwa nilivyokupenda nitaweza. Kwa hivyo, Ray akatoka na mtoto wa kichina mpaka huku Tanzania umasaini akaanza kuvishwa yale madumwana ya shingo na nini.

Sasa kiufupi wale wenzetu wanatamaduni za kukeketa mchina akaridhika. Lakini baada ya kuona vile waswahili wa kule wakaona huku mchina kaweza kufata mila zote, haiwezekani atatuchafulia ukoo wakaanza kutaka kumuua. Bahati mbaya yule akarudi kwao China, lakini na China kugundua kwamba ameshatoka kwenye Utamaduni wa kwao wakamrudisha huku huku Tanzania bahati wakakutana na Ray na wakaoana. Ikawa sasa wametoroka kwao na mwanamke kaingia kwenye tamaduni si zake. Sasa ukisoma kiundani watu wanaweza kubadilika saa yoyote. Sasa haya yote yamefanywa na wenzetu ambao wamesoma na wamefaidika ziadi.

Mhe. Spika, na kidogo niingie kwenye mchezo wa kiganga. Nigeria wana michezo ya kiuganga, lakini ni ya kileo, kavaa suti na kila kitu, lakini uganga wa kwetu mtu kava nguo mbovu yumo ndani ya kibanda cha mgongo. Sasa ukitizama yale si maendeleo, kwa sasa hivi karne ya 21. Sasa lazima wasanii wetu na sisi tuwapeleke Chuoni ama wizara ianzieshe Chuo, ili tutoke kule kwa zamani twende na wakati kwa sababu na sisi tumo ndani ya dunia. Hilo ni wazo langu katika sanaa za kuiigiza.

Mhe. Spika, nikiendelea nije katika ukurasa wa 230 katika sehemu hiyo ambayo inazungumza Wajumbe wa Bodi. Bodi itakuwa na Mwenyekiti, lakini Mwenyekiti hapa kapewa sifa. Mimi nahisi bado hazijakidhi haja. Huyu Afisa mtendaji ambae atakuwa anahusika na hii dhamana kaambiwa kuwa awe mtu asiyepungua digirii ya kwanza au ya pili kisifa. Lakini sifa ya Mwenyekiti anaambiwa kuwa ni mtu aliyekuwa tayari, kawa mzoefu na kuelewa mambo ya utamaduni kwa muda mrefu.

Mimi nadhani utamaduni na mimi naujua na nauelewa. Kwa hivyo, mimi nadhani hata ukinichagua katika kiti hiki, naweza kuongoza. Lakini tunataka

na kitaaluma kwa sababu Vyuo vipo sasa hivi, je, kitaaluma Mwenyekiti mtu afikie fani gani, ningeomba hili kama limesahaulika, basi lingeengezewa nyuma ili tukapata mtu aliyekuwa mzuri katika bodi yetu, kwa sababu ukisoma kazi za bodi ni kubwa mno na zinataka mtu anaeweza kuwa mtaalamu.

Sasa kama muongozaji utaalamu ana wa kubahatisha, nadhani bodi haitokwenda kule kule ilikokusudiwa. Kwa hivyo nashauri Mhe. Waziri bado sifa kwa mimi binafsi za Mwenyekiti hazikukidhi haja, bado mkae na wataalamu wako ili mtoe mwenyekiti atakaeweza kuongoza bodi kwa dhamira iliyokusudiwa kwenye mswada huu.

Mhe. Spika, tuje kwenye sifa ambazo Mjumbe anaweza kuacha Bodi ana kutenguliwa kwenye Bodi.

(a) Iwapo mjumbe hatoweza kutekeleza kazi zake vizuri inakuwa katoka kwenye ujumbe wake.
(b) Sifa ya kwanza inasema kwamba kutokana na tabia mbaya na mwenendo mbaya.

Mhe. Spika, hapa mimi nadhani tusijizungushe hapo tungesema mtu akiwa mgonjwa na hakuyoko katika afya nzuri, hatekelezi kazi zake uzuri anajitoa kwenye Bodi. Wazo langu katika hii (a).

Mhe. Spika, nije ukurasa wa 231 hapa panazungumziwa: Bodi katika kutekeleza kazi zake, itakuwa na uwezo wa hii iliyoandikwa ya (c) kuweka na kuzipa nguvu kanuni za wafanyakazi na maadili ya wafanyakazi na nidhamu na viwango vya utendaji wa kazi kwa wafanyakazi wa bodi kuzipa nguvu kanuni. Sasa kanuni anatunga nadhani waziri na bodi inasema inataka kuzipa nguvu nilitaka nielewe nguvu hizo watatoaje ama watasimamiaje. Nilitaka maelezo ya ziada hapa, ili nifahamu kwamba akishatunga kanuni waziri bado za kanuni watazipa nguvu vipi katika utekelezaji wake, kwa sababu ukisoma haraka haraka kutaona ni kitu chepesi, lakini ni kitu kigumu. Sasa nataka kujua kuwa watatumia njia gani ya kuweza kuzipa nguvu hizi kanuni.

Mhe. Spika, nije ukurasa wa 233, huku nije kwenye sehemu ya tano unaambiwa ni “Mambo Mengineyo”. Nije kwenye makosa sehemu ya nne. Hapa imezungumziwa makosa kijumla na adhabu ya jumla. Mimi nadhani kungetafutwa njia nyengine za kuweza kutoa adhabu zaidi kwa sababu hapa imeelezwa kwamba mtu yoyote atayekuwa ameondosha filamu ama sehemu unataona kwamba makosa yamo zaidi ya 20, lakini adhabu ya aina moja tu, kwamba mtu atatozwa laki tano ama miezi sita.

Sasa mimi nadhani hii naona kama tumeripua tu. Tungekaa na tukaambiwa kuwa, labda mtu akiondosha filamu ama akilete filamu mbaya, adhabu yake kitu fulani. Ngoma mtu akicheza sivyo ilivyokusudiwa ama kaondosha maadili yetu, iwe kiasi kadhaa. Lakini hapa mambo yote yamechanganywa unaambiwa kuwa ukikamatwa na ukionekana na kosa, laki tano au miezi sita. Nadhani kuna makosa mengine hayalingani kutokana na uzito wa lile kosa. Sasa ningelishauri, kama wataalamu wamenifahamu, basi Mhe. Waziri nadhani iko haja tukayafafanua haya makosa, na baadhi ya makosa tukapunguza adhabu kuliko makosa yote tukaweka adhabu moja. Nadhani kwa mawazo yangu hayatokuwa mantiki nzuri.

Mhe. Spika, baada ya hapo nadhani nimemaliza. Mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa jimbo la Mfenesini, nawaomba Waheshimiwa wenzangu tuchangie na tuiunge mkono. Mimi kwa niaba ya wananchi wangu tunaunga mkono kwa asilimia mia moja na naomba upite, ili uweze kufanyakazi kulinda maadili na utamaduni wa nchi yetu. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Salmin Awadhi Salmin:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Spika, kwanza nianze mchango wangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwingi wa kurehemu kwa kuweza kutukutanisha hapa leo katika Baraza lako tukufu hili la Wawakilishi, kwa lengo la kuendeleza shughuli zetu na kazi zetu za Baraza.

Pili nimshukuru na nimpongeze Mhe. Waziri wa wizara hii Mhe. Ali Juma Shamuhuna na Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu, wakurugenzi mbali mbali na mmaofisa wao kwa kuandaa mswada huu wa sheria ambao kama Baraza lako tukufuu litaukubali na kuupitisha,. basi itakuwa ni sheria inayohusiana na masuala ya kuanzisha Bodi ya Filamu na maonesho na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwa kweli tuwapongeze sana viongozi wetu hawa kwa kufikiria jambo hili ambalo ni mara nyingi wananchi wengi wamekuwa wakilizungumza juu ya kukosekana kwa maadili na silka mbali mbali za watu wetu wa Zanzibar, na kwa haraka haraka basi wameweza kuchukuwa hatua ili kuona kwamba inakuwepo sheria ya kulidhibiti jambo hili, pamoja na kwamba huko nyuma kulikuwa na sheria. Lakini sheria iliyokuwepo hapo mwazo ilikuwa na mchanganyiko mkubwa. Lakini sheria hii inakusudia kuanzisha bodi maalum itakayoshughulikia jambo hili mahususi.

Mhe. Spika, mwezangu Mhe. Ali Abdalla Ali alizungumzia juu ya karatasi zilizotumika kuandaliwa huu mswada, karatasi za rangi hii. Kwa kweli alisema kuwa zinampa tabu kwa sababu hana miwani, lakini mimi ninayo miwani, lakini nami inanipa tabu hivyo hivyo.

Mhe. Spika, kama yalivyo madhumuni na sababu zilizopelekea kuandaliwa kwa mswada huu ambapo sheria inakusudia kulinda, kuhifadhi mila, silka, utamaduni, maadili na desturi zetu za wanzanzibari.

Kwa kweli madhumuni ya sheria hii na sababu kama nilivyotangulia mwanzo ukizitizama kwa mtazamo ni nzuri na inaonesha dhahiri kwamba sisi wenyewe tumeridhika na zile tamaduni zetu za kizanzibari, silka zetu, mila zetu. Lakini Mhe. Spika, tunapozungumzia suala la mila, silka na tamaduni za wanzanzibari, tunakusudia kwamba tunataka Wazanzibari twende katika mambo yaliyopita zamani. Inaonekana tabaan yameturidhisha ni mwenendo mzuri sana, ni mambo ambayo wazee wetu walikuwa wakiyatenda nyakati zile za kale.

Lakini pia ninajiuliza. Je, hivi sasa zile tamaduni za kale na silka za kizamani bado zina nafasi katika dunia ya leo ya utandawazi? Jibu la haraka haraka utaona hazina nafasi kwa wakati wa leo. Kwa sababu leo hii tunazo televisheni mbali mbali ambazo zinaonesha vipindi mbali mbali. Hebu tuangalie zamani tulikuwa na vyombo hivi? Ukiiangalia hii hii televisheni tunayoizungumza, sisi Zanzibar tulikuwa na televisheni yetu TVZ na tukajaribu kuiboresha na kuifanya iende katika mila na silka zetu za Kizanzibari. Tumejaribu kwa kila hali na kwa upande mmoja tunasema tulifanikiwa kwa sababu kulikuwa na vipindi vile vya mapema ambavyo baada ya muda watoto hawaruhusiwi kuangalia vinavyofuata, wanaangalia watu wazima. Vile vile tulikuwa tukiangalia mambo mbali mbali, ili kuona kwamba televisheni ile ya Zanzibar haiharibu silka na utamaduni wetu.

Lakini, leo hatuna televisheni ya Zanzibar tu, hapa Tanzania tuna televisheni mbali mbali ambazo zinaonekana vizuri tu ndani ya visiwa vyetu. Tunazo zile *cable* ambazo zinaonesha vipindi zaidi ya 52 ambazo zinapatikana hapa kwetu visiwani Zanzibar. Pia sasa hivi tunazo kompyuta zenye *internet* ambazo unapata fursa ya kuona mambo ya aina mbali mbali. Katika dunia hii ya leo ya utandawazi tuna sekta ya utalii ambayo huko nyuma haikuwepo. Sekta ya Utalii inapata nafasi ya kukusanya wananchi wa mataifa mbali mbali wenye tabia na silka tofauti, wote wanaingia katika visiwa vyetu.

Mhe. Spika, utashangaa unapopita mitaani sasa hivi kama kuna ligi kule Uingereza vijana na watu wazima wote masikio yao yako katika ligi inayochezwa kule. Huo ndio utamaduni wetu? Hawana habari kabisa, na ligi

zetu za Zanzibar. Siku inayocheza Manchester na Liverpool utakuta watu wamejaa katika televisheni. Ukiuliza leo kuna nini? Utaambiwa, leo ni Manchester na Liverpool. Kwa maana hiyo ulimwengu umepanuka.

Mhe. Spika, tulikuwa na ngoma za asili hapo zamani ambazo sasa hivi hazisikiki tena. Kwenye sherehe zetu, tulikuwa na ngoma ya mahumbwa ambayo ni nzuri tu, na ngoma nyengine mbali mbali za asili. Lakini, leo kwenye shughuli zetu za harusi, utakuta kuna rusha roho. Utaona kwamba mambo yetu ya zamani tulikuwa tunayapenda na tulikuwa tunatakiwa tuyasimamie vizuri, tuone kwamba yanaendelea na vizazi vyetu vijavyo wanapata nafasi ya kuyajua. Kijana wetu wa leo ukimueleza juu ya ngoma kama hizi za mahumbwa na nyengine, basi hana anachokielewa, lakini tunasema kwamba tuko katika dunia ya utandawazi.

Mhe. Spika, kwa kweli hatuwezi kupingana na wimbi la mabadiliko ya dunia. Hilo lazima tulikubali. Mhe. Spika, baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964, kulikuwa na sheria hapa ambazo zilikuwa zinamwelekeza Mzanzibari namna ya kuvaa nguo. Mwanamke hatakiwi kuvaa nguo ya kubana, sketi fupi, akivaa akishikwa na askari maana yake ni kosa la jinai na kulikuwa na hukumu zake. Hata mwanamme nae akivaa suruali ya chupa au lile buga pana, pia alikuwa anashikwa na kupelekwa katika vyombo vya sheria. Sheria zile zilikuwa kama hii sheria ambayo sasa hivi tunaipitisha. Zilikuwa na lengo la kulinda silka na utamaduni wa Mzanzibari. Lakini Mhe. Spika, tujiulize je, sheria zile zimefutwa au bado zipo? Kama zipo zinafanya kazi?

Sheria zile hazikufutwa zipo, lakini zimefutwa kutokana na hali ya mabadiliko ya dunia, na lazima tuyakubali mabadiliko yanavyokwenda. Leo hii utakwenda kumshika mtu kwa sababu kavaa suruali ya kubana? Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba mabadiliko ya dunia, ni lazima tuyakubali.

Mhe. Spika, tunapozungumzia majumba ya sinema labda tunayafahamu mimi na wewe, ambao tulikuwa huko nyuma tunayatumia kwa kwenda kuburudika. Lakini hebu tuangalie watoto wa leo, ukimwambia jumba la sinema atafahamu kitu gani, haelewi. Kwa sababu majumba yenyewe ya sinema hayapo. Tulikuwa na majumba matatu hapa ya sinema. Lilikuwepo *Cine Afrique*, lakini sasa hivi sijui limegeuzwa kitu gani. *Empire* siku hizi imekuwa *Super Market, Majestic* sijui limegeuzwa kitu gani. Kwa hivyo hayo majumba yenyewe ya sinema hayapo na kilichosababisha yapotee ni masuala haya ya vyombo vilivyokuwepo sasa hivi. Watu wanapata michezo mbali mbali kwa kutumia kanda mbali mbali. Kwa hivyo, majumba yale ya sinema yameonekana sasa hivi hayafai na hayaendani na wakati na ndio maana unakuta yanapotea.

Mhe. Spika, hii ndio hali halisi ya Zanzibar ya leo na kama nilivyotangulia kusema kwamba ni lazima tukubaliane nayo. Mhe. Spika, kama nilivyosema awali kwamba nakubaliana na hoja ya mswada huu, imekuja wakati wake, ina madhumuni na malengo mazuri. Lakini je, inaweza ikafanya kazi kama tulivyokusudia kwa wakati huu tuliokuwa nao? Jibu hatujui.

Mhe. Spika, baada ya dibaji hiyo sasa niingie kidogo ndani ya mswada wenyewe. Mswada huu ni mdogo sana, lakini umekamilisha mambo yote kama yalivyokusudiwa. Kwa hivyo, kidogo tuingie humu ili tuone kwamba ama tunatoa mawazo yetu juu ya vifungu mbali mbali au kama tuna maswali tupate nafasi ya kuuliza, ili Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, basi afanye majumuisho ya pamoja.

Mhe. Spika, katika Sehemu ya Pili ya mswada inazungumzia kuhusu Kuanzishwa kwa Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho, ambapo kifungu cha 3 kinaelezea namna bodi itakavyokuwa. Kifungu cha 4 cha mswada kinazungumzia kazi za bodi. Sasa mimi nitatoa mawazo yangu hapa kwenye kifungu cha 4.

Mhe. Spika, naomba nikinukuu kifungu cha 4 (a) kinasema:

Kifungu cha 4 (a):

> "Kuhakiki filamu za sinema, kanda za video (CD, DVD, HDV) na nyenginezo, mabango ya biashara na matangazo maalum, majarida mbali mbali kabla ya kusikilizwa na kuoneshwa kwa jamii."

Sasa neno kuhakiki kwenye *interpretation* huku halikujitokeza kwamba tunapozungumzia suala la uhakiki tunakusudia kufanya nini. Lakini neno uhakiki limejitokeza kwenye tafsiri ya neno sensa, ambayo inasema maana yake ni ukaguzi au uhakiki, bado imejirejea ule uhakiki. Lakini kifungu kinasema kuhakiki filamu za sinema, pengine inatupitikia labda kuangalia, kutazama kwa mtazamo wangu. Pana neno hapa mabango ya biashara, hili ndio kidogo lililonipa *headache*. Mabango haya ya biashara ni biashara ipi? Kwa sababu pia nimetizama huku kwenye *interpretation*, tafsiri ya mabango ya biashara haikuonesha. Kama tunavyojua katika mji wetu wa Zanzibar, tuna mabango ya biashara ya aina mbali mbali. Kuna haya yanayokusudiwa katika mambo ya biashara, kuna haya ya mambo ya mila kama yale ya Bi Kidude na Bwana Bakari Abeid barabarani. Lakini hapa haikuainishwa ni biashara zipi au ni mabango yote yaliyokuwepo katika mji. Sasa, kidogo hapa tulikuwa tunahitaji ufafanuzi juu ya haya mabango ya biashara yaliyokusudiwa hapa. ni yote yatahakikiwa hata yale ambayo hayahusiani na sheria hii?

Mhe. Spika, kifungu cha 4 © naomba kununukuu kinasema:

Kifungu cha 4 ©:

> "Kuhakikisha kwamba filamu zote zinazorekodiwa ndani na nje ya Zanzibar na zinapata usimamizi wa bodi wakati wa kurekodi, ili kulinda maadili na utamaduni wa visiwa vya Zanzibar".

Lakini bahati nzuri hapa kifungu hiki kimefanyiwa marekebisho nilipokiweka ilikuwa bado hatujapata haya marekebisho.

Kifungu cha 4 (d) naomba kununukuu kinasema:

> "Kufanya uhakiki wa maonesho yote yanayohusu michezo ya kuigiza na burudani nyengine zote za sanaa".

Mhe. Spika, kama unavyojua sasa hivi nchi yetu hii imekuwa. Mambo haya yanayozungumzwa hapa ambayo yanatakiwa kuhakikiwa na bodi yapo mengi. Mambo ya burudani, michezo ya kuigiza, michezo wakati mwengine inazuka tu ndani ya burudani. Sasa unapozungumzia kufanya kazi ya uhakiki wa maonesho yote yanayohusu michezo ya kuigiza, hapa kidogo nadhani tutapata kazi ya ziada. Watahakiki vipi hawa? Maana yake kuhakiki ni kufanya lile jambo ambalo linatakiwa kabla ya kulifanya, liwe limeshasahihishwa kwamba hili sasa ni sahihi kwa hivyo endeleeni kulifanya.

Mhe. Spika, kifungu cha 4 (d) nahisi bodi itakuwa na mzigo mkubwa sana kwa sababu maigizo ni mengi, maonesho ni mengi, kwamba kabla ya jambo lolote kufanyika bodi kwanza ifanye uhakiki juu ya maonesho au michezo ile ya kuigiza. Hapa kidogo tunahitaji kusudio hasa lililokusudiwa, ni lipi ili tuwe na utekelezaji bora wa sheria yetu, isije ikabakia kama zile sheria nyengine ambazo zipo tu, lakini haziwezi kufanya kazi.

Lakini Mhe. Spika, naunganisha hapo hapo naomba kununukuu kifungu cha 4 (i) kinasema:

Kifungu cha 4 (i):

> "Kutoa ruhusa kwa filamu za sinema, kanda za video, michezo ya kuigiza na burudani, nyimbo za taarab, ngoma, muziki na nyenginezo".

Kwa maana hiyo, maeneo hayo baada ya kuhakikiwa sasa bodi ndio itaruhusu, kwamba mchezo huu wa kuigiza uendelee. Kwa hivyo, bado ninaonesha mashaka yangu juu ya vifungu hivi ambavyo nimevitaja.

Mhe. Spika, kifungu cha 5 (1) kimezungumzia Muundo wa Bodi, ambapo bodi itaundwa na wajumbe wafuatao ambao wameelezwa hapa chini. Mhe. Waziri amepewa nafasi ya kuteua wajumbe wasiozidi sita kutoka katika mikoa yote ya Zanzibar, ambao ni mahiri katika taaluma ya utamaduni na sanaa. Mimi hili sina tatizo nalo, isipokuwa kuna wenzetu ni mara nyingi wamekuwa na malalamiko na yanakuwa ni ya kweli kwa sababu yanaambatana na dhana halisi ya ushirikishwaji. Hizi taasisi binafsi mara zote zinakuwa zinalalamika, kwamba hatushirikishwi pamoja na kwamba kauli ya serikali inasema kwamba tutafuata mfumo ule wa *Private Public Partnership (PPP).* Lakini, bodi zetu mara zote tunakuwa hatuwashirikishi hawa.

Kwa hivyo Mhe. Waziri pamoja na muundo huu uliokuwepo sasa hivi, basi hebu tuangalie ni taasisi zipi angalau tupate japo wajumbe wawili waingie humu kwenye bodi, kwa sababu hawa watatusaidia katika utekelezaji wa shughuli zetu na mambo yetu. Hawa ni wadau wetu wakubwa sana. Tungeomba katika hizi nafasi zako sita, uchukue nne hizi mbili zipelekwe katika vyombo hivi, ili hii dhana ya ushirikishwaji wa wananchi wa hizi taasisi za kiraia, basi ionekane inatimia.

Mhe. Spika, suala hili nitalizungumza katika bodi zetu zote tunazokwenda nazo sasa hivi, kwamba angalau tuwe na wajumbe kutoka katika taasisi za kiraia. Tumekuwa tukipata malalamiko kila siku, kwamba serikali dhana yenu inakuwa hivi, lakini hamtushirikishi ndio maana mambo yanaharibika. Ukiangalia ni kweli. Kwa hivyo tuwashirikishe hawa, ili yale maamuzi tunayopitisha mara zote yawe ya wote.

Mhe. Spika, naomba kunukuu kifungu cha 7 (1) kinasema:

Kifungu cha 7 (1):

> “Waziri anaweza kutengua au kusimamisha uteuzi wa mjumbe yeyote aliyemteua chini ya kifungu cha © cha sheria hii.”

Mhe. Spika, nilikuwa najiuliza kwa nini iwe © peke yake. Naomba kunukuu kifungu © kinasema hivi:

Kifungu ©:

> "Ikiwa mjumbe atapatikana na kosa la jinai likiwemo la udanganyifu, kutokuwa mwaminifu na tabia mbaya."

Huyu sasa Mhe. Waziri anaweza kutengua au kusimamisha uteuzi wake. Lakini vifungu karibu vyote, navyo vinahusika na kifungu hiki cha Mhe. Waziri kumsimamisha. Naomba kunukuu kifungu (a) kinasema:

Kifungu (a):

> "Iwapo mjumbe hawezi kutekeleza kazi zake."

Kifungu (b):

> "Kutokana na tabia mbaya au mwenendo mbaya."

Huyu maana yake amekuwa hafai kwa mujibu wa sheria hii. Lakini tumemnukuu kifungu kimoja tu cha (c). Kwa hivyo Mhe. Spika, nilikuwa nahisi bado katika vifungu hivi, isiwe specific tu (c) viangaliwe vyote, ambavyo ikiwa mjumbe atakuwa na udhaifu juu ya hili, mbali ya maeneo haya mengine, basi Mhe. Waziri apate nafasi ya kumsimamisha na kufanya uteuzi mwengine.

Mhe. Spika, chengine ni kifungu cha 8 naomba kunukuu kinasema:

Kifungu cha 8:

> "Bodi inaweza kuweka utaratibu wa kuendesha shughuli zake za jumla na zinazohusiana na uitishaji wa mikutano, taarifa, taratibu katika mikutano ya bodi, utoaji na ukaguzi wa kumbukumbu za mikutano ya bodi na mambo yanayohusiana nayo."

Hili suala, bodi inaweza maana hailazimishwi. Hivi karibuni tulipokuwa kule *Zanzibar Beach Resort*, mwalimu wetu alitwambia mara zote katika sheria neno inaweza lisijitokeze. Kwa sababu anaweza maana yake linaacha uhuru, na hili jambo ni la lazima. Kwa hivyo kama kuna bodi inaweza, basi iwe ina kitu cha kulazimisha. Kwa sababu suala la kuweka utaratibu na kuendesha shughuli zake ni jambo la lazima. Kwa hivyo kama huko kwenye sheria mnayosema ya Kiingereza kuna *may* basi tuweke *shall,* ili jambo hili liwe linalazimisha.

Tuna mifano Mhe. Spika, tumeanzisha sheria yetu hapa ya Haki, Kinga na Fursa za Wajumbe ambayo nayo sheria inasema hivi hivi, kwamba waziri

anaweza kutunga kanuni inatumika sana. Mpaka leo kanuni haijatungwa. Kanuni ya utekelezaji wa Sheria ya Haki, Kinga na Fursa za Wajumbe tumepitisha, lakini mpaka leo haijatungwa namna ya kuiendesha ile sheria. Pia, kuna *practise* ya sheria nyengine mbali mbali, lakini na hii inatokana na hii *may*. Kwa hivyo neno hili nadhani tuliweke vizuri, ili bodi sasa ilazimike kufanya mambo yake.

Mhe. Spika, pia katika kifungu cha 22 Sehemu ya Tano, ambapo Mhe. Waziri anaweza kufanya marekebisho ya kanuni kwa ujumla, ili kutoa uwezo wa utekelezaji mzuri wa sheria hii. Nayo imejitokeza tena, hii anaweza, kwa hivyo inamhiarisha. Lakini huwezi kusimamia na kuendesha sheria hii bila ya kuwa na kanuni, kwa sababu sheria haiwezi ikamaliza kila kitu. Kwa hivyo, na hapo basi sheria hii imlazimishe waziri kutunga kanuni za uendeshaji bora wa sheria.

Mhe. Spika, nadhani kwa mchango wangu huo mfupi kidogo na maelezo yangu ambayo nimeyatoa, Mhe. Waziri atayazingatia na kuyatolea ufafanuzi. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Magomeni tunakubaliana na mswada huu na tunaunga mkono. Nawaomba na wajumbe wenzangu tuuchangie vizuri kwa mustakbali mzuri wa nchi yetu, ili tuone kwamba silka, mila na utamaduni wetu sisi wenyewe na vizazi vyetu haupotei. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ya kutoa mawazo yangu japo kwa uchache kuhusu mustakbali wa jamii ya Wazanzibari. Mhe. Spika, madhumuni ya mswada huu kama alivyotueleza Mhe. Waziri, ni kujaribu kulinda silka, mila, maadili na utamaduni wa Mzanzibari. Mimi binafsi labda niseme leo nimeshukuru sana kwa mara ya kwanza serikali inaliona hili, kwamba kuna haja ya kulinda mila, silka, maadili na tabia ya Wazanzibari. Ni kilio changu cha muda mrefu. Kumbukumbu zitasema suala hili siku za nyuma nilikuwa nalipigia makelele sana.

Lakini Mhe. Spika, mambo haya ya mila, silka, maadili na utamaduni wa Mzanzibari yana tafsiri pana sana, na sidhani kabisa kwamba Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo pekee inaweza kuyalinda mambo haya. Wao watajitahidi kwa sehemu ndogo sana. Mhe. Spika, nadhani yangehitaji na taasisi nyengine nyingi za serikali, zishiriki katika kulinda mambo haya muhimu sana kwa jamii yetu. Labda niseme miongoni mwa silka, tabia na mila za Wazanzibari ni kuvaa nguo zao vizuri.

Mhe. Spika, siku za nyuma ilikuwa ni mwiko kumwona Mzanzibari anatembea kichwa wazi, Wazanzibari wote walikuwa na tabia, mila na silka zao nzuri za kujitanda mashungi vizuri sana. Huwezi kutoa tafsiri ya mwili wao isipokuwa kwenye kipaji cha uso na miguu. Hii ndio ilikuwa silka ya Wazanzibari.

Sasa nasema si rahisi kwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kuyalinda haya kwa sababu tayari tumevamiwa na wimbi kubwa la wageni wanaoingia humu. Mhe. Spika, kwa kweli wengine huwezi kuwatazama kwa macho yako, yaani sio ataona aibu yeye yule anayetazamwa, lakini utaona aibu wewe unayetazama. Sasa hawa si jukumu la Wizara ya Habari. Hawa wanachangia kwa kiasi kikubwa sana katika kupotosha na kuwafanya Wazanzibari wetu, waige mila ya kwenda ovyo bila ya nguo.

Sasa nadhani hataishia Mhe. Waziri katika wizara yake hii ya habari atatumia cheo chake cha Naibu Waziri Kiongozi, kuzishawishi au kuzitaka na taasisi nyengine nazo zidhibiti mambo haya. Kwa sababu utakapoweza kuwadhibiti wageni wanaoingia Zanzibar wakija hapa walazimike kuvaa vizuri kama wanavyovaa Wazanzibari, basi nafikiri utakuwa umefanya jambo moja kubwa sana na muhimu na hili Mhe. Spika linawezekana.

Mhe. Spika, mimi nilisoma sekondari pale Chuo cha Kiislamu, siku hizo Mkuu wa Chuo alikuwa ni marehemu Sheikh Mussa Makungu, tunamkumbuka wengi, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema. Alikuja mwalimu mmoja wa Kiingereza anaitwa Miss Wilson, alikuwa anasomesha Kingereza pale, alipokuja yule mwalimu alikuwa anatamaduni za kikwao huko, alikuwa anavaa viguo mpaka hapa kwenye magoti. Marehemu Mzee Mussa akamwita ofisini kwake, akamwambia umekuja hapa, uko katika Chuo cha Kiislamu, hapa miongoni mwa kazi zetu ni kufundisha maadili ya Wazanzibari, kwa hivyo hatutakikukuona kuvaa nguo za namna hii. Basi akauliza nivae zipi, akafahamishwa uvae nguo refu, basi yule mzungu siku ya pili tu alikuja na nguo refu mpaka alipomaliza muda wake hapa.

Sasa ndio nasema kumlazimisha mgeni avae nguo zinazostahiki kwa hapa Zanzibar ni jambo linalowezekana, ilimradi tu serikali iwe *serious*. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Naibu Waziri Kiongozi asimalizie katika wizara yake kulinda hizi mila na silka za Wazanzibari, lakini atumie wadhifa wake huo kuzishawishi na taasisi nyengine zijitahidi kadiri ya uwezo wao, ili kuhakikisha kwamba mila na silka za Wazanzibari zinalindwa. Ni kweli kuna mambo ambayo hatuwezi kuyadhibiti, kama walivyoeleza wenzangu waliotangulia, lakini tukijitahidi tunaweza kufika hatua kubwa na tukaonekana kama tuko *serious.*

Mhe. Spika, baada ya dibaji hiyo, naomba sasa niingie kwenye vifungu kidogo. Kabla sijaanza vifungu nataka niungane na Waheshimiwa wenzangu waliotangulia kusema kwamba karatasi za namna hii kwa kweli zinatupa tabu kidogo, pamoja na kuwa nina miwani, lakini bado nalazimika kuchunguza

sana. Sasa tunaomba turudishiwe ule utamaduni wetu wa karatasi nyeupe na hati zilizokuwa kubwa kidogo sio kama hizi.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 229 kifungu cha 4(i) hapa kuna kazi za bodi kwa jumla, hiki kifungu 4(i) kinaeleza, Mhe. Spika naomba nikisome hapa

Kifungu cha 4(i)

> "kuhakiki filamu zinazorekodiwa ndani na nje ya Zanzibar kwa madhumuni ya kuoneshwa hadharani".

Mhe. Spika, ninaungana sana na Mhe. Ali Abdalla ndio nikasema kuwa kanifilisi, tukisema hadharani pekee itakuwa hiki kifungu hakikidhi haja iliyokusudiwa, kwa sababu siku hizi kuna ajira moja kubwa sana ambayo vijana wanayo, hakuna mtaa wowote wa mji huu wa Zanzibar na hata sehemu za ng'ambo kulikokuwa hakuna haya maduka ya kuuza kanda zile video na CD za redio ambazo ziko nyingi sana. Zile nyengine hazirikodiwi hapa Zanzibar, zinaagiziwa kutoka nje pengine Mombasa au Dar es Salaam na kwengineko.

Kanda hizi vijana wanazipenda sana na wala hazina maadili hata kidogo. Hazioneshwi hadharani, lakini zinaoneshwa majumbani na zinaathiri sana kwa sababu pamoja na kuwa watoto wakiangalia zile kanda zinapotosha zile tabia zao, maana yake wanaona mambo yasiyostahiki kuonekanwa, lakini pia zinawapotezea wakati wao wa masomo, kwa sababu ni mambo ambayo ni *very interesting*. Mtu anawacha buku la mambo yake ya shule akaangalia pale mpaka muda akaumaliza mpaka saa 8:00 za usiku, akimaliza pale anakwenda kitandani hakupitia buku lake. Kwa hivyo, inatuathiri hata kimasomo.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana hii bodi ikiwezekana ama izuwie leseni za zile kanda kwa yale maduka ya kanda au kama sio kuzuwia leseni, basi ni kufanya uhakiki mkubwa sana, ili kuhakikisha kwamba kanda zinazouzwa mle zinakuwa salama. Zile ambazo haziendani na haya tuliyoyakusudia hapa, basi zipigwe marufuku mara moja.

Jambo jengine ni katika kifungu hicho hicho cha 5(1)(a), pale pana muundo wa bodi na hiyo (a) inataja uteuzi wa Mwenyekiti. Nataka niungane na wenzangu, maana yake hii imesema naomba kukisoma Mhe. Spika.

Kifungu cha 5(1)(a)

> "Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais na atahitajika kuwa na sifa ya uelewa wa fani ya utamaduni na mwenye kuheshimika".

Sasa hii ndio sifa yake awe na uelewa wa fani ya utamaduni, lakini huyu ni Mwenyekiti wa bodi ni chombo kikubwa sana hiki. Kuna mtu mwengine ana uelewa wa fani ya utamaduni. Samahani kama nitakuwa nimekosea, lakini hata mzee Haji Gora anao uelewa huo, kwa kweli anaweza kuwa Mwenyekiti wa Bodi Mzee Haji Gora. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri angetutajia hasa sifa za kielimu, kwa sababu hii bodi ni taasisi kubwa. Kwa hivyo, kumweka mtu mwenye sifa ndogo ndogo tu kama zile haitokuwa rahisi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilikuwa naomba pafanyiwe marekebisho madogo ili pawe na sifa ya kielimu hasa ambayo inahusu mambo haya ya utamaduni, kwa sababu watu wanasoma. Kuna taasisi ya Kiswahili hapa inatoa mpaka madiploma na sasa hivi imegeuka imekuwa ni SUZA, lakini bila shaka yatakuwa yanaendelea yale mambo kama yale. Kwa hivyo, atafutwe mtu mwenye sifa zinazokubalika.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nije kwenye kifungu cha 7(1) ambacho kinaeleza kwamba waziri anaweza kutengua au kusimamisha uteuzi wa mjumbe yeyote aliyemteua chini ya kifungu cha (c) cha sheria hii. Hapa mimi sina tatizo kubwa, nafikiri tatizo lenyewe ndani ya sheria hii hamna kifungu cha (c), na ikiwa kifungu cha (c) kilichokusudiwa ni hichi cha juu, basi ni kifungu cha 5(1)(c) sasa ikiandikwa kifungu cha (c) tu kinababaisha sana. Maana ukiangalia (c) pengine narudia hii 7(c) ambayo haizungumzi habari ya Wajumbe kabisa. Sasa naomba irekebishwe hiyo.

Jambo jengine Mhe. Spika, ambalo nilitaka nalo nilizungumze kidogo ni hiki kifungu cha 7(1)(c) sasa, naomba ninukuu.

Kifungu cha 7(1)(c)

> "Ikiwa mjumbe atapatikana na kosa la jinai likiwemo la udanganyifu, kutokuwa mwaminifu na tabia mbaya.

Mhe. Spika, huyo ni mtu ambaye anaweza kutenguliwa ujumbe wake au kusimamishwa. Mhe. Spika, hii imezoeleka sana katika sheria tunazozitunga. Mara nyingi mtu mwenye kosa la jinai huelezwa kukosa sifa za ujumbe hata wa Baraza lako tukufu Mhe. Spika imo hii. Kama mtu atapatikana na kosa la jinai na atafungwa kifungo cha miezi sita ama zaidi, basi huyo anakosa sifa za kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mimi sio mwanasheria, lakini nahisi hapa pana kasoro. Kwa sababu kupatikana na kosa la jinai pengine mara moja ndani ya maisha ya mtu, basi hakujamfanya mtu huyo awe na tabia mbaya au uwe huo ndio mwenendo wake wa kutokuwa muaminifu pengine ni ajali tu.

Mhe. Spika, utakuta kuna watu wengine wanafanyishiana. Mtu anaweza akafanya jambo akakusingizia na kwa bahati mahakama baada ya kuchunguza na wanaochunguza pale mahakamani ni binadamu kama sisi wakashindwa kugundua kama yule mtu kumbe kasingiziwa, kwa hivyo akapatikana na kosa na akahukumiwa kifungo cha miezi sita au zaidi. Sasa kwa kitendo hicho pengine yule mtu sio tabia yake kabisa.

Kwa mfano mtu kaja mwenzake akamtilia bangi mfukoni kwa sababu ya kumfanyishia tu, yeye hana habari kama mfukoni mwake katiliwa bangi, halafu akamwendea askari akamwambia bwana eeh yule ana bangi mfukoni. Basi askari wakakukamata na wakakukuta na bangi kweli, ukapelekwa mahakamani hatimae kesi ikathibiti kuwa umefanya kosa wewe la jinai kukutikana na bangi, kumbe si tabia yake na pengine tendo hili halijawahi kukutokea katika maisha yako hata siku moja, wala halitajirudia baada ya siku hiyo. Sasa mtu huyo umkoseshe haki zake pengine za kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Mjumbe wa Bodi ya Sensa. Kwa kweli nahisi hili si jambo zuri. Mimi nadhani tungerekebisha hii lugha kidogo. Tena si katika sheria hii tu ziko nyingi hizi sheria, tukasema basi mtu mwenye hii tabia mbaya ingekuwa bora zaidi kuliko kosa la jinai.

Kwa mfano, katika kosa hili la jinai unaweza ukasema huu udanganyifu, kutokuwa muaminifu na kuwa na tabia mbaya. Kwa sababu tabia mbaya inajulikana, unaweza ukamsoma mtu siku ya kwanza na siku ya pili, basi kumbe ndio maisha yake huko kuwa na tabia mbaya au ndio maisha yake kutokuwa muaminifu. Sasa akiwa na sifa kama hizi, basi kweli anaweza akawa hafai kuwa Mjumbe wa Bodi au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au mjumbe wa sehemu nyengine.

Mhe. Spika, kwa njia nyengine hili kosa la jinai mimi sikubaliani nalo, au vyenginevyo hili kosa la jinai lijirudie zaidi ya mara mbili katika maisha ya mtu. Hiyo sasa itakuwa ndio ile tabia yake mbaya ya kutokuwa muaminifu.

Mhe. Spika, siku moja kuna kijana mmoja aliiba baskeli, alipokwisha kuiba akaifungua vifaa alivyovitaka mwenyewe, lile fremu alilolibakisha akenda kumwekea mzee mmoja chini ya nyumba yake usiku. Sasa mwenye baskeli kahangaika kutafuta mpaka akalikuta pale nyuma lipo. Yule mzee maskini ya Mungu hata habari hana, wala haelekei hata siku moja kuwa mzee yule anaweza akaiba baskeli. Lakini yule kijana kuiona ile fremu yake iko pale akenda kumshtaki kuwa baskeli yangu nimeiona pahala fulani. Basi yule mzee akenda akakamatwa na ikawa balaa kubwa, wengi tulisikitika kwamba kwa kweli huyo aliyeiba baskeli hakumfanyia haki yule mzee. Sasa jambao kama hili halafu inatokezea bahati mbaya anafungwa, ndio unaweza ukasema mtu huyo anakosa sifa za haki zake za msingi kabisa.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana kuwa sheria zetu tunazozitunga, basi tutumie maneno mengine zaidi kuliko kosa la jinai.

Mhe. Spika, jambo jengine ni katika kifungu hicho hicho cha 7(2), naomba kunukuu.

Kifungu cha 7(2)

> "Mjumbe wa Bodi au Afisi Mtendaji anaweza kujiuzulu wadhifa wake kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mamlaka ya uteuzi na atasita kuwa mjumbe au Afisi Mtendaji pale tu litakapokubaliwa ombi lake".

Sasa hapa pana utata wa lugha kidogo, mtu mwenyewe kaamua kujiuzulu na kaandika barua yake ya kujiuzulu. Kama kilivyosema hiki kifungu hapa kwamba anaweza kujiuzulu wadhifa wake kwa kutoa taarifa. Sasa mamlaka inayohusika, maana yake kinasema hapa kuwa "atasita kuwa mjumbe mpaka pale mamlaka inayohusika hiyo ya uteuzi itakapokubali hilo ombi lake", lakini yeye hakutoa ombi, katoa taarifa. Kwa hivyo, hapa mimi nilitaka tupaangalie tena, ingekuwa kaomba kujiuzulu, basi sawa, atasita kuwa mjumbe pale ombi lake litakapokubaliwa. Lakini hakuomba, katoa taarifa na kama katoa taarifa maana yake kashajisaili mwenyewe kama mimi basi. Sasa aendelee kuwa mjumbe mpaka ombi lake likubaliwe si itakuwa ni kumsumbua mwenyewe na wakati keshaamua. Nafikiri ingewekwa lugha vizuri hapa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, sina mengi zaidi ila naomba nisisitize tu kwamba Mhe. Naibu Waziri Kiongozi katika kuyafanya haya madhumuni yake na nia yake hiyo njema ili ifike hatua ya kuridhisha, basi atumie wadhifa wake kuzishawishi na taasisi nyengine nazo zitekeleze wajibu wao kwa kulinda mila na utamaduni wa Wazanzibari. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Moh'd Ali Salim:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini zaidi namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia saa hizi tukawa tuko hapa tukawa katika hali ya uzima na tukiwa katika kazi nzito tuliyotwikwa na wananchi ya kuja kuzungumzia mambo muhimu kwa ajili ya nchi yetu.

Ninatoa shukurani hizi kwa sababu tulikuwa wengi, lakini mwenzetu mmoja katutoka na kwa masikitiko makubwa natoa mkono wa pole kwa wafiwa wote. Isipokuwa katika hili Mhe. Spika, nina wazo moja ambalo nadhani huwa hatumfanyii haki mwenzetu aliyetangulia kwa kusema tusimame tunyamaze kimya. Kwa mawazo yangu jambo ambalo lilikuwa linafaa, ilikuwa tusimame tumuombee dua, badala ya kusimama tukanyamaza kimya. Kwa sababu kimya

chetu hakimsaidii kitu, lakini tukiomba dua Mwenyezi Mungu huwenda akaikubali dua yetu na tukawa tumemsaidia marehemu.
Kwa maana hiyo namuomba *Allah* amsamehe makosa yake yote aliyoyafanya na amuweke mahali pema peponi. Pia namuomba *Allah* na sisi tuliobakia atusamehe makosa yetu na atuongoze katika njia anayoipenda yeye, ili na sisi tutakapoondoka twende tukakae huko kuzuri ambako ni kwa milele.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba sasa nianze kuzungumzia machache kuhusiana na mswada tulionao mbele yetu. Mhe. Spika, tunapozungumzia bodi ya sensa, tumekuwa na bodi ya sensa muda mrefu na ilikuwa na kazi nyingi tu za kuhakikisha kuwa utamaduni wetu haupotoshwi kwa njia yoyote ile. Kutokana na utendaji wa kazi wa bodi za sensa zilizopita, bado inaonekana kuna kasoro mbali mbali zilizokuwa zikijitokeza. Mengi tumechangia mimi nikiwa mmojawapo wa Kamati ile ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Wanawake, tulichangia katika kamati, lakini nimehisi nitakuwa bado sijawafanyia Wazanzibari haki kama kuna mambo sijayazungumza hapa Barazani.

Mhe. Spika, bodi imekuwa ikifanyakazi, lakini bado kumeonekana kasoro mbali mbali zinajitokeza, mmong'onyoko wa maadili bado unaendelea. Pengine kwa sababu hizo ikaonekana labda kulikuwa kuna matatizo ya sheria, kwa sababu kulikuwa kuna vyombo vingi vilivyokuwa vikiangalia huu mmong'onyoko wa maadili katika sehemu mbali mbali zinazohusiana na mambo ya utamaduni.

Mhe. Spika, sheria hii imekusudiwa kuondoa kasoro nyingi zilizokuwepo, ili mmong'onyoko wa maadili unaoendelea ama upunguzwe kasi au uweze kusitishwa kama itawezekana. Lakini upotoshwaji huu wa maadili kwa kweli unachangiwa na mambo mengi sana. Michezo ya kuigiza ni moja katika mambo ambayo yanapotosha maadili, nyimbo na ngoma ni miongoni mwa mambo yanayopotosha maadili.

Kwa mfano, ngoma zilivyokuwa zikichezwa na ngoma zile zile zinavyochezwa sasa, tena basi hazichezwi tu na watu hivi hivi, zinachezwa na vikundi vya kitaifa, basi zimebadilishwa.

Mhe. Spika, siku moja niliwahi kutoa mfano wa ngoma ya msewe. Ngoma ya msewe inachezwa na wanawake na wanaume. Lakini hapo zamani ngoma ya msewe wanawake walikuwa wakikamata vitambaa mkononi, ikicheza mikono tu na vitambaa, mwili wao ulikuwa umetulia. Kuna siku niliona kikundi cha taifa kikicheza msewe, wanawake hawakuwa tena wakicheza vile, mwili wao ulikuwa ukitikisika katika sehemu ambazo mtikisiko usingefaa mbele za watu.

Sasa haya yalikuwa yanafanywa na kikundi kilicho chini ya wizara, chini ya serikali.

Mhe. Spika, kwa mimi na wenzangu kama mimi tulikuwa tukiona kuwa serikali inapotosha maadili ya jamii ya Wazanzibari.

Sasa ni matumainio yangu kuwa kuanzishwa kwa sheria hii kutajaribu kwa kiasi kikubwa kuondoa kasoro za aina hii. Pia kuna matangazo katika vyombo vya habari, kuna matangazo yanayopachikwa katika mabango mbali mbali nayo yana matatizo. Pengine tutasema mengine labda ni lazima.

Mhe. Spika, leo asubuhi nilipokuwa nikisikiliza redio nimelisikia tangazo linasema "basi kama unampenda mpenzi wako usiwache kutumia kondomu kila siku". Sasa kwa sababu lile tangazo linatoka kwenye redio, hawasikilizi watu wanaohusika tu, wanahusika mpaka watoto wadogo, watoto wakubwa wakubwa kidogo, watu wazima na wazee wote wanalisikia tangazo lile. Hivi tunawafundisha nini.

Mhe. Spika, kuna mambo mengine lazima tuyatafutie pahala pakuyafundisha, kuna mambo mengine hayafai kutolewa tu hadharani kila mmoja akayapata, kwa sababu wengine hayajawahusu bado. Mambo kama haya kama kutakuwa na mpango wa kuyadhibiti, basi hii bodi ya sensa itakuwa ni chombo kinachofaa. Lakini ikiwa mambo kama hayo yatakuwa yanaachiliwa yatolewe tu kwa njia yoyote ile inayotakiwa, basi nadhani kwa mawazo yangu itakuwa mswada huu wote haujawa na maana inayostahiki.

Mhe. Spika, mimi napatwa na wasi wasi kidogo. Chombo kina nia nzuri, lakini je uwezo wake wa kufanya kazi utakuwa upo kweli, kama hivyo kilivyokusudiwa. Kwa nini nikasema hivyo, kuna mambo mbali mbali yanayochangia katika upotoshaji wa maadili ya jamii ya Wazanzibari.

Hivi sasa Mhe. Spika, akitokea mgeni ambaye Zanzibar na Wazanzibari na ghulka zao hazijui, akaingia hapa Zanzibar akaona wale wanaovaa suruali refu wanawake na *sing lend* bila ya mabuibui ndio Wazanzibari na ndio ghulka zao. Wale wanaojitanda wakavaa mikashda na mitandio ataona hawa ni wageni labda wametoka Arabuni wamekuja hapa. Sasa sijui tutawezaje kumfanya Mzanzibari akaonekana ndio Mzanzibari na yule aliyekuja tu na utamaduni wake kutoka alikotoka akaonekana kuwa huyu sio Mzanzibari. Kwa sababu hivi sasa hilo halipo, wale waliokuwa sio Wazanzibari ndio wanaonekana sasa hivi ni Wazanzibari na ile ndio ghulka ya Wazanzibari, na yale ndio mavazi yao na kila kitu chao.

Mhe. Spika, hili limenipa wasi wasi kuwa linaugumu mkubwa kwa hapa lilipofikia kurudisha hali ambayo akitokea mgeni akaujua kuwa huu ndio utamaduni wa Mzanzibari, haya Mzanzibari ndio mavazi yake, hizi Mzanzibari ndio ngoma zake na haya Mzanzibari ndio maisha yake kwa jumla. Hivi sasa kuna ugumu wa kulijua hilo.
Sasa kama bodi ya sensa itasaidia katika kulipata hilo, basi itakuwa ni jambo la busara sana sheria hii kupita na bodi hii ikafanya kazi. Lakini kama haitawezekana kufanya hivyo, basi itakuwa kupitisha sheria hii ni kutia maji pakachani. Kwa sababu ukitia maji pakachani ukayachukua, basi yote utayawacha pale pale ulipoyatia pakachani, na pakacha utaondoka nayo tupu labda imeroaroa tu kidogo.

Mhe. Spika, hilo ni jambo moja tu katika mambo yanayobadilisha ghulka na tabia za Wazanzibari. Jambo jengine sijui bodi hii itawezaje kuzidhibiti *internet café* katika upotoshaji wa maadili ya jamii ya Wazanzibari, zipo pale kila mtu ana uwezo na haki ya kwenda akaangalia anachokitaka na mle katika mambo yale mna upotoshaji mkubwa wa ghulka na tabia za Wazanzibari, mna mambo ambayo vijana wa umri fulani wasingepaswa kuyaona. Sasa suala hili sijui kama bodi ya sensa nayo itakuwa na njia ya kufanya sensa ya yale yanayotazamwa mle yakadhibitiwa angalau ikawa wale wanaokwenda kuangalia vijana waliokuwa hawajastahiki kuyaona mambo yale, nao wakafanywa pale wasiyaangalie watafute pahali pengine pakuangalia, lakini wasiangalie pale.

Pamoja na kuwa hiyo si dawa, kwa sababu sasa hivi watu wanaangalia nyumbani, ndani ya simu tu, mengi tu wanayaona. Sasa bodi ya sensa ina kazi, kwa sababu kwa njia hiyo haiwezi kuingilia kwa sababu si hadharani tena. Utakuta ni kikundi cha watu kinakaa wanaangalia mambo ambayo hayastahiki kuangaliwa, mambo ambayo yanapotosha tabia za nchi yetu. Je, bodi ya sensa itafanya nini katika haya. Kwa kweli ina kazi ngumu tena sana.

Mhe. Spika, ukiachilia mbali hayo, kuna haya pia ya kawaida ambayo ilivyo iwezekane kuyazuia. Kuna hizo kanda zinazokodishwa. Kwa ilivyoniingiza katika akili yangu, kwa maduka ya kanda niliyoyaona yaliopo, sijui bodi ya sensa itachukua muda gani, kuziangalia kanda moja baada ya moja zilizomo madukani, mpaka kanda zile zote wazimalize na wahakikishe kuwa nakala waliyoikubali wao ndio itakayooneshwa. Kwa sababu itabidi lazima wawe na alama maalum ya kuitia kanda ile, ambayo wao wameithibitisha kuwa inastahiki kutizamwa. Vinginevyo inaweza ikatizamwa kanda kwa kuwa hakuna ithibati maalum inayowekwa, baadae ikatumika kanda nyengine ambayo haikuthibitishwa, lakini kwa sababu ni mchezo ule ule zile sehemu ambazo zingepaswa zitolewe zikawa bado zinaendelea kuwepo.

Kwa hivyo hili mimi nalihisi ni gumu mno na linaweza likachukua miaka kulimaliza. Sasa sijui kutakuwa na utaratibu gani wa kuzipitia kanda zile mpaka zimalize zote na ziwe na ithibati ili zijulikane na mtu akiiona tu ajuwe kanda hii imepitishwa na bodi yaa sensa, na kanda hii haijapitishwa na bodi ya sensa. Hilo ni jambo jengine ambalo kwa mawazo yangu pengine lingekuwa ni gumu, lakini lina umuhimu mkubwa katika kutunza maadili ya nchi yetu. Sasa Mhe. Spika, baada ya kuyaona yote hayo kuna hii sheria ambayo sasa tunaijadili na baadae sheria hii ikipita ina maana tunatarajia kazi zake zitakuwa nzuri.

Mhe. Spika, nije kidogo katika suala moja ambalo tulilijadili, lakini sikuridhika na hatima ya mjadala wetu. Katika miswada mingi tumekuwa tukizungumza suala la mwenyekiti kuwa na sifa. Katika mswada huu kwenye kamati ilionekana kuwa Rais ni mtu mwenye busara  na vyombo vingi vya kumshauri, kwa hivyo anaweza kuweka Mwenyekiti ambaye anafaa.

Lakini bado kwa mawazo yangu binafsi Rais ni binadam. Marais wanabadilika kutoka siku hadi siku na wala si Marais wote ni wenye akili za aina moja. Kwa hivyo, kila Rais ana mawazo yake pamoja na uwezo wake wa kupokea ushauri anaopewa.

Sasa ukimuachia huru Rais achague mtu anayemtaka anaweza kuyapinga ushauri aliopewa asiufuate na akafuata akili yake vile anavyotaka kufanya. Kwa maana hiyo, kama hatukumuekea muongozo hata kidogo bado tunaweza kupata mwenyekiti wa bodi hii ambaye hastahiki kuwa mwenyekiti.

Mhe. Spika, nadhani kuna haja ya kuweka angalau sifa za chini kabisa za mtu ambaye angefaa kuwa mwenyekiti na wala tusiweke sifa za juu, ili tumpe nafasi Rais ya kuchagua miongoni mwa wenye sifa zile na zaidi kupindukia. Lakini tusimpe nafasi Rais kuchagua mtu asiye na sifa au chini zile.

Suala hili tumekuwa tukilijadili sana katika Baraza hili na katika miswada mbali mbali inayoletwa hapa na huwa tunarekebisha. Kwa hivyo, ninapendelea katika mswada huu, suala la sifa ya mtu anayefaa kuwa mwenyekiti ninafikiri kuna haja iwepo na wala Rais hatujampunguzia madaraka yake kwa kumuekea sifa ya chini. Tungempunguzia madaraka yake tukimuekea sifa ya juu, isipokuwa tunasaidiana naye tu kumuelekeza kama Wajumbe wa Baraza.

Mhe. Spika, mswada huu ni muhimu ambao ni uti wa mgongo wa utamaduni wa Mzanzibari. Tunapozungumzia utamaduni kwa miaka ya nyuma tumezoea kwamba utamaduni ni ngoma za asili “Utamaduni ni ngoma za asili kwetu ni dawa” *(Kicheko/Makofi).*

Tunapozungumzia utamaduni sio ngoma za asili kama walivyoimba wasanii. Tafsiri halisi ya utamaduni ni maisha ya wananchi wa nchi fulani au maisha ya watu wa kijiji fulani ndio utamaduni wao, yaani maisha yanajumuisha mambo mengi sana.

Mhe. Spika, napenda kutoa mfano mdogo tu ambao mtu yeyote asingefikiria kuwa ni suala la utamaduni. Watu wawili waende kufanya haja chooni wenye tamaduni tofauti, basi mmoja atajipangusa ndio utamaduni wake na mwengine atatumia maji ndio utamaduni wake. Kwa hiyo, mambo kama hayo watu hawafikirii kuwa ni utamaduni na kila mmoja anao utamaduni wake katika hilo *(Kicheko/Makofi)*.

Kwa maana hiyo, utamaduni ni suala zima la maisha na ndio maana nilipoanza kuzungumza nilizungumzia suala zima la mavazi. Kwa sababu mavazi pia ni utamaduni wa nchi, ikiwa wenye mavazi yaliyokuwa si ya nchi ile ni wengi zaidi kuliko wale wanaovaa mavazi ya nchi ile, tunaambiwa kwamba utamaduni umebadilika.

Sasa kuna mambo yanaweza kubadilika na wala yasiathiri sana utamaduni. Lakini kuna mambo yakibadilika yanaathiri utamaduni kwa sababu akiingia mgeni wakati wowote hajui utamaduni wa pale ni upi.

Mhe. Spika, ninamuomba Mhe. Waziri kwa sababu yeye ndiye msimamizi mkuu wa Bodi hii ya Sensa, kwa hiyo bodi yake ihakikishe kuwa tunarudi katika utamaduni wa Mzanzibari na mtu yeyote atakayeingia Zanzibar basi ajue huu ndio utamaduni wa Mzanzibari.

Watu wengi wanafikiria kuwa hawa wageni wanaokuja watalii, ni watu ambao hawarekebishiki, hawaambiliki na wala hawasikii. Suala hili si kweli, kwa sababu watalii wanafuata mnavyotaka wenyewe. Kwa mfano, watalii wakiambiwa watalii wanawake wakiteremka hapa wavae nguo mpaka chini vizuri tu bila ya matatizo yoyote, lakini wakiachiwa huru wavae wanavyotaka wenyewe basi watatembea hivyo na kila kitu utakiona.

Kwa hiyo, hili pamoja na kuwa si la Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, lakini Sensa Bodi inaweza kutoa ushauri kwa wizara zinazohusika kuhusiana na hili, ili utamaduni wetu tuweze kuuhifadhi vizuri.

Mhe. Spika, mswada utakapokuwa sheria itakuwa ni muhimu lakini itategemea utendaji wake wa kazi pamoja na kuwezeshwa kufanyakazi. Kwa sababu kuna vyombo vingi muhimu, lakini uwezeshwaji wa kufanyakazi zake ni mdogo na matokeo yake vinashindwa kufanyakazi inavyostahiki.

Ninadhani nitoe mfano mdogo tu ambao nao pia ni sehemu ya utamaduni. Lugha ni sehemu ya utamaduni wa nchi, yaani Baraza la Kiswahili ni sehemu ya utamaduni wa nchi. Lakini kutokana na kutokuwezeshwa unapita mwaka mzima hakuna kikao hata kimoja cha Baraza kinachofanywa na matokeo yake utaambiwa inashughulikiwa kamusi.

Wakati sheria inasema Baraza likutane mara nne kwa mwaka na iliwekwa hali ile makusudi kwamba kukutana mara nne kwa mwaka kuna kazi zake zinazotakiwa kufanywa. Kwa hivyo, kushughulikia kamusi na kuacha vikao vile vya kupeana mawazo pamoja na kupanga huwa hakujafanywa kitu.

Sasa na bodi hii ya Sensa lazima iwezeshwe na iweze kufanyakazi zake kama inavyostahiki, ili ifikie pahala turudi japo kidogo kule tunakotokea, pamoja na kuwa haiwezekani kurudi kwa asilimia mia kwa mia, lakini angalau kwa sehemu kubwa tuweze kuulinda utamaduni pamoja na maadili ya jamii yetu. Kwa sababu leo tumefikia pahala pabaya na pagumu. Kwa maana hiyo kuna haja ya kuangalia tunakwenda wapi.

Mhe. Spika, baada ya hayo ninakushukuru sana ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Spika, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sisi kukutana leo hapa. Pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kutoa mawazo yangu kwenye mswada huu wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Sensa ya Filamu na Maonesho pamoja na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kwa muda mrefu kama alivyozungumza Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwamba tulikuwa na hamu ya kuundwa kwa bodi, ili kusawazisha mambo ambayo yanahusiana na filamu na maonesho pamoja na mambo mengine.

Mhe. Spika, tusijeitegemea bodi peke yake kwamba inaweza kulinda mila na silka. Kwanza tujue kuwa Zanzibar ni nchi kama nchi nyengine imo katika utandawazi na hao vijana wetu ndio wenye kuona zaidi yale ambayo sisi tunasema yaundiwe bodi ya yalindwe.

Kwa sababu siku moja nilimuona mtoto mdogo anayo simu, lakini kile nilichokiona kwenye simu ninafikiri baba yake hajakiona. Kwa hivyo, tunayo kazi kubwa sana ya kulinda silka. Kwa maana hiyo, vijana wetu wamekuwa wataalamu wa kucheza na mambo ya teknolojia kuliko watu wote. Kutokana na hali hiyo ninashindwa kutafsiri.

Mhe. Spika, tuangalie kwenye madhumuni na sababu mswada huu unasema "Mswada huu unakusudia kuweka Sheria ya kuanzisha Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho Zanzibar. Mswada wa sheria unaopendekezwa unakusudia kulinda na kuhifadhi mila, silka, utamaduni na maadili ya Mzanzibari na kwamba sanaa haitumiki kupotosha maadili hayo".

Mila zinaweza kulindika. Kwa sababu kama alivyozungumza Mhe. Mohammed Ali Salim (Al-hajj) leo kidogo kama si sauti yake basi nisinge mjua maana tumemzoea kumuona kuwa na ndevu na leo hana. *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, mila zinalindika kwa mfano lakini si mfano mzuri. Watoto wa kiume wa Zanzibar wote hutahiriwa, lakini wengine hawafanyiwi na hii ni mila tena inalindika. Lakini mila ya kivazi Zanzibar haiwezi kulindika tena maana Zanzibar ni sehemu ya dunia.

Kwa maana hiyo, zaidi ya kuundwa bodi ya sensa, ninafikiri ziko baadhi ya sheria zirekebishwe, ili kuweka vile viwango vya adhabu ambavyo vinaweza kumtetea Mzanzibari akubali kulinda lakini sio kwa hiari.

Katika maeneo tulio sisi ya utalii hawa ndugu zetu wamezidi zaidi kuliko hao wageni, angalau wale wageni wanalala kwenye ufukwe ukitaka unakwenda kuangalia na usipotaka basi. Lakini wale ndugu zetu wanaokwenda kufanyakazi kule haisemeki, maana mishono ya nguo sio.

Kutokana na hali hiyo, kuna kazi kubwa sana ya kuyalinda baadhi ya mambo kwa hapa Zanzibar. Kwa nini yatakuwa magumu, kwa sababu zamani mila zinalindwa na watu wote katika jamii. Lakini leo mtu akimtoa kasoro mtoto wa mwenziwe jinsi alivyovaa, habari itafika kwao kwa sababu siku hizi kila mtu analea mwanawe na kila mtu analea mtoto wake kwa anavyomtazamia.

Kwa mfano, akimuona mtoto wake amevaa kwa kumsaidia uchumi, wewe ukimkosoa hakosoleki. Kwa sababu kila mtu analinda mtoto wake kwa jinsi anavyompatia mahitaji yake. Kwa hivyo, tusijeisingizia bodi kwamba hailindi silka pamoja na mila kumbe vile sisi wenyewe hatujawa tayari.

Mhe. Spika, watu wa zamani mila walikuwa wakilinda kwa pamoja na wala halindi mtu mmoja pekeyake na siku hizi haipo hali hiyo. Kwa mfano, zamani mtoto akimuona mjomba wake anampokea mkoba pamoja na kumsalimia vizuri na wakati wa leo hawezi kumsaidia chochote zaidi ya kumsalimia kwa salamu ya kileo "habari gani?"

Sasa mila hii inatoka wapi, kwa sababu haitoki Bara, labda Wazungu wanayo kwa sababu tunasikia Mzungu akikuuliza *How do you do*? Wewe uitikie *How*

*do you do thank you*. Lakini kwa kiswahili tuna taratibu zetu maalum za kuona kwamba tunailinda ile mila kwa kumuenzi yule mtu, sasa hakuna kumuenzi mtu na tutalinda vipi haya mambo mengine.

Ninadhani kinachoweza kulinda ni Bodi ya Sensa ni Filamu na Sanaa za Maonesho. Kwa sababu filamu ni kitu cha kutengenezwa na sio cha maumbile, sasa kama kitu cha kutengenezwa bodi inayo nafasi ya kuona kitu hiki kwa kilivyotengenezwa kiko sawa au kina kasoro.

Hata hivyo, katika dunia hii ya sasa kuilinda filamu kuna kazi kubwa sana. Kwanza ni sehemu ya biashara, pili ni sehemu ya maendeleo yenyewe na tatu ni sehemu ambayo sisi wenyewe tumetaka iwepo. Kwa mfano, kivutio cha utalii zaidi ni filamu na michezo.

Mhe. Spika, nani hajui kule tunakokwenda kulazwa kule hoteli ya Kempinski wale wanaopiga ngoma na kucheza vile sio tunavyotaka. Kwa sababu tuliwahi kwenda kulala kule Mapenzi Beach, yaani zile aina ya ngoma zinavyopigwa kwa wale washabiki wanaokwenda kuangalia kweli ndio tunao uwezo wa kuzilinda mila.

Kwa hivyo, lazima tuone mambo gani tunaweza kusema tutashirikiana na bodi katika kulinda, kwa kweli yako mambo mengine ni vizuri tukashirikiana na bodi katika kulinda na kuwa pamoja na katika kufanyakazi, ili kupunguza matatizo hayo.

Katika mambo ambayo yaliyotajwa kwenye mswada huu ni kuhusu michezo. Kwa sababu michezo nayo ni sehemu ya mila na hii bodi ilikusudia kufanya sensa katika masuala hasa ya michezo na mambo mengine. Lakini iko michezo mingine kama hujaicheza vile ilivyo basi haufikiriwi kama ni mchezo.

Kwa mfano, michezo mingine ambayo inaigwa kutoka nje ya Zanzibar, lazima iigwe vile ilivyo na kama haitoigizwa vile ilivyo basi hautambulikani kwamba mchezo ule ni kivutio.

Lakini hata hizi kazi za vinyago, siku moja tulikwenda Tanzania Bara na kamati yetu, tulipelekwa sehemu moja tulioneshwa vinyago na tuliviona jinsi vilivyotengenezwa, mwanamme huwezi kukitizama kinyago cha mwanamke na mwanamke hawezi kukitizama kinyago cha mwanamme.

Isipokuwa lazima niwasifu ni hodari wa kutengeneza na vile ndivyo anavyotangazwa Mwafrika hadharani, maana yake wanaonunua zaidi Wazungu sio sisi. Kwa sababu kwanza tuliona pale mbele kuna ngarawa na tulipewa maelezo ninafikiri ilikuwa ni Arusha.

Mhe. Spika, tulipoingia mle ndani kuangalia vile vinyago vilivyotengenezwa vina hatawa na vinatisha  sana. Kwa hivyo, pale vinatafsiri hii ndio asili ya Mwafrika alivyo. Pamoja na hayo ile *organ* ya mwaname ilivyotengenezwa ya zamani na sasa pamoja na zile tofauti zake inafurahisha, lakini mambo mengine huwezi kuangalia.

Sasa vitu vile haviuzwi Tanzania Bara tu na hata katika maeneo ya utalii Zanzibar lazima tuingize ndio tunafanya biashara.

Mhe. Waziri ninakuomba utakapokuja kufanya majumuisho unifahamishe, maana yake tulisema hadhari ni kuanzia watu watatu na hata wanane au kumi, lakini kama wanaongia zaidi ya watu kumi bado ni hadharani au sio hadharani.

Mhe. Spika, katika mswada huu utakapokuwa sheria na tunajua kwamba sheria ni msumeno unakwenda mbele na nyuma. Kwa hivyo, itakapotokezea mtu kwa utashi wake kama alivyosema Mhe. Abdalla Juma Abdalla akasema kwamba kinyago kile kimeoneshwa hadharani, yaani zaidi ya watu kumi au kumi na tano wanapita pale na kuona.

Je, kuna utaratibu mwengine wa kushtakiwa yule aliyeonesha ama kutakuwa na sheria ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji inamlinda, kwa sababu yeye ameweka kwenye utalii na wala hakuweka chumbani na ameweka sehemu ambayo kila mtu anaona, utatumika utaratibu gani.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ninalotaka kuzungumza ni kuhusu michezo ya sarakasi. Michezo hii inaoneshwa kwa njia tofauti na mingine inapendeza na inapokuwa inapendeza huoneshwa zaidi hadharani kuliko maeneo mengine. Sasa kama mchezo haukuwa na maadili ya Kizanzibari, lakini ni sehemu ya maonesho hivyo mpaka wafuate taratibu za bodi au italazimika aoneshe kutokana na hali halisi ilivyo.

Kwa mfano, Bodi ya Sensa iko mjini maana yake wajumbe wake wanaweza kutoka sehemu zote, lakini mara nyingi makao makuu yake bodi zote zinakutana mjini. Bodi iko mjini na yule anayetaka kuonesha amepeleka maombi yake kwa bodi na muda wa kukaa bodi kwa ajili ya kujadili bado haujafika.

Je, taratibu gani zitatumika au bodi itakasimu madaraka au itasubiri muda ufike ndipo mwombaji apate idhini ya kuonesha mchezo ule.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ninalotaka kulichangia katika mswada huu ni kuhusu sehemu ya ufafanuzi. Kwa kiasi fulani nilifahamu kwamba Katibu Mtendaji atakuwa ndiye mtu mwenye dhamana katika kushughulikia vikao,

lakini kama yeye hayupo au msaidizi wake ama anaweza kutokea afisa mwengine yeyote kushughulikia, ili bodi ifanye kazi zake vizuri.

Mhe. Spika, baada ya hayo sina mengi kwa sababu nilikuwa mjumbe na niliona nizungumzie baadhi ya maeneo ambayo wananchi wangu wanaweza kufahamu. Kwani maneno mengine ya kiswahili lakini ya kiingereza kwa mfano, tukisema sensa mimi nitafahamu kwamba ni hesabu na masuala mengine, lakini kwa mtu wa kawaida hafahamu.

Hivyo Mhe. Waziri hatuwezi kutumia neno jengine badala ya sensa au filamu, maana kule kwetu hakuna hata sinema, kwa hiyo hili neno filamu hatuwezi kusema neno picha.

Vile vile kuna matangazo mengi ambayo yanakwenda kinyume sana na silka. Hivyo, kuna utaratibu gani wakuona kwamba kuna chombo maalum cha kusimamia matangazo na hasa matangazo ya biashara, lakini kuna matangazo mbali mbali yanayokiuka maadili katika nchi.

Je, kuna utaratibu wowote na lazima haya nayo yawe yanapitiwa na Bodi ya Sensa au vipi, kwa sababu humo njiani utacheka kwani hayendi sambamba na silka wala utamaduni. Kutokana na hali hiyo, inaonekana matangazo haya hayana utaratibu wa wizara yoyote, kwani kuna wizara nyingi ambazo zinaingiliana katika kuweka matangazo.

Mhe. Spika, ninamshukuru Mhe. Waziri hivi sasa katika matangazo ya Bodi ya Sensa na mambo mengine umejaribu kuyatoa kule yanakoleta utata, kwa sababu sheria nyengine zimechanganya mambo mengi kwa pamoja. Lakini mswada huu tunaoujadili umeyataja mambo ambayo yatayafanyia kazi, ili kukupa nguvu yawe hayana urasimu mkubwa na wala tafsiri ya watu wengi.

Suala la mwisho mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe mswada huu tunaukubali kwa yale madhumuni yake mazuri uliyoyakusudia hasa yale ya filamu lazima zipitie kwenye bodi, ili kuondoa makuruhu katika jamii.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana, ahsante.

*(Saa 7:00 mchana kikao kiliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya mwanzo jioni hii ya leo, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia hali ya uzima na afya kwa kubaki hapa na kuzungumza.

Mhe. Spika, kwanza wajumbe wengi akiwemo Waziri Kivuli wamezungumza umuhimu wa huu wa mswada na hali ya kutengeneza mila na desturi za Zanzibar, umuhimu wa kuingilia kati wakati wote unapatikana katika kila maeneo serikali inapoona kwamba kuna mambo ambayo hayaridhishi katika maeneo yale. Kwa hivyo huu mswada wa kuanzishwa bodi hii, isiwe ni *formality* tu ya kwamba tumeanzisha bodi, lakini ionekane ni hali ya kuingilia ili kuinusuru hali mbaya ambayo inaendelea kujitokeza.

Mhe. Spika, katika hali kama hii ambayo tunaizungumza ya mmong'onyoko wa maadili katika jamii, basi vile vichochezi vinavyoleta mmong'onyoko huu, havina budi kutizamwa na kushughulikiwa, mojawapo ikiwa ni hizi CD, Cassette au filamu na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo.

Kwa ruhusa yako, naomba nitoe mfano mmoja ambao nchi moja tajiri kidogo hivi, iliajiri watu wengi kutoka Bangladesh kwa kazi mbali mbali za maendeleo ya nchi ile. Sasa baada ya kukaa kwa muda mrefu kwao, hakukupatikana mvua na kiongozi akatangaza kutaka sala ya kumuomba Mwenyezi Mungu ili inyeshe mvua. Sasa baada ya kusaliwa sala ile, siku ya tatu ilitangaziwa kunyesha mvua kubwa, lakini sio pale Bangladesh. Sasa watu wakafanya utafiti, mvua inaombwa huku vipi itanyesha Bangladesh, kumbe waliokwenda mle msikitini na kuswali wengi wao walikuwa ni wale wa Bangladesh wale wenyewe nchi walikaa majumbani hawakwenda. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu akaitikia wito wa wale walioomba na akanyesha mvua kule kwao.

Kwa hivyo nahofia sana, kwamba tukiwa hatukulitizama suala hili kwa upana na uzito unaostahiki kunaweza kutufika kama yaliyowafika wale, ikawa watu wengine ndio wanaonufaika, na sisi hatunufaiki na suala lile.

Mhe. Spika, sasa nianze mswada huu kwa kuungana na mjumbe mmoja pale aliposema kwamba, hii kuitwa bodi ya sensa hakuna kiswahili chengine, au kwa sababu ya tafsiri tu ya kutoka lugha moja kwenda nyengine ya sensa bodi. Nasema hivi kwa sababu hili neno sensa hata katika vitabu vyengine havitaki

maandishi na linatumika kama hesabu za watu. Sasa nina wasi wasi kwamba neno moja tukalitumia kwa maana mbili tofauti linaweza kuwachanganya watu.

Lakini sababu ya pili ya kulitengeneza neno hili lisingelifaa kutumiwa. Binafsi ya maandishi yaliyomo katika Mswada wenyewe halikutumika hata pahali pamoja isipokuwa pale palipoandikwa tu bodi ya sensa. Mahali mwingi mmetumika kuhakiki, kufuatilia, sasa inaonyesha kuhakiki ni bora zaidi kwa sababu ndio neno lililotumika katika kuelezea kazi za bodi yenyewe.
Mhe. Spika, kama walivyosema wenzangu karatasi yenyewe ndio hiyo ya mwaka huu, kwa bahati nzuri nawashukuru sana waliotayarisha mswada huu kwa sababu ni mswada wa mwaka mpya wa 2009, lakini hali yenyewe ndio hii tunayoiona. Labda ni ukurasa wa 250 kama hivi, lakini ni sehemu ya pili baada ya utangulizi.

Kifungu cha 4 kinasema kazi za bodi zitakuwa kama hivi ifuatavyo:

a) Kuhakiki
b) Kuhakiki
c) Kuhakikisha
d) Kufanya uhakiki
e) Kufanya uhakiki
f) Kufanya uhakiki

Sasa naona hakuna sehemu iliyotumika kuonyesha kwamba wao wenyewe waandishi wa neno hili badala ya pale walipolitumia kule juu tu bodi ya sensa, hawapendelei tena kulitumia kusensa, kusensa. Kwa hivyo, inaonyesha kwamba halina uzito wa kiswahili kwa mantiki hii ya maana hii, namwomba Mhe. Spika, azingatie na hakuna njia nyengine ya kutumia neno jengine kwa bodi hii na kikawa kiswahili kizuri zaidi na chenye kufahamika na wengi, badala ya kutumia neno bodi ya sensa ikawa ni bodi ya kuhesabu watu.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 5 cha mswada huu bodi itaundwa na wajumbe wafuatao:-
Mimi nina maoni kama matatu katika vifungu hivi.

Kwanza suala la Mwenyekiti, haidhuru sisi tunatumia mwenyekiti labda tunamwita *Chairman*, lakini pamoja na yote hayo anahitaji kuwa na uwezo na uoni wa ile kazi ambayo amepewa, hususan katika mfumo huu wa sasa tuliokuwa nao, alioutaja mjumbe mmoja wa utandawazi na vigezo mbali mbali vya kuangalia. Nadhani ikiwa hatukuchagua watu mahiri tutabaki na mtizamo finyu wa ile kazi ya sensa, kwa sababu tutakuwa hatuna haja ya kupata watu hata wa kompyuta. Hili nimewahi kusikia kwenye vyombo vya habari vingi, kwamba sensa iko hata katika *internet* katika nchi nyingi, hususan watoto ndio wanaotumia vibaya na hufuatiliwa na hupatikana na kushtakiwa.

Kwa hivyo inahitaji kwamba, hiki chombo tusikione kwamba ni kidogo kidogo tu, lakini tukitazame katika hali ya ulimwengu wa kisasa na ule mpenyo waliopenya watu katika kuangalia na kutajwa mambo mbali mbali ambayo yanaharibu mila, ikiwemo kompyuta na *interne.* Tusiangalie katika mtizamo ule wa nyuma ambako *technology* ile ilikuwa haijafikiwa, lakini tuangalie katika mtizamo uliokuwa wa kisasa kabisa.

Kwa hivyo suala la mwenyekiti na huko mbele kuna afisa mtendaji na hata wale *member* wengine, basi wanahitaji kuwa na uelewa mkubwa zaidi kuliko tulivyokuwa kwenye miaka kumi au kumi na tano iliyopita.

Mhe. Spika, suala la pili katika vifungu hivi ni suala la idadi ya wajumbe, hapa inatajwa kwamba Mwenyekiti, Afisa Mtendaji na wajumbe wengine wasiozidi sita. Sasa kimantiki ya bodi au kamati katika suala la uongozi yaani *administration* inahitaji kupatikana kwa namba tasa yaani *old number,* kwa sababu Mwenyekiti anakuwa na hadhi ya kuamua iwapo watapiga kura na voti itakwenda sawa kwa hivyo Mwenyekiti anabaki na kura kuamua. Kwa hivyo idadi halisi ya kamati zote au bodi zote, inatakiwa iwe idadi tasa. Kwa hivyo hapa kwa sababu ya idadi iliyopendekezwa, ilikuwa iwe inasomeka wajumbe wengine wasiopungua watano na wasiozidi saba.

Kwa maana hiyo, ikiwa tunataka wajumbe wawe saba, basi watano wale na wawili hawa wanakuwa saba, tukitaka wawe tisa, lakini kwa mujibu wa hapa inatakiwa iwe wanane yaani wasiozidi sita pamoja na mbili itakuwa nane, hapa kamati itakuwa haikubaliki na siku zote itakuwa hakupatikani maamuzi, kama kura itakuwa haisadii kitu, lakini ikibidi *Chairman* anapiga kura ya maamuzi na kikao kinafikia maamuzi. Kwa hivyo, katika mfumo wa kamati inatakiwa idadi iwe hiyo. Kwa hivyo, tunaomba sana Mhe. Waziri alitazame sana suala hili na aone kwamba anaunda kitu ambacho kitafanya kazi kikweli kweli baadae.

Mhe. Spika, mimi sina mashaka na kazi za bodi hii, lakini kama nilivyosema mwanzo kwamba inahitaji kuangaliwa kwa upeo zaidi ambapo itaingiza kabisa kabisa bila ya kuficha mambo yote yanayohusiana na nyenzo za kisasa za *technology* za upenyo wa hila na utamaduni ulikuwa haufai, kwa sababu tutawapa fursa wajumbe wetu wa kuingia mpaka kwenye *internet.* Kuna watu wametajwa humu humu katika baraza, yaani ni nchi ambazo zinao uwezo wa kuchuja *internet* zinazoingia. Sasa inawezekana na sisi tukafikia hapo na kuweza kuchuja zile *internet* zinazoingia katika nchi kwa kupitia bodi hii na wakaweza kutoa manufaa makubwa, sasa hata kama mtu anakuwa anaitaka anapata matatizo makubwa.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ningependa kulizungumza ni mamlaka ya chombo chenyewe. Mara nyingi vyombo tunavyoviunda vinakuwa havina

mamlaka na kwa sababu hiyo, ama pengine ni kutokana na uchache wa ujuzi wa wale wajumbe wenyewe, lakini pia kutokana na nyenzo na fursa wanazopewa, zinawafanya wapungue mamlaka. Imetajwa hapa kwa mfano sehemu moja kama ilivyotajwa na sisi ndio tunaliendeleza. Kwamba mila na utamaduni ni vipengele vingi vikiwemo vya lugha, dasturi za watu namna wanavyojenga nyumba zao na namna wanavyokula vyakula vyao yote.

Sasa kama lugha kipo chombo chetu cha kiswahili, lakini hakipewi nyenzo. Je? utamaduni ule unafikiria kwamba utaweza kulindwa au kushughulikiwa ipasavyo.  Sasa na chombo hiki vile vile. Mimi naendelea kusema msemo wangu ule ule wa kawaida kuunda na kutengeneza ni sehemu moja, lakini kukifanya kikafanya kazi ni sehemu nyengine muhimu sana, tunaweza kuwa na vyombo vingi, lakini havifanyi kazi.

Leo hapa asubuhi palikuwa pakizungumza kuhusu usafi tuna Mabaraza ya Miji, tuna Halmashauri za Miji, tuna kila kitu kinachohitajika katika majina, lakini mji wa kilomita mia tutu unatushinda, tunapiga kelele. Kwa hivyo, tunasema tuwe makini, hiki chombo kimeshaanzishwa tuweze kukipa nyenzo zinazoweza kukiwezesha.

Mhe. Spika, nikiachana kidogo na hapa nakuja katika mifano ambayo mimi kidogo naihisi imo ndani ya Wizara. Bila ya hichi chombo, huu wakati tulikuwa nao wala sio muda mrefu tulikuwa na watu wa hapa hapa walikuwa wakishughulikia ile michezo ya kuigiza na ilikuwa watu wengi wanaipenda. Kwa sababu lugha zao ukizitizama unaweza kuzisema ndani ya nyumba, mambo yao ni ya kawaida yanayofanyika kila siku.  Mfano wa kundi hilo ninayemjua ni bwana Chimbeni na wenzake, lakini katika kipindi hiki hiki cha karibuni tumeshuhudia katika vyombo vya habari vya serikali kuna vikundi vyengine vinafanya ile michezo ya kuigiza, lakini lugha sio inayotumika. Nikiuliza wameipata wapi lugha ile ama wamekwenda kujifunza pahali sijui. Sisi huko nyuma tunakumbuka ilikuwa ni TVZ moja tu na watu wote walikuwa wakitizama  hakuna wakati uliofikia ikawa watu wanaondoka na kuwapisha wengine, familia wanatizama na wanafanya kila kitu mpaka TV inafungwa.

Lakini ghafla kumetokezea mabadiliko ukiingia mchezo wa kuigiza sasa ikiwa huna kidishi ulichokipachika huko,  basi uondoke au ufunge TV, maana yake haiwezekani kwamba mtu atatoka pale ni kijana mwanamme amfuate kijana mwanamke kwa lugha za mitaani ndani ya TVZ. Anasema poa tutaonana . Tena ni mchezo uliopitishwa katika TVZ kama nilivyomtaja yule mmoja nitataja na hili group la Makombora na wenzake kwa sababu nina ushahidi nimeshauona mimi mwenyewe binafsi. Sasa angalia, watu wa hapa hapa lakini wakiangalia michezo kwenye group hili inafanya watu majumbani wanafurahi

na wanacheka, wanatabasamu na furaha, lakini wengine lugha zao hazifahamiki.

Kwa hivyo, mimi naomba sana pamoja na hii bodi, lakini bado Wizara inalo jukumu la kutizama mambo ambayo yangeshughulikiwa na hiyo bodi. Mojawapo ni hii michezo ya kuigiza ambayo ina lugha zilizokuwa zina tofauti na mila na mafundisho ya watu. Mimi binafsi nilifikia maamuzi nikasema kutizama michezo ya kuigiza ya TVZ basi, bora utizame ngoma au muziki wa Kiarabu kwa sababu huyafahamu maneno yake, utasikia ule mziki tu basi. Lakini haya maneno ya Kiswahili unayoyafahamu linakuja neno wazi wazi pale ilitusikitisha sana.

Kwa hivyo Mhe. Spika, pamoja na maandalizi yetu ya kupata bodi, lakini tunayo nafasi ya kutizama kwa upana ni nini hasa hii bodi iweze kushughulikia. Ndio maana nikasema mamlaka ya bodi je?. Pengine watu wale wameshaigiza mchezo wao na wengine wameshaupitisha na inaonekana tabu kurudishwa. Kwa hivyo, je bodi itakuwa na mamlaka ya kurudisha michezo ambayo pengine wakubwa fulani au watu fulani ndio waliyoipeleka au kushughulikia katika kuipitisha.

Mswada huu pia una kasoro kidogo ya kutaja zile taasisi za watu binafsi namna gani zitakavyoshughulikiwa, kwa mfano maduka haya ya CD na Cassette, je yataingizwa katika ufuatiliaji wa bodi hii. Kwa sababu yale yanatolewa kwa *public na private*. Au itaachiwa mpaka yule atakayekwenda kuionyesha ile *public* ndie ambae atakwenda kushughulikiwa kwa sababu humu inatajwa watu watatu na zaidi ni watu waliokaa nje hadharani, lakini ndani ya chumba mpaka uwe na *warrant,* isipokuwa kwa kazi maalum, lakini kwa kazi ya kawaida uwe na *warrant* wa kwenda kutizama kwamba mna watu wangapi ndani watatu au zaidi.

Mhe. Spika, mimi sina mchango zaidi, isipokuwa nasema uundwaji wa vyombo hivi unategemea sana namna ya madhumuni tuliyoyakusudia. Kama tulikusudia madhumuni ya kutengeneza na kurekebisha, ni kuona kwamba tunaondokana na hali hii mbaya kwenda hali nzuri, au hali nzuri kidogo kwenda hali nzuri zaidi. Basi hiyo inaweza kutusaidia au tunapitisha vyombo hivi kwa sababu tuwe navyo. Mimi naona itakuwa hatuwasaidii wananchi wala hatuisaidii Zanzibar, hatusaidii maendeleo ya wananchi na wala hatusaidii maendeleo ya Zanzibar, kwa sababu ni nchi ambayo haina utamaduni, nchi ambayo haina lake la kusemea. Nchi ambayo haina cha kujivunia na kubaki katika hali ya kudumazwa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuweza kuchangia na kutoa mawazo yangu katika Mswada huu muhimu ambao upo mbele ya Baraza lako tukufu. Kabla ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na kutufikisha pamoja na mimi mwenyewe katika dakika hii nikiwa nimeweza kusimama kwa pumzi zangu na kuweza kuzungumza haya ambayo nitaendelea kuyazungumza.

Mimi katika mchango wangu nataka nianzie katika upande unaozungumzia madhumuni na sababu, nitapenda nianze kwa kunukuu.

"Mswada huu unakusudia kuweka sheria ya kuanzisha bodi ya sensa na filamu na sanaa za maonyesho Zanzibar, Mswada wa Sheria unaopendekezwa unakusudia kulinda na kuhifadhi mila, silka, utamaduni na maadili ya Mzanzibari na kwamba sanaa haitumiki kupotosha maadili haya".

Mhe. Spika, kabla sijaingia katika vifungu nilikuwa napenda nizungumze au nitoe maoni yangu ya jumla kuhusiana na suala zima la mila na silka za nchi yetu. Kama alivyozungumza Mhe. Waziri Kivuli asubuhi. Alisema inaonekana kwamba serikali imetanabahi, na mswada huu umekuja wakati muafaka kwa kuwa wameona maji yamezidi unga, utamaduni, silka na haiba ya nchi kiutamaduni inaonekana kuyoyomea. Hili sio suala la leo na jana wengine tulishasema zamani kama zitatazamwa Hansard mwaka 1999. Mimi nilizungumzia suala hili namna ya utamaduni utakavyoyoyoma kidogo kidogo na maadili yatakavyozidi kupotea na ndivyo ilivyotokea. Nitarudia kidogo maneno kama nilivyosema jana kwamba imekuwa ni ushahidi wa kinyamwezi, tumesubiri liwe au ni mwendo wa jongoo kasubiri mpaka agonge ndio akajua kwamba hakuna njia.

Mhe. Spika, kinachosaidia au kinachosababisha maadili ya nchi kuporomoka ndani ya nchi yoyote ile pamoja na sababu nyengine nyingi. Kwanza ni kutokana na wageni wanaoingia katika nchi hiyo bila ya utaratibu na ndiyo hali iliyozungumzwa asubuhi hapa. Kama unataka kumuona Mzanzibari halisi ni yupi, basi sasa hivi ni tabu na huenda wale Wazanzibari sasa hivi wakawa wanaonekana ndio wageni na wale ambao wamekuja kama wageni na sasa wana jina la ukaazi ndio wanaonekana kwamba ndio Mzanzibari alivyo.

Mhe. Spika, kwa kufuatilia hata matangazo mbali mbali ya Televisheni za Bara namna ya matangazo yao wanavyoyapeleka katika mambo ya utalii na mambo mengine kama mambo ya kale, utakuta kwamba wanajigeza zaidi na mambo ya mwambao kama kwamba wao ndio Wazanzibari haswa. Mhe. Spika mimi binafsi linanisikitisha. Masikitiko yangu sijui yatafikia wapi, kwa sababu wakati mwengine maoni yetu inakuwa kama tunatia maji pakachani kama alivyozungumza mwalimu wangu asubuhi. Ukitia maji pakachani utaondoka na

pakacha lako tupu, sana sana litakuwa limeroa tu. Hali hii ndio imetufikisha hapa. Hali sio nyepesi sana ya kuwa itawezekana kirahisi rahisi.

Mhe. Spika, mimi nataka nitofautiane na wale walionitangulia kusema kwamba hali imekuwa ni mbaya na haitawezekana kuirejesha ile hali ya kawaida kama ambavyo ilivyokuwa zamani au angalau ikafanana ukajulikana utamaduni wa Mzanzibari hasa ni upi. Labda ninukuu maneno ya Kiingereza wakati Raisi mpya wa dunia anatoa kampeni zake na mpaka siku ya kutoa shukurani alikuwa ana maneno anayasema "*Yes, we can*" Alikuwa anashajihisha kwamba hakuna lisilowezekana. Na mimi nilikuwa nawaomba wenzangu pamoja na kiti chako Mhe. Spika, kwamba tusikate tamaa, hakuna lisilowezekana katika ulimwengu huu. Ikiwa tumeweza kupeleka chombo angani na wakachukua vyombo wakavipeleka chini ya bahari na vyengine vinatembea katika mgongo wa ardhi basi yote yanawezekana, labda roho tu kuitengeneza, hiyo ndio mtihani.

Mhe. Spika, katika haya niliyoyasema kinachotakiwa zaidi ni kuzingatia na kutanguliza nia njema katika kuona namna gani tunaweza kuanza. Ilizungumzwa kwamba sasa hivi kutokana na utandawazi. Na huu utandawazi Mhe. Spika, sijui kwa nini ni sisi tu ndio tunaoupa nguvu kwamba haiwezekani kwa sababu kuna utandawazi. Si kweli Mhe. Spika. Utandawazi upo lakini na kudhibitiwa ni kukaa na kuona ni namna gani tunayakabili mambo.

Mhe. Spika, asubuhi imezungumzwa kwamba hivi sasa kila mtu nyumbani kwake ana CD yake au TV, DVD au VIDEO kwa hivyo hana haja ya sinema. Mhe. Spika, majengo ya sinema tumeyatupa sisi wenyewe tu na tumeyadharau tukayaona kwamba hayana maana. Lakini miji iliyoendelea kuliko sisi kwa mfano kama London au Uingereza na naamini pengine na mabara mengine ya Ulaya yapo hivyo. Sinema kitu muhimu mpaka leo hii na huko ndiyo yalipoanzia hayo mambo ya utandawazi mpaka yakafika huku kwetu. Lakini sisi sijui kwa nini tunakata tamaa au tunaona kwamba haiwezekani.

Mimi nadhani tujifunze kwamba wenzetu wanafanya vipi. Katika kujifunza tusitizame nyumba ya pili tu unaweza kwenda hata kiambo kinachofuata au mji mwengine. Ndio maana katika kujifunza tumeambiwa kwamba tuitafute elimu hata kama ni China, haina maana kwamba ni nchi ya China tu lakini ina maana kwamba uwende umbali zaidi na kwa wakati huo mbali zaidi ilikuwa ni China. Kwa hivyo na sisi sasa hivi tunaweza tukafika katika nchi yoyote katika dunia hii sio lazima tupande boti mpaka hapo tu tukishuka ndio tukawa tunajifunzia hapo, ingawa na hapo bado tunaweza kujifunza.

Mhe. Spika, katika haya nadhani hata uingiaji ni suala ambalo tunalirudia sana kulieleza kwa sababu ni mambo mtambuka linaingia kila mahala, nitaomba

univumilie pia nilichomeke kwa sababu panahusika. Wageni wanaoingia katika nchi yetu bila ya mpangilio na ikawa wanaingia tu lakini hawatoki kwa kiasi kikubwa sana wanatuharibia utamaduni wa nchi yetu, kwa sababu ya kuiga na mambo ya sauti za busara na mengineyo inakuwa zaidi tunapokea yale ya watu yanayokuja na tunaacha yetu.

Mhe. Spika, sikuwahi kukisoma kitabu kinachoitwa cha jando na unyago, lakini nafikiri kilikuwa kikieleza mambo mengi ya Kiswahili na utamaduni wake na utarajibu wake, sijui kwa nini kilipigiwa marufuku. Kwa namna nyengine labda kuna watu maalumu walikuwa hawatakiwi wakisome, lakini kuna umri ambao wangefahamishwa. Hata hichi kilio tulichokuwa nacho leo cha mambo sijui ya kupiga vita ukimwi nadhani hicho kitabu kilieleza mambo mengi kwa upande wa kina mama na kina baba, vijana, watoto na wazee. Siwezi kusemea zaidi lakini nilikuwa najiuliza kwa nini. Nadhani kulikuwa na mambo mengi ambayo silka zetu na mila zetu zilikuwa mule zimeelezwa. Kwa hili nakubali kukosolewa kama nitakuwa nimekosea katika haya maelezo yangu.

Mhe. Spika, kama ulivyo mswada huu sio mkubwa kwa hivyo huo ulikuwa ni utangulizi, sasa naomba nitoe maoni yangu machache katika huu Mswada wenyewe. Nikitanguliza sehemu ya kwanza kifungu cha pili katika tafsiri ya neno sanaa. Hapa yameelezwa maneno mengi lakini naona kama kitu kimoja kimeachwa na nitapenda ninukuu kabla sijaendelea na mchango wangu. Sanaa inajumuisha sanaa za maonyesho, uchezaji wa maigizo, ngoma, muziki na sarakasi. Sanaa zipo za ufundi, uchoraji, usukaji, ufinyanzi, uhunzi na ushoni, tenzi, ngonjera na majigambo. Sijui hapa Mhe. Spika, majigambo yamekusudiwa nini. Ukiendelea kuna upigaji chapa, picha tuli. Ningependa akija Mhe. Waziri hii picha tuli anifahamishe ndio kiswahili hicho au vipi.

Mhe. Spika, kwa sababu mioni mwa mambo ambayo yameporomoka sana katika maadili ya nchi yetu ya Zanzibari ni lugha yetu ya Kiswahili. Kama tunavyoona kwamba sasa tumetoka katika kuvaa mabaibui na nguo zilizokuwa zinaendana na maadili yetu na badala yake tunavaa jinzi za kubana na vishati vyenye kitovu nje, kiuno nje, machuchu yote yanaonekana, hapafunikwi vichwa tena, basi na Kiswahili kimeharibika katika hali kama hiyo.

Mhe. Spika, hapa kuna maneno yameshawahi kusemwa, sitaki niyarudie, maneno ya sasa yanasema kwamba habari ndiyo hiyo. Kiswahili kimevurugwa kama mfano wa bata anavyovuruga tope, nathubutu kusema hivyo. Kinachoniumiza zaidi kwamba sijui kwamba tunaridhika na hali hii, kwa sababu utakuta na sisi wenyewe tunayapa nguvu. Wageni wacha wayatumie lakini utakuta na sisi tunayatumia. Leo watu hata wakisalimiana mtu mzima unamwambia “mambo” badala ya kumsalimia kwa heshima katika maamkizi

tunayoyatumia. Badala yake kila siku tunapata kama sio maneno mawili au matatu mapya, yanaanzia upande wa pili halafu na huku utaona kwenye taarifa zetu za habari, zinarudia mambo ambayo kwa kweli ukitafuta tafsiri yake inakwenda kwa mbali mno.

Mhe. Spika, picha tuli mimi sijafahamu na kama nimefahamu maana yangu ni kwamba hichi sio kiswahili. Mtu yeyote Mzanzibari Mswahili ukimwambia picha anafahamu lakini ukiweka na tuli, nashindwa kupata ile mantiki ambayo imekusudiwa. Pengine naijua lakini ninachosema hapa ni kwamba Kiswahili hichi sicho, hatuwezi kusema picha tuli, ukisema picha tu inajulikana.

Nikiendelea katika paragrafu hiyo hiyo picha za Video, filamu, sinema, maonyesho ya maigizo, muziki, muziki wa ala, nyimbo, noti, kwanza nilifikiri za kutumia lakini baadaye nikafahamu kwamba ni zile *keyboard* za mambo ya muziki. Sasa na hii jazi sikuona tafsiri yake kama ilifanyiwa marekebisho kama walifahamiana huko katika Kamati au pengine tutachukua jazi kama ni *uniform*, taarabu na disco.

Mhe. Spika, jambo ambalo nahisi limepungua ni uimbaji. Katika hii paragraph nzima inayoelezea sanaa basi uimbaji ni neno ambalo linajitegemea. Haidhuru humu imeandikwa nyimbo, lakini nataka niifafanue kidogo. Nyimbo inaweza kuwepo lakini ikawa hapana mwimbaji, sasa na ule uimbaji nao ni sanaa. Kwa hivyo nilikuwa napendekeza kwamba hili neno uimbaji nalo liongezwe hapa. Kwa sababu unaweza ukanipa nyimbo Mhe. Spika, vikapigwa vinanda vikawa vinakwenda upande huu kwa sababu mwimbaji ni mimi ambaye sina uimbaji na vinanda vikawa vinakwenda huku.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu na mimi nitapita kidogo kwenye kifungu cha 4 ambacho takriban wachangiaji wote wamekizungumza. Mimi nataka nirudie kusema kwamba katika huu uhakiki unaofanywa basi na lugha nazo pia zitizamwe. Nadhani hapa iwe ni kazi ya bodi pamoja na mambo yote hayo wanayoyafanya basi na lugha nayo itizamwe kwa maana ya kwamba iwe imekaa vile ambavyo inatakikana na isiwe ni Kiswahili cha kisasa. Maana hii kusema kwamba lugha zinakuwa (Kiswahili kinatanuka) ndio matokeo yake mpaka mwisho inabadilika kabisa.

Mhe. Spika, hili liangaliwe vizuri ili kama ni kuenzi utamaduni basi vizazi vyetu vijavyo wajue kwamba Kiswahili hasa ndio kipi, maneno hasa ya Kiswahili ni yepi badala ya kuja wakakuta mambo ya uboreshaji au kuhabarisha. Nina wasi wasi yasije maneno haya yakaingia kwenye vyombo vyetu vya habari vya hapa, yabakie huko huko kwao. Kwa sababu kule silaumu wanapokuwa na maneno kama haya, kwa sababu wao kwao kiswahili ni lugha ya pili na wengine kama sio ya tatu, wanatangulia na lugha zao za kienyeji

wenyewe huko halafu tena ndio kinakuja Kiswahili, lakini sisi tukitoka tu basi ukianza kusema maneno ya mwanzo unakuja zako na Kiswahili mpaka mwisho, lugha nyengine zinakuja baadaye kwa sababu unakuwa unasoma lakini ile ni *original* ukizaliwa tu umezaliwa nayo.

Mhe. Spika, halafu katika suala zima la kazi za bodi pakoja na mambo ya kutoa vibali na mambo mengine mimi nilikuwa naomba sana. Kuna hawa wenzetu wanaopita na mabolingo kwa gari. Sijui bodi ndio inayowapa kibali kile cha kupita na magoma na kucheza katika hali alizozieleza Mhe. Moh’d Ali Salim (Mulla) asubuhi. Ninachoomba mimi kwamba wapangiwe na wakati wa kupita na yale magoma yao barabarani. Wanaweza kupita wakati wowote lakini wakati wa sala Mhe. Spika, mara nyingi huwa ndio zinapamba moto, huku adhana inaadhiniwa na huku ngoma ndio zinapita. Viko vipindi nawapite wapige ngoma nyingi, lakini kuna vipindi *at list* watupe nafasi kwa mujibu wa silka na utamaduni wetu, tunaposikia adhana tunakwenda kutekeleza ibada zetu. Wakati mwengine kinapita kishindo, pataadhiniwa, patasaliwa watu hawana habari. Na kwa sababu ya mambo yanayopita kwenye hilo gari wengine wanajikuta hata kwenda kusali hawajenda kwa sababu walikuwa wakishughulishwa pale.

Mhe. Spika, hili naliomba sana katika utaratibu mzima wa hizi kazi za bodi waone kwamba wanawapa vibali hawa wanaotoa matangazo hususani wale wanaopita na magari basi kuna wakati iwe ni makosa na waingie katika hichi kifungu cha adhabu na kifungo watajua wenyewe wanavyohukumu huko lakini katika kipindi kama hicho na katika miji kama hii yetu basi matangazo hayo yasitishwe basi angalau katika kipindi hicho wapangiwe hasa iwe hakuna masuala kama hayo.

Mhe. Spika, kuhusu kifungu namba tano na mimi naungana mkono na wenzangu kuhusiana na uwezo wa huyu Mwenyekiti awe ni mtu mwenye uwelewa wa kutosha. Inawezekana pengine kaja pale na digrii zake lakini akawa haelewi utaratibu kwamba kuna silka na mila. Kwa sababu haikusemwa hapa kwamba mwenyekiti hapa atakuwa nani na haikuwekwa mipaka. Bahati nzuri sasa hivi tupo wengi. Kuna Miswada mengine inaweka wazi kwamba awe ni Mzanzibari mwenyewe. Lakini hapa kwa sababu haikusemwa sijui atawekwa nani. Sasa pengine anaweza akaja mtu awe ana mila tofauti akatuletea vurugu mechi. Nilikuwa napenda na sifa hii nayo izingatiwe kwamba huyu Mwenyekiti na Afisa wake mtendaji na ikiwezekana na wajumbe wote basi wawe ni Wazanzibari kwa maana ya kwamba tuwe makini katika kuona tunadhibiti ule mmong’onyoko wa maadili ambao sasa hivi ni kilio chetu.

Mhe. Spika, sasa nataka niingie katika sehemu ya nne ya Mswada huu kifungu cha 19. Hapa nilikuwa nasisitiza kuhusiana na matangazo yanayoelezwa hapa. Maonyesho ya kutumia matangazo kwenye magari. Hapa naomba nisisitize tu kwani nimeshalizungumza kwenye kifungu cha 4.

Mhe. Spika, mchango wangu utakuwa sio mrefu sana, zaidi nilikuwa nasisitiza kwamba kadiri ya michango ambayo imetoka na tunaendelea kutoa michango tusione kwamba tutashindwa pahali popote. Tuone kwamba inawezekana na tujiandae hivyo kuona namna gani tunaweza na njia zipi tutakuwa tunazitumia ili kuona kwamba tunaliokoa jahazi hili na kuiokoa mila na silka ya utamaduni wa nchi yetu katika nyanja zote, zikiwemo vile vikundi vya ngoma za utamaduni za kitaifa kama zilivyozungumzwa asubuhi.

Mhe. Spika, kwa kweli inasikitisha kuona kwamba tunayaona mambo yanaharibika lakini unapiga makofi. Ngoma nyingi za visiwa hivi huwa hazichezwi katika hali ya mwili kuwa na taharika na kuweza kuwashughulisha watu wengine. Kwa hivyo tulikuwa tunaomba sana hii bodi kupitia wizara yake ianze kufanya marekebisho ya zile ngoma zetu na vikundi vyetu vya ngoma vya kitaifa ili tuweze kuwaelimisha na wengine. Shekhe mzuri ni yule anayeyahubiri ndiyo anayoyatenda, isiwe fuateni maneno yangu msifuate vitendo vyangu.

Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia machache sana katika Mswada huu ambao kwa bahati nzuri mimi nimepata fursa ya kutoa maoni yangu ya kutosha katika kamati. Lakini hata hivyo sina budi kuchangia machache kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kabla sijachangia Mswada huu nije katika jambo moja ambalo kwa leo tulipaswa iwe kama wimbo lakini bahati mbaya sijamsikia hata mwenzangu mmoja kuuimba wimbo huu nao ni kumpongeza Barak Obama.

Mhe. Spika, sisi tukiwa kama ni Waafrika hatuna budi kumpongeza Barak Hussein Obama kwa kuwa Mmarekani wa kwanza mweusi kuongoza taifa kubwa duniani la Marekani, kinyume na utabiri wa Robert Mugabe. Robert Mugabe alisema kwamba haiwezekani hata siku moja kijana yule mwenye asili ya Kiafrika kupewa nafasi ile na Wamarekani, aliwafikiria Wamarekani wabaguzi kama yeye. Lakini bahati nzuri Wamarekani wakamjibu Mugabe na wakamwambia sisi huyu uliyesema kwamba hatuwezi kumchagua tumemchagua. Kwa hivyo nasema ni furaha kwa Waafrika walio wengi lakini itakuwa ni karaha kwa Mugabe ambaye hakupenda kijana yule achaguliwe kwa sababu ambazo anazijua yeye mwenyewe.

Mhe. Spika, sasa nije katika Mswada wenyewe. Kama nilivyotangulia kusema kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii na nimepata fursa ya kutosha kuchangia Mswada huu katika Kamati na marekebisho mengi tumefanya pamoja na Waziri mwenyewe katupa mashirikiano mazuri. Lakini sasa nieleze yale ambayo nimehamasika kutokana na michango ya wenzangu naomba niyaseme.

Mhe. Spika, wenzangu wengi waliochangia wamekuwa wanazungumzia hili suala la ujumla la kulinda utamaduni. Kulikuwa na mawazo ya aina mbili kuna wachangiaji wengine wamejenga matumaini na huu Mswada kwamba utaondoa tatizo lililokuwepo la ukiukwaji wa maadili. Kundi jengine limeonesha wasi wasi kwamba kweli hili suala litaondoka kwa sababu mbali mbali, wengine wametoa mfano kwamba ni utamaduni wetu kuanzisha mambo kama haya lakini *delivery* inakuwa haipo.

Mhe. Spika, mimi ufahamu wangu kwa kadiri nilivyousoma huu Mswada katika kamati na mpaka hivi sasa kwamba hautaondoa au hautakata kiu ya Waheshimiwa Wawakilishi kwa hivyo wanavyochangia wao. Au nisema kwamba halitopatikana jibu la kuondoa kero zilizokuwepo hivi sasa za ukiukwaji wa maadili kwa Zanzibar. Kwa sababu huu Mswada unazungumzia eneo dogo sana na ukiukwaji wa maadili katika mambo na kanda hizi mbali mbali zinazotumiwa. Huu mswada kimsingi unazungumzia juu ya kufanya sensa ya filamu za maonyesho lakini hauna mapana sana ya kushughulikia mambo mengine mengi kama tunavyotaka sisi waheshimiwa kama ya mavazi n.k.

Mhe. Spika, inaonekana kwamba kumbe hata huu Mswada kama tutaupitisha bado kutakuwa na haja ya kutafuta mbinu nyengine ya kushughulikia hizo kero wanazozingumzia waheshimiwa. Mswada huu unazungumzia eneo dogo sana la hizi kero za maadili zinavyovunjwa. Kwa hivyo ukiangalia majukumu yake katika hizo kazi za bodi kuna majukumu 11 yametajwa pale kuhakiki filamu zinazorikodiwa ndani na nje ya Zanzibar. Kwa kweli hapa zinahusu filamu, CD na kadhalika, hawendi mbali zaidi. Kwa maana hiyo hii sheria hata kama itapitishwa na hata kama itasimamiwa kwa asilimia mia moja bado itashindwa kutatua tatizo la Waheshimiwa Wawakilishi hili la ukiukwaji wa maadili katika nchi kwa ujumla. Kwa maana hiyo bado itakuwa sheria haijatosheleza kupambana na yote.

Sasa kuna changamoto mbili ambazo zitaweza kupambana na Wizara. Changamoto ya kwanza ni kuhakikisha kwamba huu Mswada wanausimamia kikamilifu. Changamoto ya pili kuanzia Baraza hili sasa likimalizika waanze kukaa katika wizara ili wafikirie njia nyengine na wafanye nini juu ya hili, kama waje na Mswada mwengine wa sheria ili kufikiria hizi kero nyengine za

Waheshimiwa ambazo humu hazikuwa *covered*. Mswada huu unazungumzia kitu kimoja ambacho ni filamu. Katika uchunguzi wangu hilo ndio jambo moja ambalo ndio nimeliona na nikasema hili kwamba nilizungumze. Kwa hivyo tuna haja ya kuwa na mtazamo mpana zaidi wa kudhibiti haya maovu yaliyozungumzwa na Waheshimiwa.

Mhe. Spika, Mswada huu hautatosheleza kutatua hayo matatizo ambayo Waheshimiwa wameyazungumza kwa upana. Mswada hata ukipita utakuwa unazungumzia maeneo machache. Ukiangalia yote ambayo yametajwa katika kifungu cha 4 hayawezi kutosheleza kutatua hizo kero.

Mhe. Spika, na mimi nije katika suala ambalo waheshimiwa wenzangu wamelizungumzia. Huu mswada wa sheria unapiga marufuku uoneshwaji wa hadharani nao umetafsiriwa ni katika majengo maalum au nje pahala penye mkusanyiko wa watu watatu au na zaidi, kama katika majengo maalum au nje. Hiyo ndiyo tafsiri ya hadharani, lakini kwa watu wanaoangalia mtu na mkewe nyumbani au mtu na marafiki zake, itakuwa sheria haijawabana. Kwa hivyo, hata wanaoangalia nyumbani na sio nyumba ya biashara hawatakuja kubanwa na sheria hii. Sasa je, hawa ambao hawabanwi na sheria hii tuwafanye nini.

Kwa sababu kusema kwamba na hawa tutunge sheria tuwabane watu mpaka katika majumba yao hilo haliwezekani itakuwa tunapingana na Katiba kwa kuingilia uhuru wa faragha wa mtu ambao umekatazwa na Katiba. Ukiangalia ibara ya 25 (1) ( C) ya Katiba inakataza mtu kuingiliwa katika faragha isipokuwa labda kwa sababu maalum, mfano askari wanataka kufanya ukaguzi. Kwa vyovyote serikali haiwezi ikatunga sheria ikasema ipite majumbani na iangalie watu wenye *internet*, pengine mtu na mkewe ndani wamefungua wanaangalia kanda ya X huku tena itakuwa ni kuingilia uhuru wa faragha wa watu, hivyo serikali haiwezi. Lakini hawa *individual* ambao hawapo katika *public* na sasa hivi ndio wengi kuliko hawa waliokuwemo kwenye *public buildings*. Tatizo ni kwamba hii sheria haitoondoa tatizo, itapunguza tu tatizo. Kwa sababu zipo kama hizi *Internet Cafe*, wengine wana *computer* za majumbani, watu wana CD zao wanaingia nazo majumbani. Tatizo bado litakuwa lipo.

Mhe. Spika, tatizo hili linaweza kuondoka labda kwa kujenga maadili katika jamii. Nadhani kama jamii itaandaliwa mpaka mtu mwenyewe akaona mimi kwa umri wangu kuangalia mambo haya katika simu yangu, kwani watu wanaangalia kwenye simu tu siku hizi. Mtu kama huyu utamkamata vipi kwenye sheria, katika simu watu wanaangalia vitu vikubwa vikubwa Mhe. Spika. Nasema matatizo haya ni makubwa kwa hivyo haya yanawezekana kwa jamii kubadilika kila mtu akafika pahala akaona kwamba jambo hili nisifanye.

Kwa hivyo, kazi hii lazima iende sambamba na kufundishwa watu maadili mema, lazima hili lianze chini, kuanzia watoto wadogo waanze kupewa mafunzo ya uadili ili wakue nayo mpaka wafike pahala mtu awe anaweza kujikataza mwenyewe. Lakini kama mtu hujamfundisha akajikataza mwenyewe na akaogopa kuangalia picha nyengine kwa kweli tatizo hilo nasema litakuwa kubwa wala hatutaliweza.

Mhe. Spika, mimi katika kamati niliwauliza swali wenzangu, Mhe. Naibu Waziri alinisaidia sana. Niliuliza swali hili la maadili kwa sababu ukiangalia katika huu mswada ukurasa wa 228 pahala penye ufafanuzi kifungu cha 2 lipo neno maadili. Mhe. Spika, tunaambiwa, "maadili" maana yake ni mafundisho yanayotolewa kwa jamii yenye nia ya kuongoza mwenendo mzuri katika jamii husika. Mhe. Spika, lakini sasa hivi Zanzibar sio jamii yenye utamaduni mmoja tena. Nadhani hili tunaelewana kwamba Zanzibar ya leo haina utamaduni mmoja tena ina tamaduni nyingi. Sasa hivi kuna *conflict* ya *culture* kila mmoja unataka uushinde mwenzake, na inaonekana huu utamaduni wa zamani unashindwa na utamaduni mpya.

Kwa hivyo, hili ni tatizo kwa sababu zamani mwanamke wa Kizanzibari ilikuwa anavaa baibui la nyuzi, sio mabuibui haya ya leo ambayo yanabana sehemu zote zinaonekana. Pamoja na kwamba tunasema wanawake wanavaa suruali vitu vinakuwa viko juu hadharani. Sasa ndio nikasema utaona ndio ile migongano ya utamaduni, huyu mmoja anavaa suruali kitovu nje, lakini mwengine unamkuta anavaa baibui, msalie Mtume. Kwa kweli mabaibui ya nyuzi ukifanyia utafiti nafikiri kwa kutwa nzima sifikirii kama unaweza ukapata hata mabuibui kumi na tano.

Mhe. Spika, nasema Zanzibar sasa hivi ina tamaduni nyingi, maana yale mabaibui asili yake hasa sio ya Zanzibar yanatokea Middle East. Lakini leo imekuwa ni sehemu ya utamaduni wa Zanzibar, haya ya nyuzi ndio hasa utamaduni wa hapa. Kwa hivyo, kila mmoja anajiona yeye ni sawa kwa sababu ukimkataza huyu anayevaa *blue jeans*, lakini na huyu mwenzake anayevaa baibui ambalo limembana mantiki iko wapi. Kwa hivyo, mimi nasema kwa kweli ni vurugu mechi kwa sababu hatuna utamaduni mmoja kama vile Wahindi. Wahindi ukikuta wa kabila fulani wale Mabaniani lazima avae winda. Nakumbuka mwaka mmoja alikuja Makamo wa Rais hapa tajiri mzima yule, basi alikuwa anavaa winda, lakini ndio Wahindi walivyo hata waliopo hapa pamoja na kwamba wapo ugenini, lakini utamaduni wa Zanzibar umeshindwa kuwabadilisha Wahindi.

Hivyo ndio inavyotakiwa sisi tabia yetu ni kama makasuku kuiga tu. Ndio nasema kwamba tuna kazi tena pevu au chukulia wenzetu wengine ukiachia hawa Wahindi, kama jamaa wa Nigeria hata ukamkuta tajiri bado utamkuta

mpaka leo ana heshima zaidi kuvaa yale mavazi ya kwao na hata wakenda katika mikutano ya kimataifa, bado hawathamini isipokuwa kuvaa mavazi ya kwao. Lakini hapa kwetu mheshimiwa tuambizane ukweli ukimuacha maalim Moh'd Ali Salim ambaye alikwenda Lesotho akavaa kanzu na koti nani mwengine anayekwenda nje akavaa kanzu na koti. Sote tukenda huko fahari yetu ni kujitia kitanzi. Mhe. Hamza Hassan Juma hakubali mpaka ajitie kitanzi, awe sawa sawa na Barack Hussein Obama. Nasema hili ni tatizo, maana yake tuna laumu, lakini hata sisi tumeshindwa kujua utamaduni wetu hasa ni upi. Hilo ni tatizo, ndio nikasema hata hii tafsiri ya maadili ni tatizo.

Mhe. Spika, mimi nilitoa mfano katika kamati Mhe. Naibu Waziri alinijibu vizuri niliridhika na alivyonijibu, lakini nilifanya kama masihara nikasema hivyo hizi zinazoitwa *modern* taarab tutaweza kuzidhibiti, kwa sababu *modern* taarab zinavyochezwa ni kama vile alivyozungumza Mhe. Moh'd Ali Salim asubuhi. Lakini nikasema kwamba ile taarab asilia sivyo vile ni kwamba watu wanakaa kitako wenyewe wanafanya mambo yao raha mustarehe. Sasa ukimwambia huyu kwamba usifanye hivyo, itabidi kwa sheria hii sasa tuingie katika *hall* lile la Mafunzo.

Kwa sheria hii, itabidi bodi siku ya Jumamosi tupeleke vijana pale Mafunzo, wakaangalie taarab hapo siku zote huwa wameshamkodi Khadija Kopa kwani anapocheza huwa ana michezo yake hawezi kuibadilisha. Ukija kumwambia kwamba hivi ni kinyume na utamaduni wa Zanzibar, hilo litakuwa ni tatizo. Ukimwambia acheze kama maadili ya taraab zile za zamani atakwambia hii ni *modern taarab,* sio taarab ile ya zamani. Mhe. Spika, ndio nikasema kwa kweli hili tatizo ni gumu, wala sio rahisi kama tunavyolifikiria. Hili suala ni gumu na lina matatizo mengi.

Mhe. Spika, tukija katika hizo harusi ambazo tunasema ni za kizamani mama zetu wameolewa wakati huo wa unyago. Mhe. Spika, unyago huwa unachezwa ndani, lakini kwa wenzetu jamii kama za Kimakonde haumalizii ndani, siku ile ya kutolewa mwari lazima uchezwe nje. Siku nyengine utachezwa ndani ni sawa, lakini ile sheria ya kwamba *public* itakuwa haijawabana kwa sababu ile si *public,* ni nyumba yao ya ndani wana shughuli zao. Lakini kuna siku lazima mwari atolewe nje ukija ukimwambia kwamba jamani kidogo punguzeni mambo, hivyo hawatakuelewa kwa sababu ni utamaduni wao.

Mhe. Spika, ndio nikasema kwamba Zanzibar haina tamaduni moja bahati nzuri ina *communities* nyingi na bahati mbaya sana niseme kila *community* ime-*retain culture* yake, hatujafika pahala tukaona *culture* moja. Hili ni tatizo. Kwa hivyo haya mambo kwa kweli yanahitaji kufanyiwa *research* ya kutosha katika kutekeleza, vyenginevyo yanaweza yakaleta matatizo.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba nilikuwa Mjumbe wa Kamati, sina mengi isipokuwa naomba nimalizie kwa kutanabahisha tu, kwamba sheria hii mimi ninavyoiona italeta ugumu katika utekelezaji wake bodi iwe makini na iwe na watu mahiri. Kwa kweli wasije wakafanya makosa wakaja wakamfikiria kila mtu anafaa kuwa Mjumbe wa Bodi, watakapofika pahala wakafikiria kwamba kila mtu anaweza kuwa mjumbe wa bodi, nadhani tatizo linaweza likatokea.

Mhe. Spika, mimi ninavyoiona bodi hii inataka iwe na watu wa aina mbili. Kwanza inatakiwa watu Mhe. Salmin Awadh Salmin yeye alisisitiza wachukuliwe watu katika vyama vya kiraia *NGOs.* Mimi nakubaliana na rai zake, lakini pia mimi nafikiria tusije tukaangalia watu labda kwa elimu zile za madarasani tu, lakini wajumbe wa bodi lazima tuangalie watu waliokuwa wana uzoefu mwingi wa maisha ya tamaduni hizi. Lazima watu kama hawa tuwapate kwa sababu watatusaidia kwa mengi sana. Kwa hivyo, lazima bodi iwe na watu wasomi, wa kileo na vile vile iwe na watu wazima ambao kweli wanajua hasa hizi tamaduni zilizopo Zanzibar ni zipi, ili kila mmoja tumjengee heshima kumlindia utamaduni wake na tufike pahala tukom-*promise which culture should prevail,* lakini naona kwa kweli ni tatizo na linaweza likatuletea matatizo.

Mhe. Spika, nije hapa katika haya madhumuni unajua katika hili Mhe. Zakia Omar Juma alinukuu katika madhumuni na sababu anasema. "Mswada huu unakusudia kuweka sheria ya kuanzisha Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho Zanzibar. Mswada wa sheria unaopendekezwa unakusudia kulinda na kuhifadhi mila, silka, utamaduni na maadili ya Mzanzibari, na kwamba sanaa haitumiki kupotosha maadili hayo". Kwa hivyo, wao hapa wamesisitiza sanaa haitumiki kupotosha maadili, wamekuwa wajanja sana wamejifunga hasa kwamba wao wanachosikiliza hapa ni sanaa na sio yale mambo mengine ambayo tumeyachangia. Kwa hivyo, mimi naomba tusiishie kwenye sanaa wakae wafikirie na mambo mengine kwamba hayapotoshi jamii. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Suleiman Hemed Khamis:** Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuzungumza machache juu ya suala zima la uanzishwaji wa bodi ya sensa, lakini badala yake tutasema uhakiki, filamu, sanaa na maonesho.

Mhe. Spika, neno uhakiki ni neno sahihi zaidi kuliko hili neno sensa, kwa sababu neno uhakiki tunalitumia mwahala mwingi sana, mfano Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi katika vyombo vyote vya wananchi na vya serikali inafanya uhakiki wa vyombo hivyo. Kwa hivyo, neno uhakiki ni kama kuchunguza au kukagua kitu ukaangalia zile kasoro zake na ukataka zile kasoro

ziweze kurekebishwa. Hili tunalolifanya hapa litakuwa katika hili tunalolizungumza kama ni sensa, lakini itakuwa ni kulihakiki jambo kwamba unajua lile neno lazima litakuwa lina matatizo, kwa hivyo unataka liwekwe katika njia nyengine. Kwa hivyo, neno ambalo litakuwa muafaka hapa badala ya sensa nafikiri ni neno uhakiki, ni neno rasmi na nafikiri ni neno bora zaidi.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme tu kwamba Zanzibar tunao utamaduni wetu ambao ni wa asili. Tuna mila zetu ambazo ni za asili, tuna silka zetu, tuna hulka zetu yaani tabia zetu na tunajuana kwa tabia zetu na pia tunajuana katika nyenendo zetu zote Wazanzibari. Mimi nataka niseme kutokana na yote haya mila zetu, desturi zetu pamoja na kivazi ambacho ni cha asili tulichokuwa tukikitumia na mwendo wetu wa asili pamoja na muelekeo wetu katika suala zima la utamaduni. Sasa hivi tunaona kwamba Zanzibar hakuna utamaduni wa asilimia juu ya mia kwa hivi sasa. Zamani miaka ya nyuma tulikuwa nao utamaduni wa asilimia juu ya mia, lakini ni kitu gani kilichofanya hata hii asilimia juu ya mia ikapotea ni kutokana na maingiliano ya watu ndio uliotufanya sisi katika suala zima la mila zetu, desturi zetu, itikadi zetu tulizokuwa nazo zote zimeweza kubadilika kutokana na mchanganyiko.

Sasa kwa Unguja kwa hali ilivyo hivi sasa na ukilinganisha Unguja na miaka iliyopita haiwezi kuwa sawa sawa bila shaka sote tunaona kuna mabadiliko ndani ya nchi. Mabadiliko yanakuja pale ambapo watu wanaingiliana pahala pamoja yaani wanatoka sehemu fulani wanaingia sehemu fulani wanakuja na tamaduni zao, mila zao na desturi zao na hulka zao, ni lazima walioko pale itategemea *strength* iko upande gani, *ethics* iko upande gani katika mambo haya yote kwa jumla. Ni wepi watakaozidiwa kama wao ni wengi sana wanaweza wakabadilisha mila na desturi za mahala pale kwa wale ambao watakaoingia.

Kwa hivyo, sisi tunavyoamini hapo miaka ya nyuma kwamba asili yetu sisi tulivyowaona wazee wetu walikuwa wanavaa kanzu, kofia, koti na viatu vya makubadhi hiyo ndio asili yetu. Ukenda sehemu yoyote ya Unguja, utakuwa hiyo ndio asili yetu. Lakini nani aliyebadilisha kivazi hiki cha kanzu, kofia na koti. Wengi jamii ya sasa hivi utawakuta kivazi kile kimeanza kupotea. Hata elimu ambayo sisi ilikuja ikaingiliana baina ya mtawala sultan pamoja na watawala wengine waliokuja kutoka Europe. Maskuli ambayo tuliokuwa tumejengewa tayari yameweza kubadilisha mila zetu, desturi zetu na mwenendo wetu ambao tuliokuwa tumeanza zamani. Zamani ilikuwa mambo mengi ni ya vyuo, skuli ilikuwa hakuna baadae zikaingia skuli ndio zikaanza kubadilisha desturi zetu na mwenendo wetu tukakuta badala ya kuvaa kanzu hatuvai tena kanzu na nafikiri hayo nitakayoyasema wengi mtakuwa mashahidi mnayajua.

Nakumbuka hapa hapa Unguja kulikuwa na baadhi ya skuli ziliwahi kuleta matatizo baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na baadhi ya skuli nyengine ambazo watoto wao kama Maruwehi ilikuwa lazima watoto wao wavae kanzu. Nafikiri hili hamuwezi mkakataa kwani hili suala lilikuwepo. Serikali ikasema hilo hapana lazima wavae suruali na shati. Sasa ndio utakuta imeanza kupotoka hii kidogo kidogo sasa hivi ni mchanganyiko. Kwa hivyo, hatuwezi tukasema sasa hivi utamaduni wetu kweli ni asilimia mia moja, tunaweza tukakisia tu labda ni asilimia ngapi ya utamaduni wetu.

Kwa hivyo mimi nataka tuulizane je, kwa wakati huu hivi sasa tunaelekea wapi? Kama tunataka utamaduni wetu urudi ule wa asili, je inawezekana kurudisha utamaduni ule ule. Ndio maana ukaona katika karatasi hii ina ufinyu wa maelezo, imezungumzia habari ya mambo ya kanda, mambo ya filamu na mambo ya maonesho na sanaa. Lakini utakuta sisi wazungumzaji haiwezekani kuzungumza hili tu bila ya kuzungumzia ule utamaduni wetu wa asili. Kwa hivyo, ndio maana utakuta tunachanganya yote tunayatia pahala pamoja.

Mhe. Spika, mimi niseme tu kwamba utamaduni wetu umeanza kupotea katika miji ya Zanzibar, lakini unapokwenda katika sehemu za mashamba utakuta kidogo kuna tofauti baina ya shamba na mjini. Kidogo shamba kuna mambo ambayo yale ya asili wanaendelea nayo, lakini ukija katika maeneo ya mjini ambapo kuna mkusanyiko wa watu wengi wa sehemu mbali mbali wanaingia pale, utakuta pale kuna maingiliano ya watu kwa hivyo hawa ndio waliosababisha utamaduni ukapotea hasa katika maeneo ya miji.

Mhe. Spika, mimi nasema tu kwamba itafika wakati utamaduni wa Zanzibar utapotea kama hatukuchukua hadhari kidogo kidogo, lakini mimi nashukuru kwa hapa hatua iliyoanza kwa wizara hii kuanza kutunabahisha. Kwa sababu mimi nasema kwamba tumechelewa tulikuwa wapi kwa muda wote huo zaidi ya miaka 40 ya utawala. Suala hili lilikuwa lisiletwe leo tuangalie tunakwenda na nchi na maendeleo ya nchi, lakini na utamaduni umeanza kupotea miaka arubaini iliyopita, leo ndio tunataka kurudisha utamaduni. Je, inawezekana kurudisha huo utamaduni? Mimi nasema sio rahisi hilo tumechelewa.

Mhe. Spika, suala hilo halikuulizwa limepotea na ile kauli ambayo nafikiri Rais wetu alianza kuzungumza zamani Rais Ali Hassan Mwinyi alisema "Unguja ni njema atakae aje". Watu wamekuja lakini hatukuangalia kwamba mila zetu, tamaduni zetu, silka zetu, hulka zetu na tabia zetu zitapotoka. Tumeangalia maendeleo tu, lakini hapa tumepasahau tunamshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kumtanabahisha waziri kuanza kuleta haya kidogo kidogo ni kwamba akili sasa hivi imeanza kufunuka baada ya miaka 40 kupita.

Hili tunasema kwa ufupi ni suala zima tayari matokeo yake sasa tunasema ni kuporomoka kwa maadili ya Wazanzibari. Tukifanya tathmini sasa hivi

tunaweza kutathmini kwamba tuko katika asilimia fulani ya utamaduni tulionao Zanzibar. Kwa hivyo, nani aliyeathiri huu utamaduni wazee wa zamani katika utamaduni huu hawakuathirika, watakaoathirika hivi sasa katika utamaduni ni hao watoto wetu ambao tunaita *future generation* ambao wanazaliwa sasa. Hawa ndio watakaoathirika kwa sababu sasa hivi kwa vyovyote kwa hali yoyote vijana wetu tuliokuwa nao wamekuwa wakaidi, wamekuwa washupavu, wamekuwa sio wasikivu kutokana na hali ya utamaduni ambao unaingia hivi sasa.

Zamani ilikuwa hakuna suala zima la madawa ya kulevya na sote tunakubaliana hapa, lakini sasa hivi angalia vijana wetu asilimia ngapi ya vijana wetu wemashaanza kupotoka. Hii ni kuonesha maadili ya vijana yameshaanza kuporomoka na vijana wanaanza kututoka kidogo kidogo na hasara kwa taifa. Vijana hawa ambao hivi sasa wapo *Mental Hospital* na wengine wamo ndani ya majumba vitendo vinavyoendelea sasa hivi kwa vijana wetu, hivyo kweli hiyo ndio tutaita *future generation* yetu itakayosaidia baadae, haiwezekani.

Kwa sababu hao vijana watakaokuja ni wendawazimu watupu sasa tutawategemea nani. Mimi nasema hili suala lililokuja mara hii halitoshi na lifanyiwe upanuzi zaidi na tuangalie hali halisi ya hivi sasa inavyojitokeza, kwa nini likatokezea hili lililotokezea hivi sasa mambo ya ubakaji. Hivyo miaka ya nyuma ya utamaduni wetu, mila zetu na desturi zetu na wazee wetu walivyotulea mambo ya ubakaji tuliwahi kuyasikia haya, sasa hivi yametokea wapi haya mambo ya ubakaji mtu wa miaka arubaini au hamsini anambaka mtoto wa miaka kumi na mbili. Kitu gani kilichofanya hivi mtu huyu huyu tunae katika utawala huu wa miaka arubaini sasa hivi anafanya vitendo vya kubaka.

Kwa hivyo mimi nasema hili suala lililokuja ni muhimu sana tuliangalie kwa makini na undani zaidi. Mimi naona kwa kuanzia haidhuru kwenye sensa bodi ifanyiwe uhakiki, lakini na huku tuingie na tuangalie haya yametokezea na yanaendelea kutokezea na idadi ya watu ambao wanafanya ubakaji hivi sasa idadi inaongezeka. Hilo ni suala muhimu vile vile kuangaliwa tuangalie historia yetu ilikotoka na tuangalie hivi sasa.

Mhe. Spika, filamu ni kanda ambazo tayari zimerikodiwa, na hizi kanda ambazo zimerikodiwa kuna kanda zilizorikodiwa hapa Unguja, kuna kanda zilizorikodiwa Bara, kuna kanda zilizorikodiwa nchi za nje, kutoka Europe zinaletwa hapa *cassette* chungu nzima. Zipo tena nyingi sana. Kwa hivyo, tunazo zetu za Unguja, tunazo za Bara, tunazo zile zinazotoka nje, katika kuangalia mambo haya tuangalie kanda zote tatu. Tuangalie kanda zetu za hapa Unguja zinazorikodiwa hapa, tuangalie kanda ambazo zinarikodiwa kutoka

Bara na tuangalie kanda ambazo zinatoka nje ambazo vijana wetu wanaziangalia.

Mimi nasema kwa jumla kanda zote hizi zina kasoro tena kubwa sana na kama tusipoangalia vizuri, basi hiyo *future generation* ambayo ya watoto wetu ambao tunawategemea watoto watakuwa na akili za kupumbaa pumbaa hawatokuwa na akili nzuri. Kwa sababu wanapata mambo yaliyokuwa hayamo katika maadili yetu wanachukua mambo zaidi kuliko ule uwezo wao. Mtoto wa miaka minane au miaka kumi na mbili unakwenda kumuweka mbele pale anaangalia *cassette* ambayo ndani yake imerikodiwa machafu matupu, atajifunza nini mtoto yule. Mtoto yule ataanza kuwa jeuri, mjuba, hana adabu, hasikii na anaona yeye ameshakuwa mkubwa sana wa kuweza kufanya yale.

Mimi nasema suala hili sio geni katika nchi hii. Suala la kuhakiki filamu zilizokuwepo katika nyumba hizo za burudani, hizi zilikuwa zikihakikiwa na kanda ambayo ilikuwa inaonekana kwamba ni chafu, basi sehemu ile yote inatolewa. Kama alivyozungumza mwenzangu nafikiri Mhe. Ali Abdalla Ali alizungumza hapa, akasema kwamba tunataka tuone kile kitendo kichafu hakimo hasa katika kanda ile, isingojee mtu ambaye anaona kile kitu anajua sasa hivi wanaingia ndani wanakwenda kufanya nini, sasa hivi ndio inavyojitokeza. Mhe. Spika, unamuona mtu tayari anavua nguo na mwengine anavua nguo huwa kuna nini zaidi ya hilo, hakuna jengine. Kwa hivyo, hapo mtoto huwa ameshajifunza jambo baya pale. Mimi nasema hili suala alilozungumza Mhe. Ali Abdalla Ali naliunga mkono kwamba hilo lisiwemo ikiwa tunataka kuhakiki filamu zote, ikiwa ni sinema basi tuhakikishe lile tendo linaloonekana ni la dhahiri kwamba litatokezea likatwe mtoto asilione.

Waheshimiwa Wajumbe kwa taarifa yenu maduka ya *cassette* yamekuwa ni mengi sana, si hapa tu Unguja mpaka Pemba kila kichochoro maduka hayo yapo. Watoto hawazuiliki, watoto ambao wadogo wadogo kuna maeneo wanafungiwa maplastiki ya mchele wanajaa tele na hawarudi kwao kama si saa saba au saa nane za usiku, haya mtoto huyo baba atamuweza tena na hazuiliki? Sasa mimi nasema kitu kizuri apewe mtoto kukiona lakini tukihisi kwamba hii *generation* itakuja kuharibika basi tuanze kukidhibiti na mapema.

Mhe. Spika, filamu za nchi za nje sasa hivi vile vile zinakuwa mbaya kwa sababu zinaonesha mambo mabaya tu, kwanza tuachane na wazungu kwa sababu hulka zao na zetu sisi ni tofauti kabisa. Mtoto wa kizungu haoni haya kumuuliza baba yake hiki nini atamuuliza pale pale mbele ya mama yake na watu wengine. Sisi kwa desturi zetu hatuwezi, atamtafuta baba pembeni amuulize baba hiki nini? Pengine asimuulize hasa atavumilia atakuja kujua baadae. Lakini kwa maumbile ya watu wa *Europe* kitu chochote kwao hakina aibu na anaweza kuuliza jambo saa yoyote, mahala popote na kitu chochote

anachokitaka na kupata jibu *immediately* bila ya ku-*hesitate* kwamba nitakupa halafu au baadae, atampa pale pale.

Sasa mimi nasema hizi kanda kwa kweli tunataka watoto wajifurahishe lakini hii kazi ya bodi ambayo itaifanya hii kazi ni kazi kubwa sana, *let us admit the fact* kwamba hii kazi ni kubwa tena ni nzito kwa bodi tu peke yake haiwezi ikaikamilisha.

Kwanza ninachofikiria kwa wakati uliopo hizi kanda ni nyingi sana. Mimi nataka kutoa ushauri kwamba kuanzia hivi sasa wizara ianze kuchukua hatua kanda yoyote isiingie mpaka hizi zilizopo zimalize kuhakikiwa, zihakikiwe zimalize zionekane hazina matatizo halafu watu wapewe. Kama tukiruhusu kuingia kanda na mbali ya kanda zilizoko Unguja na Pemba katika *window shops* hii kazi itashinda kweli, ni ngumu sana nawasikitikia bodi labda bodi ziwe 20 ndio wamalize hii kazi lakini kwa bodi moja hawawezi wakamaliza.
Suala la hadharani kisheria sawa, sasa yule baada ya kuhakikiwa labda atakwenda lakini jinsi gani tutazidhibiti kwamba katika duka hili zimo kanda zaidi ya 2000 mpaka 3000, ni lazima kila kanda ambayo itakuwa imehakikiwa pawe na alama fulani au kitu fulani cha kuonesha kwamba hizi zimeshapitiwa na nyengine bado, sijui utaratibu utakaopita. Bodi wana kazi kubwa sana nawapa pole. Lakini kuna zile nyengine ambazo zinafanywa si katika eneo la nje lakini zinachukuliwa ndani, watu wanachukua kanda chafu wanatizama ndani ya nyumba yao wenyewe kama ikiwa baba, mama na watoto wanaangalia au wanangoja watoto wameshalala wanaangalia kanda yao lakini kwa nini iwe hivyo? Kuna lipi kubwa? Naona mambo ni yale yale.

Mimi nafikiri tuifanye hiyo kazi bwana tuziangalie kanda zote tusikubali nchi yetu kuchafuliwa namna hiyo. Kwa sababu tukiruhusu kanda hizi kuingia utakuja wakati ambao sisi wenyewe tutakamate vichwa hatujui tufanye nini tutaanza kuwapiga magongo watoto wetu wakati wakosa ni sisi wenyewe. Sisi ndio dhamana ya watoto kwa sababu tunakinga watoto wa baadae ambao tunategemea ndio watakaokuwa mawaziri, marais na kila kitu ndio watakaoendesha nchi hii, lakini *where are we leading them*? Mimi nafikiri tufanye kazi ya kutosha maduka ya *cassette* tuyaangalie vizuri.

Mhe. Spika, sheria ipo imeshaandaliwa lakini bado iangalie vizuri katika mambo yote kwa jumla. Televisheni zipo, simu zipo, sasa hizi televisheni nyengine haijambo kama hizi zetu zinaonesha saa mbili au tatu, lakini kuna kipindi fulani kama saa nne au tano huko televisheni pia inatoa habari mbaya mbaya. Jamani hizi zitatupeleka pabaya sana.

Mhe. Spika, tuna simu hizi za sasa na watoto wote wanaweza wakatumia simu kuliko baba, mtoto anajua namna ya kuisanifu na akakwambia hapa kuna hiki

na hiki watoto wamekuwa *very expert* mahodari kweli kweli. Sisi hatushughuliki lakini wao kila kitu wanakijua na wao ndio wa mwanzo kuangalia hayo mambo mabaya. Sasa tuseme huu utamaduni kweli tukitathmini hapa Zanzibar *average wise*, tuangalie watu wangapi wanamiliki simu katika nchi hii mimi nafikiri robo tatu ya Wazanzibari wanamiliki simu labda robo moja tu ndio hawamiliki. Watoto wanawake wote wana simu, watoto wanaume wengi wao wana simu vile vile wana-*communicate* nini zaidi ya hayo tunayosema kwamba ni ya maasi? Hakuna zaidi.

Mimi nafikiri tuna kazi kubwa sana hizi simu nyengine hazidhibitiki kwa sababu tayari watu wako katika biashara, huu ni ulimwengu wa kibiashara wanatanua biashara zao lakini ndani ya biashara zile mna mambo ambayo hayaridhishi kama tuna njia ya kuyazuia haya nafikiri tuyazuie.

Mhe. Spika, katika suala zima la ngoma na ndani ya ngoma kuna mambo mawili, kuna uchezaji, ndani ya ngoma inaweza kutoka nyimbo. Nyimbo zetu nyingi ambazo zinatoka katika ngoma kwanza nakwambieni huo msondo siku hizi ushapotea haupo hasa, na sidhani kama kijana wa leo ukamwambie fanya utamaduni wetu ukamuweka pale atakwamba hizo zilipendwa nafikiri hiyo ndio lugha inayotumiwa. Lakini sasa tutafanya nini ili kumuokoa huyu kijana? Ngoma zetu ni lazima tuweze kuzirekebisha ziwe nzuri ili tuondoshe yale ambayo tunayazungumza sasa.

Hivi sasa kuna mambo ya kuzungurusha zungurusha, haya kidogo yana matatizo kama wenzangu walivyozungumza, si vizuri mbele za watu. Kama ingekuwa mtu yule ambaye anafanya vile ni mwanawe mmoja wetu angefurahi? Kama mmoja wetu ni mwanawe wa kumzaa anayefanya mambo yale angelifurahia hilo suala? Angelifumba macho au angeondoka kwa sababu ile ngoma haichezwi kama ilivyokuwa ikichezwa zamani, inachezwa kwa miundo ya kisasa kuwavutia wale watizamaji na kama hawakufanya vile itaonekana ngoma hajaicheza vizuri. Mimi naona hapa lazima tuangalie vizuri.

Vile vile na nyimbo zetu tuziondoshe bwana, mna mambo mengi ya vivutio katika nyimbo hizo zinawavutia vijana. Kwa hivyo, hizi nyimbo vile vile ziweze kuchunguzwa na kuangaliwa. Nyimbo zetu za Kizanzibari, nyimbo zetu zinazotoka Bara na nyimbo ambazo zinatoka nje pia ziangaliwe kwa vizuri. Kwa hivyo, mimi nasema bodi hii ya kuhakiki mambo yote haya yaliyokuwa hadharani na mengineyo peke yake itakuwa ni vigumu sana, ningeomba kwamba hili suala wachangiwe na watu wengine japo kwa *private sector* ziweze kuingia ili kuweza kuwapa msaada.

Kwa mfano, hivi sasa utakuta kuna vikundi vya Dini ya Kiislamu, vikundi hivi kwa kweli vimepiga hatua kubwa sana, wameweza kuwadhibiti wanawake kwa

mafunzo maalum kila jioni wanapata mafunzo na elimu ya kutosha, haijambo wengi wameweza kustirika. Sasa mimi nafikiri kitu kama hiki kuweza kufanya katika makundi mengine ya jamii hilo suala lingeweza kusaidia. Tuweze kuangalia sio katika jamii tu kuangalia katika michezo yetu athari zote zinazotokea hasa katika ngoma zetu za kitaifa na zilizokuwa si za kitaifa vile vile.

Mhe. Spika, masuala haya mimi naweza nikayatabiri kwamba hayako katika *short term program* mambo haya ni ya *long term program*. Kwa sababu unapopanga malengo yako unaweza kuangalia haya ni malengo ambayo yatakuwa ni ya muda mfupi na yatakayoweza kutekelezeka au *program* zake ni *long term.* Hii ni *long term program* ni *term* ambayo itachukua muda mrefu sana.

Mhe. Spika, hakuna mtu ambaye hataki mabadiliko *we need changes*, kwa nini tukataka mabadiliko? Kutokana na haya machafu lakini sasa wewe ikiwa huna sauti ya kuzungumza ndio pale utaona machafu bado yanaendelea. Sasa sisi tuliomo ndani ya Baraza tuna wajibu wa kuyasema haya na tuna wajibu wa kuishauri wizara au serikali kutokana na haya kwamba tunahitaji mabadiliko kwenye machafuko ya utamaduni wote wa Zanzibar urudishwe ule ule wa zamani kama itawezekana. Lakini tutadhibiti vipi? Swali ndio hilo. Mimi nafikiri hakuna miujiza katika swali, huwezi kulifanya suala lile kwa mara moja ukaweza kufanikiwa, nahisi tuweze kupiga hatua baada ya hatua ingawa hapa programu yake imelenga kwa vitu maalum lakini utaona inahusu kwa jamii yote ya Kizanzibari.

Mhe. Spika, taratibu zote lazima ziwekwe, kila aina ya taratibu zinazohusu masuala yetu ya utamaduni ziwekwe, uhakiki uwe mzuri, michezo yetu ambayo vijana wetu wanacheza iweze kuhakikiwa vizuri, maonesho yatakayotolewa baadae ya aina yoyote ni lazima yahakikiwe vizuri sana, filamu zetu ikiwa ni sinema, ikiwa za kaseti ziangaliwe vizuri, matangazo yetu yote ambayo tunayaweka hadharani ni lazima tuyakague kwa vizuri sana. Kwa hivyo, naishauri bodi kwamba la muhimu kwa wakati tulionao iweze kutoa elimu kwa wanaohusika hilo ni jambo muhimu, tena hii elimu itolewe kwa makusudi kabisa watu waalikwe waelezwe.

Halafu ningefikiria kitu kimoja, kwa hatua yoyote ambayo tutaweza kuipiga baada ya kutoa elimu tuweze kutoa elimu hiyo tuitathmini kwa asilimia ngapi. Je, tumeweza kufanikiwa? Je, hatukuweza kufanikiwa? Ikiwa hatukuweza kufanikiwa tufanye nini? Kwa sababu huwezi kufanya jambo katika programu ya muda mrefu ikawa umefikia nusu ya ile kazi au robo bila ya kuifanyia tathmini ni lazima uifanyie tathmini na wenzako uwajulishe kwamba hapa nimefikia na nategemea kupata mafanikio. Kwa hivyo, ningeishauri hii bodi

isifanye mambo yake kimya kimya lakini iweze kutathmini masuala mazima yote haya yaliyokuwemo katika karatasi hii itoe kwa asilimia ngapi.
Halafu jengine katika hii hii bodi ambapo bodi hii ina kazi kubwa sana nidhamu ya kazi lazima iwepo. Kwa sababu tunasema watu wawe *answerable* katika kazi zao kwa sababu kuna maelezo ya kazi kwa kila mmoja ambayo anapewa *job discribution* wewe utafanya hili, wewe hili na wewe hili. Sasa mtu ambaye anakabidhiwa kazi tuhakikishe kwamba huyu ana nidhamu kazi yake ambayo ni *allocated* kwake awajibike katika kazi yake. Kwa hivyo, hii ni kazi ya bodi au mkurugenzi au yeyote atakayekuwa ni lazima ahakikishe kwamba nidhamu ya kazi inapatikana.

Pili Mhe. Spika, ninalotaka kusema ni viwango vya utendaji. Ni lazima viwango vya utendaji viwe vizuri ili kuweza kulisaidia taifa hili.

Mhe. Spika, la mwisho ni kwamba kanuni zote za wafanyakazi kupewa nguvu za kisheria. Kwa sababu kwanza kazi ianze katika bodi, bodi iwe na uwezo, nguvu, nyezo, iwezeshwe, hayo yote yakipatikana nafikiri tunaweza kupiga hatua nzuri.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nakushukuru sana ahsante.

**Mhe. Ali Denge Makame:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia Mswada wa Sheria ya Sensa na Sanaa za Maonesho pamoja na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, awali ya yote niipongeze wizara hii kwa kuanzisha mswada huu na kuuleta hapa kwa kuuchangia na kuupa baraka zake.

Mhe. Spika, kweli sasa hivi kuna haja kubwa ya kuunda bodi hii ya kuangalia masuala haya. Kwa sababu sasa hivi baadhi ya mila na silka zetu nyingi zimekuwa zinapotoshwa au hazifuatwi kwa mujibu wa utaratibu ulivyo. Sasa hivi kuna wimbi kubwa la vijana wetu au watu mbali mbali ambao baada ya kuenzi na kutunza silka na mila zetu wanazipotosha kwa makusudi. Hivi sasa utakuta vijana wengi ambao kwa makusudi nidhamu, heshima na taratibu za kuilinda nchi hawana. Utamkuta kijana anafanya maovu basi wewe mtu mzima unamkataza hayo majibu atakayokupa utakamata kichwa hujui useme nini. Kwa mfano, vijana wale wanaochunga punda wanapakia mizigo kupita kiasi na ukimuonya tu basi anakupa jibu kwamba mlete mzazi wako ikiwa wa kike au wa kiume ili abebeshwe ile mizigo. Kwa hivyo, nidhamu na heshimia zimekuwa hafifu, hivyo kuundwa chombo hiki kwa kweli kitaleta faraja kubwa kupunguza au kuondosha kabisa masuala hayo.

Hapo miaka ya nyuma kama miaka 50 mpaka 60 kulikuwa na wakuu walikuwa wakiitwa Mudiri, baadhi ya mambo mengi yalikuwa yakikwepeka kwa kuwa baadhi ya mambo walikuwa wanaamua wao wenyewe. Mtoto kafanya maovu anachapwa matokeo yake yale masuala yanakwenda vizuri. Tumekwenda hatua mbali mbali ikawa hayo mambo yanaundiwa taratibu na yanarekebishika nakukaa vizuri. Lakini hivi siku za kati kati vijana wetu wamepamba moto wamekuwa waharibifu na hawataki kusikiliza wazazi na maamuzi ya wakubwa wao wanafanya wanavyotaka. Kwa hivyo, kama kutakuwa na bodi basi baadhi ya mambo yatanyooka na hii mila na utamadumi utahifadhika na utakuwa na hadhi kama ulivyokuwa hapo zamani.

Mhe. Spika, kama mambo ya utalii au mahoteli ni mipango ya kileo lakini kwa kweli kuna baadhi ya wawekezaji wengi kwa baadhi ya nchi kama Arabuni na nyenginezo utakuta wanafuata mambo ya mila za kiasili za nchi zao, lakini bado mahoteli yale yanakwenda vizuri. Hapa petu watoto wetu wameharibika kweli wanapenda kuiga mambo ya wageni na wanapotosha utamaduni wetu. Kwa hivyo, kama bodi hii itapata mwekezaji angalau kutoa mifano ya mwekezaji huyo ikiwa wa ndani au wa nje yaani ile hoteli ichukue mila za Kizanzibari tu basi kidogo italeta matumaini na faraja kwa wale wageni ambao watafika katika hoteli ile.

Kwa mfano, kama mwanamke anaweza kuvaa mitandio au nguo zilizokuwa zinastahiki, akinababa wakavaa kanzu za darzi na fimbo zao basi italeta mfano mzuri na wageni wengi katika mahoteli kama yale watapenda. Kwa hivyo, bodi hii kama itatoa taaluma kwa baadhi ya wawekezaji ili mmoja kufanya mfano kama huo basi italeta kivutio kwa baadhi ya wageni wanaokuja katika nchi yetu.

Kama inavyoeleweka nchi ya Zanzibar iling’ara na ilivuma kwa silka na mila zake za kitamaduni jinsi zilivyokuwa zikiwakarimu wageni mbali mbali waliofika hapa visiwani. Kuna mambo ya ngoma na tuna ngoma nyingi tu za asili ambazo ni nzuri zinavutia zikipigwa na zina michezo mizuri, lakini vijana wetu wa sasa wanazidharau na kufuata ngoma za kileo ambazo hazina faida kwetu. Kuna ngoma za taarab, msewe, beni ambazo zikipigwa zinafurahisha na haziharibu silka na mila zetu. Kama hizi beni utakuta wanakuja wageni kama unawaelimisha watakuwa wanacheza, kuna wazungu wanacheza ngoma hizo wamejitanda kama sisi wenyewe, akinababa wa kizungu wanacheza japo hawajui kucheza vizuri lakini wanacheza na inaridhisha na kufurahisha. Kwa hivyo, utakuta ngoma kama hizo zilikuwa zinaridhisha na zinalinda silka na utamaduni wetu. Bodi hii kuundwa kwake nafikiri itasimamia na kutoa taaluma kwa watu kupitia vyombo vya habari ili kufuata silka na mila zetu hizo.

Mhe. Spika, leo kuna ngoma ambazo zimejitokeza lakini utashangaa zinaharibu silka na mila zetu. Kwa mfano, kuna ngoma za kibuki, sunsumia, kwa kweli hizi ukizitizama kwa undani mchezo wake na mambo yake yanaharibu mila na silka zetu. Ngoma hizi utakuta zinakwenda kinyume na mila na silka za Kizanzibari. Ngoma hizi kama zitabadilisha michezo yake na mipigo haina haja ya kufungiwa, lakini kama itaendelea kama hivi zinavyofanywa kwa kweli zitaharibu mila zetu. Kwa hivyo, warekebishe michezo yao hawawezi kurekebisha basi bora zifungiwe kama si hivyo zitaharibu mila za watu wetu.

Mhe. Spika, kwa kuwa mambo mengi zamani yalikuwepo yanabadilika kidogo kidogo na mengi kuzidi tena. Kama inavyoeleweka huko tunakotoka binadamu tulikuwa tunavaa majani, tukavaa mavazi ya wanyama kama ngozi, tukaja tukavaa nguo ambazo nzuri tu na mpaka kurudi kule kule kuvaa nguo ambazo hazistahiki. Kwa hivyo, utakuta taratibu hizi kama zitasimamiwa huenda tukakaa vizuri na tukavaa mavazi yanayostahiki katika nchi yetu. Kwa sababu vijana wetu wengi wanaiga tu lakini kama wataelimishwa na kupewa taratibu za kuvaa mavazi ya mila zetu, kwa kweli watapendeza na kufurahisha na kumuweka mtu pahala pazuri. Vile vile inakuwa tija kwa wale wageni wanaotutembelea na kufurahi sana kama watatukuta tumevaa mavazi ambayo yanastahili mila zetu. Lakini kama tutafuata mavazi ambayo si ya mila zetu tunaharibu silka na sifa zetu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, bodi hii pindipo ikiundwa na *section* zake zote kikamilifu haya mambo huenda yakapungua. Hapo nyuma tulikuwa na mavazi membamba ikawa kishindo watu kukamatwa kwa sababu ya nguo nyembamba na fupi matokeo yake yakaondoka yakaja mavazi ya nguo pana, nazo zikaondoka lakini sasa zinarudi tena zile nguo za kashfa. Mhe. Spika, haya yote kama yatakaliwa kitako kupangiwa utaratibu mzuri tutakwenda vizuri.

Mhe. Spika, nije ukurasa wa 229 kifungu cha 4(b) naomba kunukuu:-

Kifungu Nam. 4(b):

> ”Kuhakiki filamu zitakazorikodiwa ndani au nje ya Zanzibar kwa madhumuni ya kuoneshwa hadharani”.

Mhe. Spika, kwa kweli hivi sasa masuala ya filamu tunayo mengi kwenye maduka, kwenye maghala na mengine yanarikodiwa hapa hapa nchini kwetu na mengine nje ya nchi. Kwa hivyo, utakuta filamu hizi zinakuwa na picha mbali mbali ambazo nyengine zinaelimisha lakini nyingi zao zinapotosha. Kwa kuwa picha hizi zimeshakuwa nyingi nchini kuzifanyia ukarabati au kuzichunguza ni kazi nzito.

Ningemuomba Mhe. Waziri anayehusika na wizara hii akashirikiana na watu wa sheria labda kama mtu ataleta picha iliyokuwa haina maudhui nzuri au filamu ile haina picha za kuleta utamaduni wetu, ni picha za mafundisho mabaya basi iwekwe kanuni au sheria ya mtu yule kupewa adhabu ikiwa ya faini au ya kifungo, hapo ndio kidogo utaondoka huu utaratibu wa kuleta filamu zilizokuwa si nzuri kwa maadili ya wananchi wetu.

Vile vile kuna baadhi ya vyombo vyetu vya habari wakati mwengine kama walivyosema baadhi ya wajumbe hapa huwa wanateleza wanaonesha picha ambazo si nzuri kwa maadili yetu ya Kizanzibari kwa kuangalia na familia ndani ya nyumba. Kwa hivyo, wale wafanyakazi wa vyombo vyetu vya habari wawe makini pale wanapozionesha picha zile, kwanza wazipitie na kuziangalia vizuri wasirushe tu watakuwa wanaharibu maadili na mila za Kizanzibari.

Mhe. Spika, ingawa tumezidiwa na mitandao mbali mbali na mipango ya kimaendeleo lakini kama tutayakemea huenda tukapata afuweni ya kupunguza na kuwafanya vijana wetu wafuate maadili yetu na mila za Kizanzibari. Kwa kweli hatua iliyofikiwa kwa watu wetu si nzuri, wamekuwa hawana nidhamu, heshima hata akija mgeni tofauti na ripoti za nyuma jinsi Zanzibar ilivyo na sasa unaikuta imegeuka iko vyengine. Kwa hivyo, kama kutakuwa na utaratibu huu utasaidia angalau kuweka sawa matatizo mbali mbali yanayotaka kujitokeza kwa vijana wetu hawa.

Mhe. Spika, nakuja katika suala la muundo wa bodi ukurasa wa 230 kifungu cha 5. Hapa ametakiwa Mhe. Waziri kuunda bodi baada ya Wajumbe waliokuwepo na kuteuwa Wajumbe wengine wasiozidi 6.

Mhe. Spika, hapa katika muundo wa bodi huu ningetoa maoni yangu uangaliwe sana katika kuunda bodi hii ambayo iwe na watu mashuhuri na wale waliokuwa na uzoefu ambao wameshaona mengi na wameshasikia mengi kwa mfano wawemo angalau wakuu wa dini, aweko Mkuu wa Mkoa aweko mwanasheria japo mmoja au mtungasheria Mwakilishi japo mmoja na mtu mzima mwanamama ambae ana umri unaostahiki kutulia na kutoa mawazo katika kuimarisha bodi hii. Pindipo itaundwa bodi hii kwa mtizamo huo naona kutakuwa na mchango mzuri katika kufuatilia masuala haya ya kuimarisha mila, silka na utamaduni wetu Zanzibar. Mhe Spika, uundwaji wa bodi hii utasaidia pindipo yatafuatwa maagizo kama haya.

Mhe. Spika, ukurasa wa 232 kifungu cha 15 (b) utafutaji wa fedha. Pindipo bodi hii itaundwa kwa mujibu wa mitandao jinsi walivyoiandika katika gazeti hili kwenye njia ya utafutaji wa fedha, nafikiri itakuwa ni rahisi na kufanikiwa katika michango yao mbali mbali. Kama inavyoeleweka mipango hii ya filamu ya Utamaduni ina nyezo nyingi kwa ajili ya fedha na mahitaji mbali mbali, kwa

mfano kama uagiziaji wa kanda na mambo ya *Video* ikiwa yamo katika sehemu yao itakuwa katika mambo ya mapato na TRA ikiwa wako karibu nao. Nafikiri huenda wakapata chochote kile kinachoingizwa kanda hizi ili kusaidia bodi hii.

Mhe. Spika, katika mipango mbali mbali ya uanzishwaji wa vikundi vya sanaa au mambo mbali mbali vijijini au pindipo bodi hii itaunda watu maalumu kufuatilia itakuwa ni rahisi kupata michango mbali mbali ya kusaidia katika bodi hii ya uanzishaji wa Sanaa, Mila, Utamduni na Filamu.

Mhe. Spika, mimi mswada huu kwa kushirikiana na wananchi wangu wa jimbo la Amani naunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Ahsante Mhe. Spika na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo. Kwa hakika mchango wangu mimi hautokuwa mkubwa sana, baada ya wenzangu asubuhi ya leo kuogolea sana katika mswada huu. Mhe. Spika, mimi nimesimama kuzungumzia jambo muhimu sana ambalo nimeona na mimi nitie baraka zangu kidogo.

Kwanza, nataka nianze na eneo la madhumuni. Mhe. Spika, mswada huu unasema kwamba umekusudia kulinda na kuhifadhi mila, silka, tamaduni na maadili ya Mzanzibari. Na kwamba sanaa haitimiki kupotosha maadili hayo. Mimi kwa maoni yangu neno kulinda hapa limechelewa sana ilipaswa labda iwe unakusudia kufufua na kuhifadhi mila, silka na utamaduni wa Mzanzibari.

Mhe. Spika, kulinda tumechelewa tayari mila na desturi zetu zimeshapata mmong’onyoko mkubwa. Kwa hiyo, hauhitaji kulindwa huo mmong’onyoko wenyewe ikiwa tutalinda kwa kweli hatotukuwa tunafanya jambo la maana. Kwa mswada huu au mswada mwengine lakini panahitajika sasa kufufua na kuhifadhi mila. Mhe. Spika, kwa kweli tuko katika hali mbaya sana na kama walivyosema waliotangulia lazima tujiulize walifikaje katika hali hii. Mabandiko yanaonesha kwamba shughuli za filamu Zanzibar zimeanza miaka ya 1910. Baada ya vita vya kwanza vya dunia masuala ya filamu yalianza kwa kasi.

Mhe. Spika, utawala wa wakati huo maandiko pia yanaonesha kwamba miaka ya 1920 na mwaka 1930 taasisi za kufanya sensa za filamu zilianzishwa miaka hiyo. Sasa kumbe ilikuwa inaonesha kwamba Zanzibar ilikuwa inasheria za *decree* ambazo zilikuwa zinafanya uhakiki wa filamu tokea wakati huo. Suala la kujiuliza inekuaje kama kuanzia miaka hiyo mpaka leo karibu miaka 90 kumbe tuna taasisi au vyombo vilivyowekwa kisheria vya kudhibiti mambo haya. Lakini leo tunajikuta mila, silka na utamaduni wetu umemong’onyoka kiasi cha kutisha sana.

Mhe. Spika, kumbe si taasisi tu ndio inayohitajika kwa sababu kama taasisi kuanzia mwaka 1920 zilikuwepo. Na kwamba hata tunaanzisha bodi hii maana yake si tu ambayo inahitajika kulinda mila na tamaduni zetu. Sasa hili ni jambo ambalo Mhe. Spika, wizara ingeliweza kulifikiria kwa umakini zaidi ili tusiwe tunakimbilia kuanzisha taasisi tu. Lakini lazima tuangalie mambo mengine ambayo ndio sababu zake.

Mhe. Spika, tumefika pahali pabaya sana hivi leo tunamwona kijana wa kiume wa Kizanzibari amesuka nywele ni jambo la kawaida sana. Mshamba kama mimi ninaetoka Gando nikishangaa shangaa watu wataona huyu bado hajastarabika. Kwa kweli, mtihani utakuta vijana wengine wanamalemba makubwa sasa, mimi huuliza ile ni nini huambiwa zile ni nywele ilimradi ni rasta wamezifinyanga ndani ya kichwa na hawa ni watoto wetu kabisa Mhe. Spika.

Sasa mimi nahisi kwamba tuna hali ngumu sana. Kama walivyosema wenzangu bodi itakuwa na kazi moja pevu na sidhani kama wataweza kumudu tatizo hili. Lazima kwa maoni yangu wazazi jamii yenyewe na serikali kwa jumla tubadilishe mtazamo wa jumla. Wazazi tuna jukumu kubwa, jamii pia na serikali nayo ina jukumu kubwa zaidi. Haya mambo matatu lazima yafanywe kama mafya, yaani kuwe na utatu wa pamoja baina ya wazazi, jamii kwa jumla na serikali. Vyenginevyo hatufiki na tutaendelea kuharibikiwa sana.

Mhe. Spika, nitoe mifano miwili mwaka mmoja uliopita pale Wete kupitia hii meli inayoteremkia Wete. Mhe. Spika, waliteremka wazungu kama wanne, wawili wanawake na wawili wanaume. Wale wanawake mavazi waliovaa ilikuwa ni mtihani kidogo wana kivazi cha juu kidogo na cha ndani kidogo na halafu wana kama kanga, lakini ni nyepesi kile kivazi cha ndani unakiona. Jamaa wakasema hawa wasiingie mitaani ikawa vurugu kidogo. Vurugu yenyewe ikabidi wakatoka jamaa pale wakenda nao mpaka Makao Makuu wa Polisi pale wakasema hawa kuingia hivi hapa petu haiwezekani. Ikabidi O*CD* alipowaona akasema kweli haiwezekani. Kwa hivyo, wakaamriwa wale wanaume zao wakanunue kanga pale nne waje wajifunge moja juu na moja chini, halafu wakaambiwa haya nendeni. Sasa kidogo ilitoa funzo mimi nafikiri huwa wanaambiana. Siku hizi si nadra kuwaona wazungu pale Wete wakiwa katika hali mbaya.

Mhe. Spika, lakini baada ya muda mfupi tena ikatokea jambo jengine kubwa katika Hoteli ya Wete, ilivumia jioni moja kuna shughuli moja kubwa na adhimu. Nikauliza shughuli gani, nikaambiwa kuwa wanaume wawili wanakuja kuoana. Nikauliza tena hawa wanatoka wapi nikaambiwa wanatoka Mombasa, wameamua kuja kuifanyia hapa Wete harusi yao, basi jamaa wakasema kuwa hii harusi isifanyike hapa vyovyote itakavyokuwa na ikawa kuna vurugu kubwa

hatimae harusi haikufanyika. Lakini wenyewe wakenda polisi shughuli yao imeharibiwa wametutia hasara kwa kweli ikabidi kuna kesi na hadi hivi leo wale waliosababisha harusi ya wanaume wawili kuharibika wana kesi Mahakama ya Wete.

Sasa hapa pana tatizo kidogo kwamba jamii inajaribu kuzuia yale ambayo mila, desturi na silka zetu hairuhusu. Lakini vyombo vya dola bado, sasa nasema kwamba haya ni mambo yanahitaji ushirikiano mkubwa.

Mhe. Spika, baada ya dibaji hiyo nina mambo muhimu sana ambayo ninataka niyachangie ndani ya mswada.

Kwanza, mimi ningeishauri bodi hii wakati wanaangalia hizi kanda au filamu wawe wanazipa *group*, wenzetu wanafanya hivyo mfano nchi ya Ireland ni moja ya nchi ambayo imejitahidi sana kukinga jamii yao kutokana na uvamizi wa jamii nyengine, na wanafanya hivyo kwa sababu Waingereza pale kama ni kiongozi wa nchi zile pale. Kwa hivyo, hujaribu kutoa zile tamaduni zake ziwe zinaigwa na nchi zile. Sasa hapa Ireland wanajaribu sana kuzuia.

Katika hilo wana chombo madhubuti sana cha hii ya Bodi ya Sensa na wanajaribu mara zote kuhakikisha kwamba filamu zote zinazooneshwa pale zimepewa vikundi. Mfano lazima filamu iwe na *group* mmoja katika tano huwa wanabandika ukiona *"G"* hiyo huwa ni *General* kila mtu anaweza kuiona, wakiandika *"PG"* maana yake hiyo ni chini ya umri wa miaka 12 wanaweza kuona, wakiandika *"12A"* zaidi ya miaka 12 wanaweza kuiona wakiandika *60A* zaidi wa miaka 15 na 18. Sasa wanajaribu na kwa kweli wamefanikiwa kidogo na filamu yoyote itakayoonekana haina alama zozote hilo ni kosa la jinai na mtu anaweza kufikishwa mahakamani na ikithibitika, basi anatozwa faini au kifungo.

Mhe. Spika, kwa hali ambayo imetufikia sasa Bodi hiyo kwa kweli kama walivyosema wenzangu sijui watatumia utaratibu gani. Lakini wana kazi moja ngumu na kubwa kama watataka wafanikiwe.

Mhe. Spika, kifungu 4 (c) kinasema kwamba filamu zote zinazorikodiwa ndani na nje ya Zanzibar zinapata usimamizi wa Bodi wakati wa kurikodi ili kulinda maadili na utamaduni wa visiwa vya Zanzibar. Mhe. Spika, hii ni kazi ambayo ni ngumu haiwezekani mambo yanafanyika katika mahoteli ya kitalii ya ajabu ajabu huko na wao watakuwa na mkono gani mrefu wa kuona.

Mhe. Spika, nitoe mfano mara moja waliambiana jamaa leo tuna filamu safi sana kutoka nyumbani njooni tuangalie. Wakajikusanya katika ukumbi wanaangalia filamu kutizama ile filamu ni kanda iliyopigwa Zanzibar na

mmoja waliorikodiwa ni dadaake baba mmoja na mama mmoja yuko kama alivyozaliwa  na mtu wa miaka 30. Sasa nilikuwa najiuliza Mhe. Spika, kuhakikisha kwamba filamu zote zinazorikodiwa ndani na nje ya Zanzibar zinapata usimamizi wa Bodi wakati wa kurikodi ili kulinda maadili na utamaduni wa visiwa vya Zanzibar.

Mhe. Spika, Bodi itakuwa na mkono gani kuhakikisha kwamba kila ambalo linafanyika wanalihakiki. Kwa kweli, nahisi kwamba  ni jambo zito na ambalo litakuwa utekelezaji wake hauwezekani.

Pili, kufanya uhakiki wa maonesho yote yanayohusu michezo ya kuigiza na burudani nyengine zote za sanaa. Hili nalo si jambo rahisi wanaweza watu wakafanya uhakiki. Lakini wakati wanafanya kwenye *hall* ilitokea katika nchi ya *Qatar* wanajitahidi sana, lakini mara moja walihakiki kikundi cha sanaa kikaruhusiwa wakati wako katika *hall* yule mama aliekuwa anaonesha ile michezo akaanza mambo ya ajabu ambayo bodi haikuyaona. Lakini yuko katika *hall* akaanza kufanya mambo ya ajabu ikiwa mtihani mkubwa. Baadae walipoulizwa walisema kwamba huyu alikuwa mlevi na siku hiyo alikuwa amelewa, lakini siku ya bodi alikuwa hajalewa.

Mhe. Spika, najiuliza sasa na sisi Zanzibar itakuwaje, ulevi Zanzibar upo mwingi nimeambiwa sina hakika na hili naweza kurekebishwa rikodi ya kiwanda cha bia cha Dar es Salaam inaonesha kwamba mambo ya bia baada ya Mkao wa Dar es Salaam unaofuatia ni Zanzibar. Sasa ikiwa ulevi ndio sababu ya mambo haya sasa Zanzibar sijui na ikiwa habari hii  niliyoambiwa ni kweli sijui tuko wapi Mhe. Spika. Kwa hivyo, bodi hii ina kazi kubwa.

Kifungu (f) kinasema kutoa miongozo ya jumla kuhusu uoneshaji bora ya michezo ya kuigiza na burudani nyengine. Hapa pana tatizo na jambo gumu. Mfano, mmoja Mhe. Spika, kama miezi minne iliyopita nilisafiri na boti ya Sepider kutoka hapa kwenda Pemba asubuhi,  kufika pale baada ya muda kuondoka tumeshafika Bet-el Ras ikatiwa filamu moja, kuangalia ilikuwa ni hatari kubwa yaani Mhe. Spika, kama umekaa wewe na mtu unaemstahi, lazima utaondoka katika boti hii yetu hapa. Sasa mimi nikautizama ule mkanda nikawaendea mimi mwenyewe nikawauliza, jamani hii vipi nani anahusiana na habari hii. Kwanza nikajitambulisha mimi ni Mwakilishi nikawaomba watoe. Nikajibiwa kuwa kamuone bosi. Nikenda huku mchezo unaendelea huko chini baada ya nusu ya mchezo tukakubaliana na bosi kwamba mchezo utolewe na ukatolewa.

Sasa tatizo ni kwamba mchezo ule ulirikodiwa Dar-es Salaam pale pana vikundi vingi vya kurikodi na tutake tusitake pamoja na udugu mkubwa tulionao na wenzetu, lakini kuna mambo mengine ya mila tunatafautiana. Kuna

mambo mengine kwa wenzetu ni ya kawaida na kwetu ni matusi huo ndio ukweli wenyewe. Bodi ya Sensa iliyoko Dar – es Salaam kama wanafanya hii kazi kwa mujibu wa taratibu zao wanaona kwamba hili jambo ni la kawaida, lakini kwa kwetu sisi ni tusi. Sasa na hili ni jambo limeshazoeleka hata mimi mara moja nilikuwa katika mkoa mmoja sipendi kuutaja napita na mwenyeji wangu tukasikia zogo akanambia tupite hapa tuone tukaona kuna ngoma ya kuchezwa mwari anatolewa nje. Kwa kweli, nikastaajabu sana yaani yule binti vile alivyo pana baba, mama, mjomba kuna watu wake wa karibu nao kumuangalia ni jambo la kawaida. Lakini sisi kwetu huwezi kuona maungo yale ya mwanao au mtoto wa karibu yako haiwezekani, lakini kwa wenzetu ni jambo la kawaida silka na mila zao inaruhusu.

Sasa mchezo kama ule ukiingizwa katika boti ukioneshwa baina ya Pemba na Unguja mtihani mkubwa hatuwezi kukubali. Sasa hii boti itakuwa na uwezo gani wa kudhibiti mambo kama haya. Kwa hivyo, nasema kwa kweli kuna tatizo kubwa sijui wataanza wapi na wamalize wapi. Lakini majukumu waliyopewa kwa kweli ni jambo ambalo sijui tutafanyaje tuna mtihani mkubwa.

Mhe. Spika, na mimi naomba niseme kama walivyosema wenzangu katika kifungu cha 5 Mwenyekiti lazima sifa yake iwekwe vizuri. Ni jambo moja finyu mno wenzangu wamesema na kwa sababu ya uzito wa chombo hiki na mwenyekiti ambae kakiongoza hatutaki mtu awe wa kubahatisha, lazima sifa yake iwe inaeleweka. Kwa hivyo, kusema uelewa tu kwa kweli atashindwa kufanya kazi ambayo tunahitaji afanye na kwa kweli lazima awekewe sifa ambazo zinaweza kutumika vizuri, si mambo ya uwelewa kwa kweli kama unaweza kuyapima.

Halafu Wajumbe wengine wasiozidi 6 watakaoteuliwa na waziri kutoka mikoa ya Zanzibar walio mahiri katika taalamu ya utamaduni na sanaa. *Wallahi* sijui wenzangu, lakini kigezo cha umahiri wa jambo ambalo pia ni kigezo ambacho kinaweza kupimwa kwa mtu anavyotizama, ni vizuri pakawekwa kiwango cha taaluma umahiri ni mtizamo mtu unavyomwona, lakini hauwezi kipimika vyenginevyo. Kwa hivyo, na hata hapa ningeshauri Wajumbe wawekewe sifa za kitaalamu ambazo zinaweza kutumika vizuri. Lakini na hata hao Wajumbe wenyewe ni vizuri wakaangaliwa nao hawajapata mmong'onyoko wa maadili au mengine. Kifungu cha 7 (b) waziri anaweza kutengua au kusimamisha uteuzi wa Mjumbe yoyote aliemteuwa chini ya kifungu cha sheria hii (b) kutokana na tabia mbaya au mwenendo mbaya. Hapa nilikuwa najiuliza nini kigezo cha mwenendo mbaya au tabia mbaya, pengine watasema kwamba labda ni mlevi, lakini kwa wengine ni tabia nzuri akaona yeye anaelewa. Kwa hivyo, ataona si tatizo au mzinzi unaweza kusema ni tabia mbaya, lakini kwa

mwengine ambaye ni mzinzi ataona si tatizo. Wizi kwangu mimi pengine nitasema ni tabia mbaya lakini aliye fisadi anaona si tatizo.

Mhe. Spika, nasema kwamba kutokana na mwenendo mbaya mimi ningeona kifungu hiki hakina maelezo ambayo kinaweza kupimika. Mhe. Spika, ujue kwamba hii ni sheria na kama tunatunga sheria tusiweke *provision* ya kumuwezesha waziri akatumia nafasi yake kiajabu ajabu. Anaweza kusema huyu bwana nimuondoe kwa sababu ya tabia mbaya, sasa tabia mbaya vipi, kwa kweli tabia mbaya au mwenendo mbaya. Nafikiri hapa kifungu hiki kingeondoka kingetafutiwa utaratibu mwengine, au pakafanywa *definition* ya tabia mbaya au mwenendo mbaya, tusiweke mambo hivi ya kijumla jumla ambayo yanaweza yakatumika vibaya.

Halafu Mhe. Spika, naomba kunukuu kifungu cha 13 (1) kinasema:

Kifungu cha 13 (1):

> "Kutakuwa na Afisa Mtendaji wa Bodi ambaye atateuliwa na Waziri."

Mhe. Spika, tumezoea katika sheria zetu watendaji hawa kuteuliwa na ama Waziri au Rais. Mimi nahisi tungebadilika sasa, ushauri wangu tungetangaza nafasi kama tunahitaji Afisa Mtendaji wa Bodi ya Sensa halafu Wazanzibari wanaojihisi wana sifa waombe, ikesha bodi ichague. Nafikiri huo ninaopendekeza ni utaratibu mzuri, Afisa Mtendaji atawajibika kweli kwa bodi, atajua kwamba nikifanya mchezo bodi itaniondoa itaweka mtu mwengine mwenye uwezo na mchapa kazi. Lakini Afisa Mtendaji anayeteuliwa na Waziri au Rais, bodi inaweza ikawa inanung'unika tu meneja hivi, meneja hivi, wakawa wanapoteza muda wanashindwa kum- *convince* Waziri au Rais amuondoe mtendaji ambaye hafai au ni mzembe.

Kwa hivyo mimi ushauri wangu ni kwamba nafasi hizi za utendaji vijana waliosoma wapo zitangazwe watu waombe, bodi itaangalia mtu aliyekuja kama ana sifa wamuajiri, wakiona anafanya uzembe hafai watamfukuza. Sasa huu ni utaratibu ambao wenzetu wanafanya, lakini sisi bado tunalea ukale wa kwamba Waziri au Rais ateue watendaji. Kwa kweli tunapata matatizo kiutendaji, tunapata uzembe na bodi inakuwa dhaifu katika kuweza kumdhibiti mtendaji ambaye hatoi yale ambayo sheria inazungumza atoe. Mhe. Spika, huu ni ushauri nafikiri tungebadilika.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo na mimi nimuunge mkono Mhe. Zakiya Omar Juma kuhusu suala la kutoa ruhusa za mambo ya burudani wakati nyeti. Ni vizuri burudani zianze labda baada ya sala ya Ishaa. Lakini utaona wakati mwengine magoma yanapigwa msikiti huo hapo hujui adhana, hujui dua,

almuradi mtihani moja kwa moja. Mhe. Spika, sijui jambo gani linatupa mashaka kwetu sisi. Ni kweli baa ni nyingi zimetuzunguka hasa hapa Unguja Mjini. Hili jambo labda tuje kulizungumza siku nyengine. Lakini basi zishauriwe angalau baada ya sala ya Ishaa ndio mapigo yaanze, wapige wanavyotaka mpaka saa nane au alfajiri haya. Mhe. Spika, kuna watu wengine wapo msikitini wameshafanya mambo mengi huku nyuma, wengine wameshakuwa watu wa ngoma sana kwa hivyo wapo pale angalau wanatubia, ukimpitishia ngoma wakati ule unamkumbusha nyuma kidogo inakuwa mtihani.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu nitoe mfano mmoja. Siku moja Pemba ilipita shangwe ambayo ni ngoma inayopigwa na zumari, ikapita msikitini mwadhini kishaadhini bado kukimu na kusali. Sasa mmoja aliyekuwemo msikitini ni mpiga zumari mzuri sana, safi sana siku za nyuma, akaisikiliza zumari inakuja, akasema huyu anayepiga hii zumari kaikosea haipigwi hivi. Sasa waliomo msikitini wanamuona jamaa anahamanika wanaulizana vipi huyu? Kila ikikaribia msikitini mshawasha unampanda zaidi anaona vile vidole vyake anavyoipiga sivyo anaharibu ile *tune* inavyotoka. Basi jamaa kidogo wakamuona kishakuwa nje ya msikiti, kutahamaki jamaa yumo ndani ya shangwe, alimnyang'anya jamaa yule akaanza kuipiga yeye kwa kweli siku ile hakupatikana. Sasa nakusudia kusema kwamba wale waliomo msikitini wakati mwengine huwa ni watu ambao wameshaanza kutubu lakini huku nyuma wameshafanya mambo mengi ya ajabu. Sasa tukiwapitishia mambo karibu yao tunawarudisha nyuma, ile toba yao yote inavurugika. Kwa hivyo tunaiomba sana bodi hii ijaribu kuangalia hilo kwamba ruhusa za kufanya burudani sawa lakini waangalie ule wakati ambao kidogo watu wanatubu ipunguze.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo na mimi nitie nyama kidogo ni suala la bodi kuwezeshwa. Kama tulivyosema na wenzangu wengi wamesema, bodi hii ina majukumu mazito na kwa kweli tunaitazamia itakapoanzishwa baada ya huu mswada kupita, basi iwe inafanya kazi kwa sababu hatuhitaji kukinga tunahitaji kufufua. Kwa hivyo hawawezi kufufua hawa ikiwa hawana nyenzo, nyenzo kubwa ni fedha.

Kifungu cha 15 (a) naomba kunukuu kinasema:

Kifungu cha 15 (a):

> "Ruzuku ya Serikali itakayoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi."

Mhe. Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri anayehusika na mswada huu kwanza ajaribu kufanya bajeti ya bodi iwe nzito kidogo. Maana wakati mwengine huletewa hapa bajeti ya kitengo au idara ikawa ni haba sana. Sisi

huulizana jamani bajeti hii atamudu kweli huyu, hata apewe yote lakini kwa kweli huwa ni ndogo sana. Sasa katika haya masuala ya bodi bajeti itakayoombwa iwe kidogo imechuchuka, asikubali *ceiling* sana katika suala hili. Kwa sababu hili suala linahusu hasa vizazi vyetu vinavyokuja. Kwa hivyo bajeti atakayoipanga ikwepe ule ukomo, asiambiwe punguza, kwa hili namuomba awe mgumu apunguze sehemu nyengine. Lakini katika Bodi ya Sensa tuna kazi ambayo tunahitaji fedha.

Mhe. Spika, la pili ningemuomba Waziri wa Fedha mkono wake uwe wazi katika hili ili bodi iwe na uwezo wa kufanya kazi. Vyenginevyo tutaunda bodi hapa tutakapofika yale yale hamna pesa, kifungu hakijaingiziwa pesa, sasa hawawezi kufanya kazi. Mhe. Spika, kadri ambavyo watakuwa hawana nyenzo maana yake ni kwamba tutaendelea kuwa na hali mbaya zaidi ihusuyo mila na utamaduni wetu.

Mhe. Spika, mimi nilisema sina mchango mkubwa kwa sababu wenzangu wameshazungumza sana. Ila niseme kwamba hili ni suala ambalo linatuhusu sote. Kama nilivyosema mwanzo sisi kama wazazi tuna jukumu kubwa, jamii kwa jumla ina jukumu kubwa, serikali nayo ina jukumu kubwa zaidi. Vyombo vya kutunga sheria navyo vina jukumu kubwa na pana, vikiwaonea haya, vikiona muhali kwa kweli tutaendelea kuharibikiwa. Tumeshaharibikiwa sana na hatuhimili kuharibikiwa zaidi. Jamii ambayo haiwezi kulinda mila na tamaduni, kwa kweli ni jamii iliyopotoka na ni mtihani mkubwa.

Sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna nafasi kubwa ya kuona kwamba mila na utamaduni wa Zanzibar umerudishwa. Mhe. Spika, Mhe. Haji Faki Shaali alisema kwamba Mhe. Mohammed Ali Salim tunapokwenda nje ajitahidi kuonesha kwamba yeye ni Mzanzibari. Lakini hata Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo nae ajitahidi sana. Tulikwenda naye safari mara moja na tulikaa kama siku saba, lakini siku tano tulizokaa alivaa koti na kanzu ya Kizanzibari. Labda ni kwa sababu ni waziri anayetokana na wizara hii, lakini nafikiri ni kwa sababu ya tabia yake ya kuona kwamba anaupa hadhi Uzanzibari. Kwa hivyo hili ni jambo ambalo ninahisi tuliige sana.

Waganda na wao wana kanzu yao bila ya kofia na huwa hawaoni haya wanaipiga muda wote. Kwa hivyo na sisi vazi letu la Kizanzibari lazima tulipe heshima na nafasi yake. Mhe. Spika, nakushukuru.

*(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 22/01/2009 saa 3:00 asubuhi)*